ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali Mfenesini.	Naibu Spika/Jimbo la
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee Kuteuliwa na Rais.	MBM/Waziri wa Fedha/
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.

10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na

	Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.

28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi Biashara, Masoko/Jimbo la Fuoni.	Naibu Waziri wa Viwanda na
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mpendae.	Naibu Waziri wa Mifugo Uvuvi/Jimbo la
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake

44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 04 Juni, 2014

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Waziri wa Afya): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 72

Malipo kwa Daktari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwanza naomba uniruhusu nikupe pole kutokana na hali yako, nakuona kama hali yako kidogo leo sio dhahiri kidogo. Vile vile Mhe. Spika, naomba uniruhusu kwa dakika moja tu kwa heshima na taadhima ya hali ya juu. *(Makofi).*

Ahsante sana Mhe. Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kumshukuru Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake, umahiri wake na ufuatiliaji wake katika Baraza hili la Wawakilishi. Jana alitoa kauli nzuri ya kuwaridhisha *backbenchers* kwa Mawaziri na Manaibu wao wanapoulizwa maswali, wawe na uhakika wa kujibu, na wajuwe nini wanachokijibu. Sio kuja kujibiana majibu ambayo hayana uhakika humu ndani. Namshukuru kwa dhati kabisa kwa kufuatilia hilo, na likiwemo lile tulilolipigia kelele la wanawake kujifungua. Nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kufuatilia. *(Makofi).*

Baada ya maelezo hayo naomba Mhe. Spika, nijibiwe swali namba 72 ambalo linawahusu wananchi wa Jimbo la Muyuni na ndio walionileta hapa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili alipokuwa akijibu swali la wananchi wa jimbo la Muyuni kuhusu kulipwa mafao yake ya miezi mitano (5) kwa daktari aliyejitolea wa Muyuni, ambapo Serikali iliahidi kuchukua jukumu la kulipa fedha hizo alizolipwa daktari huyo na wananchi.

(a) Je, kauli hiyo aliyotoa Mheshimiwa Waziri ni lini itatekelezwa kwa vitendo.

(b) Ni muda mrefu sana umepita hakuna jawabu la malipo hayo na karibu Shs. 1, 250,000/- zimetangulizwa kulipwa kwa daktari huyo, Serikali haina uwezo wa kumlipa daktari huyo.

(c) Lini daktari huyo aje achukue haki yake iliyotokana na kazi ya kuokoa wananchi afya zao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam. 72 lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba daktari huyo ambaye alifanya kazi nzuri kwa muda mrefu, haki zake zote anazodai serikali kwa mujibu wa taratibu za kisheria atalipwa haki hizo.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana daktari huyo ambaye alifanya kazi ya kujitolea kwa kipindi chote alichosaidia kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Muyuni.

Mhe. Spika, serikali yetu kwa kuthamini mchango alioutoa daktari huyo pamoja na umuhimu wa wananchi wetu kuweza kupata huduma za afya, serikali imemuajiri kwa mkataba wa miaka miwili daktari huyo kuanzia tarehe 7 Disemba, 2013 na kuanzia kipindi hicho daktari huyo ameanza kulipwa mshahara wake.

Mhe. Spika, kama alivyoelezea Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba daktari huyo kwa kipindi chote alikuwa anajitolea na serikali haikuwa na mkataba wowote na daktari huyo, hivyo serikali haina vigezo vyovyote vya kuweza kufanya malipo hayo katika kipindi chote alichojitolea. Pia ikumbukwe kwamba mtu anapojitolea huwa hastahiki malipo yoyote, bali huwa na nia

njema ya kusaidia jamii kutokana na uzalendo na imani kubwa kwa wananchi wenzake.

Napenda nirudie kutoa shukrani za dhati kwa daktari huyu na madaktari wengi pamoja na watendaji wote na wananchi wote wenye moyo wa kujitolea. Aidha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anatilia mkazo sana suala la kujitolea kwa wananchi kwa kuwa ni njia moja muhimu inayoimarisha kasi ya maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini mwaka jana Disemba 2011 lililetwa hapa Barazani swali nambari 45. Naomba ninukuu haya maneno sio yangu ni ya Mhe. Waziri, kama nitakosea nakuomba radhi kabisa ndio uungwana. *(Makofi)*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:- "Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo.

Napenda nirudie kwamba serikali hii. Narudia tena. Napenda nirudie kwamba serikali hii Waheshimiwa nia yake ni kutenda haki, na siku zote kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata haki zao, lakini kwa mujibu wa sheria zilizopo haki zote za daktari huyo zitalipwa kwa kufuata utaratibu".

Tayari daktari keshajitolea karibu miezi sita. Haya maneno ni ya Mhe. Mohammed Aboud sio yangu mimi. Sasa ukweli sijui uko wapi, kama serikali imeshindwa kulipa shilingi 1,250,000 basi itamke hapa hapa hiki ni chombo cha wananchi, sio aibu. Haya sio maneno yangu, ikiwa kiongozi kama Waziri anatoa kauli kama hii. Je, mawaziri wengine watakuwa na mfano gani?

Swali ni lini watamlipa daktari huyu haki yake, haya sio maneno yangu ni yeye mwenyewe alisema haki zake atazifuatilia ili zilipwe, lakini mpaka hivi leo mwaka mzima huu unakwenda zake, haya ni maneno yake Mhe. Mohammed Aboud, hii ni *hansard* yake. Ikiwa yeye ni Waziri kioo, manaibu waziri watafanya nini, watajibu hivi hivi tunavyotaka kujibiwa humu ndani.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, swali lako ni nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Alipwe haki yake tu basi hakuna tatizo lolote, aniambie ni lini atampa?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, maelezo yake Mhe. Jaku Hashim Ayoub na maelezo yangu yako *very clear*, na kwa mtu yeyote mwenye maarifa na akili anaelewa majibu yangu. Nilisema

serikali hii haitomdhulumu mtu yeyote yule mwenye haki yake, kwa mujibu wa sheria atapata haki hiyo, na kama kuna haki zozote za daktari huyu zitalipwa kwa mujibu wa sheria.

Vile vile ninachosema nampongeza daktari huyu kwa imani yake kubwa ya kujitolea kwa nchi yetu na imani hiyo ameweka *record* nzuri sana, na wananchi wote wanaojitolea basi wajue wanaweka *record* nzuri sana katika nchi yetu. Kwa hivyo, nawapongeza sana watu hawa, akiwemo daktari huyu.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama kuna haki yake kwa mujibu wa sheria zioneshe haki zake hizo, atuandikie rasmi zipi ambazo anazilalamikia za kisheria, malipo yake yatapatikana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nikupe pole kutokana na baridi uliopata huko unakotoka, Mwenyezi Mungu akujaalie sauti yako itoke vizuri. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuwa sheria huyo daktari hana haki ya kuweza kulipwa hayo mafao yake.

Je, Mhe. Waziri huna hata sheria ya huruma ya kuweza kumlipa japo chochote?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nchi yoyote duniani inaongozwa kwa misingi ya sheria, haiongozwi nchi kwa misingi ya huruma. Kwa hivyo, tunapofanya shughuli zetu hapa tunafanya kwa misingi ya sheria. Huruma mimi nitakuwa nayo sana, pale nitakapokuwa na fedha kama Mohammed Aboud niko tayari kumsaidia daktari huyu, lakini kama sina nitafanya nini, taratibu zilizopo za kisheria ndizo ambazo zinamuongoza daktari huyu apate haki yake. Namuhurumia na nampenda, lakini huyu daktari mzuri hakusema anataka kuhurumiwa, amejitolea kusaidia wananchi wenzake, na sifa hiyo ipo, tutampa cheti kabisa cha kuonesha kuwa amefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri Mohammed Aboud mpiga kura wangu, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa nchi yetu na serikali yetu haina utaratibu wa kutoa nishani za utumishi uliotukuka kama ilivyo kwenye nchi nyengine zilizoko hata huko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Je, pamoja na kuwa huyu mtumishi kaitumikia serikali hii kwa muda mrefu na aliamua kujitolea, haoni Mhe. Waziri kwa sababu hatuna utaratibu wa kutoa

nishani ya utumishi uliotukuka, wakamfanyia angalau fungu dogo hivi, ambalo angelitamka sasa hivi hapa la malipo tu ya kiasi fulani ya kumtunukia ikawa ni kama nishani ya utumishi uliotukuka kwa wananchi wa nchi hii?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, inaonekana daktari huyu ametetewa sana na Waheshimiwa Wawakilishi wengi, lakini ningependa wawatetee na madaktari wengine wote, madaktari wote wanafanya kazi nzuri katika nchi hii. Kama ni nishani ni lazima tuwe *fair*, tutizame kila aliyefanya kazi nzuri apewe nishani na ni utaratibu wetu wa kutoa nishani. Kila mwaka sisi hutoa nishani maalum kwa wale wanaofanya kazi vizuri na *Inshaallah* tutatizama vigezo vya utekelezaji wa daktari huyu, ikionekana anapaswa kupata nishani basi atapewa nishani hiyo na kama unakuwa mfanyakazi bora basi kuna utaratibu wa tunza maalum zinatolewa.

Kwa hivyo, tutamtazama daktari huyu kama na yeye ni daktari bora kuliko hao madaktari wengine, basi tunza hizo atapata kwa mujibu wa taratibu zetu tulizojiwekea. Hatuwezi kuvunja utaratibu kwa sababu ya mtu mmoja.

Nam. 30.

Kubinafsishwa Baadhi ya Huduma Zinazotolewa na Shirika la Bandari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kumekuwa na mapungufu makubwa ya utendaji wa Shirika la Bandari kwenye eneo la kupakuwa mizigo; kunakosababishwa na ubovu wa mashine za upakuzi. Mapungufu hayo yanasababisha usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara kushindwa kupata mizigo yao kwa wakati, kwa vile makontena mengi yenye bidhaa yanalala bandarini yakisubiri kutolewa.

(a) Ni nani wa kulaumiwa kutokana mapungufu haya kati ya menejimenti au Bodi ya Shirika.

(b) Kama Shirika halina fedha ya kutafuta vifaa vya upakuzi, kwa nini huduma ya upakuzi isibinafsishwe au Shirika kutafutiwa mkopo wa fedha za kununua vifaa hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Shirika la Bandari yaani sheria nambari 1 ya mwaka 1997, imeelezwa wazi kwamba utawala yaani *management* na Bodi ya Wakurugenzi, wanafanya kazi kwa pamoja kwa msingi wa kuendeleza Shirika letu la Bandari na bandari zake zote.

Kwa hivyo, kwa namna yoyote kwenye mafanikio ama kwenye kasoro, vyombo vyote viwili hivyo vinahusika. Aidha, tatizo la wafanyabiashara kuchelewa kupata mizigo yao, inatokana na ufinyu wa eneo la kuwekea mizigo,yaani makasha, ambapo hivi sasa idadi ya makasha yanayopokewa katika Bandari ya Malindi ni zaidi ya uwezo wa bandari kuweka na kuyahifadhi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Bandari na taasisi nyengine za serikali, tunatafuta eneo ikiwa ndani au maeneo yanayozunguka bandari, ili kuweza kuongeza eneo la kuhifadhia mizigo hiyo.

Kwa kipindi hiki tayari Shirika la Bandari wameweza kujenga eneo la zaidi ya mita za mraba 10,000. Kwa malengo hayo hayo ya kuongeza eneo la kuhifadhia makasha, ikiwa ni baadhi ya majengo ama mabanda yaliyopo bandarini yaliyovunjwa kutimiza azma hiyo.

(b) Mhe. Spika, kwa upande wa utendaji, Shirika limeanzisha utaratibu maalum wa kumjazisha fomu mmiliki wa mizigo yake na kuweza kukabidhiwa bidhaa zake sio zaidi ya siku 3. Hata hivyo, kwa upande wa vifaa na zana za kutendea kazi, shirika linaendelea kujiimarisha hatua kwa hatua kwa msingi wa awamu kwa awamu, ambapo katika bajeti ya mwaka jana shirika lilinunua vifaa kadhaa, vikiwemo *Reach Stacker* moja, *Empty Handle*" moja na *Forklift* moja. Sanjari na hayo kwa mwaka huu Shirika limepanga kununua kreni mbili (2).

Aidha, fedha za kukamilisha miradi hiyo ni kutoka mapato ya ndani ama mikopo kutoka taasisi za kifedha, yaani benki.

Mhe. Spika, serikali bado haijaona haja ya kubinafsisha kazi hizo, kwani bado shirika inazimudu na vifaa vinapatikana hatua kwa hatua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali langu halikujibiwa, niliuliza humu na nimeandika Kiswahili, ndio yale nilioouliza mapema. Mawaziri kama hawana kauli za majibu basi watwambie watajibu kwa maandishi.

Nilichoandika ni nani wa kulaumiwa kutokana na mapungufu kati ya *Management* au shirika. Nilimsikiliza kwa makini alivyonijibu swali. Mimi nataka anijibu tu wa kulaumiwa ni Shirika au Bodi ya bandari, anijibu hapo tu. Nilimsikiliza kwa makini sana Mhe. Spika.

Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nilichomjibu kwamba kwa mujibu wa sheria nambari 1 ya mwaka 1997 iyoanzisha Shirika la Bandari imeeleza wazi, kwamba *management* kwa maana ya utawala na bodi ya wakurugenzi zinafanya kazi kwa pamoja. Kama kuna mafanikio ni yao wote, kama kuna mapungufu ni yao wote.

Sasa hatuwezi kuja hapa tukasema kwamba *management* ina makosa, bodi iko sahihi au bodi ina makosa *management* iko sahihi. Hiki ni chombo kimoja, hawa wanafanya kazi kwa pamoja. Wajibu wa serikali kama wizara ni kusimamia sera, lakini wao ni chombo kimoja, wote wanafanya kazi kwa niaba ya Shirika la Bandari.

Sasa sijui hayo majibu anayosubiri labda ashuke Mtume aje amwambie ndio amridhishe. Maana yeye kauliza kati ya *management* na bodi. Hawa wanafanya kazi pamoja, kama mazuri wanafanya pamoja, kama mabaya wanafanya pamoja.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi naomba niungane na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, katika kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa hotuba yake mwanana aliyoitoa jana ya kuweka wazi majukumu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na majukumu ya Mawaziri wanapokuja kujibu maswali mbali mbali.

Pia aliwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa makini na kufuatilia mambo mbali mbali, hadi wakati mwengine kuja na takwimu juu ya maswali yao. Naomba nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kufuatilia hayo na kuyatambua na kuyaona kwamba yanafanyika. Nimpongeze tena kwa kuwa sehemu ya karibu sana na Baraza hili kwa ufuatiliaji wake.

Mhe. Spika, naomba nimuulize pamoja na majibu mazuri Mhe. Waziri swali moja dogo tu, kuwa je Shirika la Bandari lina uwezo wa kisheria kupitia bodi yake kukopa moja kwa moja au lazima lipate idhini ya Wizara husika. Sheria inawaruhusu kukopa moja kwa moja kwa ajili ya kuboresha huduma zao za Bandari. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria namba 1 ya mwaka 1997 iliyoanzisha Shirika la Bandari na kwa mujibu wa *regulation* kwa maana ya kwamba kanuni ndogo ndogo masuala ya fedha na kibajeti yanalazimika kupitia kwa Mhe. Waziri ili kuweka baraka zake tupate tuendelee, lakini chombo hiki katika utendaji wa kazi hakifungiki kwenda kutafuta fedha ama mkopo au msaada, muhimu wanafanya

mawasiliano na Wizara ili kutambua na kuweka rekodi sawa sawa ili kuona kwamba utendaji wa Shirika na Wizara tunakuwa kitu kimoja.

Lakini taratibu za kibajeti za kimwaka ni lazima Waziri aweke *concern* yake ya kuweza ku- *prove* pamoja na malipo mengine yakiwa malipo ya utendaji ama malipo ya Wajumbe ya Bodi ya Wakurugenzi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza niwapongeze sana wafanyakazi wa shirika la bandari kupitia Mkurugenzi wake kwamba wanafanya kazi mchana na usiku kupakua mizigo, lakini kwa kuwa Waziri amekiri kwamba eneo ni dogo halitoshi kwa kuweka mizigo, ni lini hasa Serikali itaona kutafuta sehemu nyengine zaidi ili wapate kutoa mizigo na Bandari iweze kutosha ile iwe ya abiria na nyengine iwe ya mizigo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru na nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake isipokuwa hili naomba nilijibu mimi kwa sababu ya matokeo yaliyotokea hivi karibuni.

Kutokana na tatizo la mrundikano wa makontena suala hili lilichukuliwa kiserikali na wiki iliyopita Mhe. Rais alitembelea Bandarini na kujionea mwenyewe hali ilivyo, kwa hivyo maamuzi ambayo yamefikiwa mpaka sasa hivi kutokana na gharama za kuyasafirisha makontena nje ya eneo lile na hali halisi ilivyo ya uwezo wa shirika, na pia makontena yaliyokuwa yameshapakiwa mizigo kutaka kupakiwa tena kwenye meli inapofika tu na kupakua mizigo.

Serikali imeamua kwanza Shirika livunje baadhi ya mabanda yake baada ya kuwasiliana na Hifadhi ya Mji Mkongwe ili iweze kutanua eneo na kuendelea kubomolewa baadhi ya mabanda ya ghala yaliyopo pale mpaka pale nafasi itakapotosheleza kwa kipindi hiki ambacho tunangojea ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri, ahsante sana.

Nam. 4

Uhaba wa Kompyuta Katika Skuli ya Biashara – MOMBASA:

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanikisha dhamira yake ya kuendeleza vipaji kwa vijana pamoja na kutoa taaluma za aina zote nchini, imeamua kuanzisha mchepuo wa biashara wa Kompyuta katika skuli ya Serikali iliyopo Mombasa (Unguja). Kwa kuwa maabara ya Kompyuta katika skuli hiyo inazo kompyuta chache mno kwani hazizidi 20, kiasi ambacho zimezidiwa mno na idadi ya wanafunzi wa mchepuo huo waliopo katika skuli hiyo, jambo ambalo hupelekea wanafunzi hao kupata usumbufu kwa kufanya majaribio na mitihani yao kwa vitendo (*Practices on test and examination*) Katika Chuo Kikuu cha SUZA.

Je, ni lini Serikali itaondoa usumbufu kwa wanafunzi hao kwa kuimarisha maabara hiyo

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 4, kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Skuli ya Sekondari ya Mombasa, Unguja na Skuli ya Sekondari ya Chasasa, Pemba ni Skuli pekee zenye mchepuo wa Somo la Kompyuta katika kiwango cha elimu ya Sekondari. Skuli ya sekondari ya Biashara; Mombasa, ina jumla ya kompyuta 11, kati ya kompyuta hizo kompyuta 10 zilinunuliwa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, baada ya kuibiwa kompyuta 5.

Kwa upande wa Skuli ya Sekondari ya Chasasa ina jumla ya kompyuta 18, kati ya kompyuta hizo, kompyuta 10 zilipatikana kupitia mradi wa uimarishaji wa Elimu ya lazima baada ya skuli kufunguliwa rasmi mwaka 2013. Ni kweli kuwa idadi hiyo ya kompyuta haitoshelezi mahitaji ya wanafunzi wanaosoma somo hilo na hupelekea usumbufu mkubwa wakati wa ufanyaji wa mazoezi na mitihani. Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

a) Skuli ya Sekondari ya Chasasa itapatiwa kompyuta 10 hivi karibuni. Kompyuta hizo zimetolewa msaada kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Seattle Marekani linaloitwa FSF. Kompyuta hizo zimekabidhiwa kwa Wizara hivi karibuni na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi. Pia, Wizara imetenga jumla ya shilingi160, 000,000/= katika bajeti yake ya mwaka 2014/2015 kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta kwa skuli mbali mbali ikiwemo hizo mbili. Kompyuta hizo zitakaponunuliwa zitaondoa kabisa upungufu wa vifaa hivyo katika skuli hizo mbili. Pia, Wizara inakusudia kufanya mazungumzo na baadhi ya makampuni kuomba msaada wa vifaa mbali mbali vya kompyuta.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Kwa kuwa amesema wameongeza kompyuta 10 mara juhudi zinachukuliwa ili kompyuta nyengine zipatikane, nataka tu Mhe. Waziri ajue kwamba kwa kuwa ule utaalamu wa wanafunzi unapatikana kwa kufanya *practicals* kwa kutumia hiyo kompyuta, na kwa kuwa hazitoshi, na kwa kuwa wanafuata kufanya mitihini SUZA Mhe. Waziri haoni kuwa kitendo cha kuwahamisha wanafunzi kutoka Chuoni pale hadi SUZA kwa ajili ya kufanya mitihani yao kwa kufuata hizo kompyuta, haoni kwamba ule uwezo wao wa kujibu maswali vizuri utapotea, kutokana na kubadilisha mazingira kutoka mazingira waliyoyazoea na yale wasiyoyazowea.

b) Pamoja na Serikali kuchukua juhudi hizo haoni kwamba kuna kampuni kadhaa ambazo ni vizuri ikaombwa itajwe kwa mambo kama hayo hapa hapa kuna *Mazrui Building Contractors* anaweza kuomba na kupata kompyuta japo kidogo, haoni ni vyema sasa akatafuta ufadhili ikiwa muda umechelewa ili wanafunzi wetu wakapata kile wanachokihitaji; yaani elimu ya vitendo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mheshimiwa nataka nikubaliane na yeye kama mazingira yanachangia bila ya shaka, mazingira ambayo umeyazoea ukiondoka na ukienda katika mazingira mengine kufanya mtihani inawezekana ikachangia ukafanya vibaya, hilo nakubaliana nalo.

Lakini suala la kutafuta makampuni hili Mhe. Spika, nililizungumza katika jibu langu mama kama Wizara ina mpango wa kutafuta makampuni mbali mbali ili itusaidie vifaa hivi mbali ya bajeti ambayo tumetenga.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba Skuli ya Sekondari ya Mombasa na ile ya Chasasa ambayo imeanzisha kwa michepuo ya kompyuta ina upungufu wa vifaa hivyo, na Mhe. Waziri amesema kwamba bajeti hii wametenga milioni 100 kwa ajili ya kazi hiyo ya kununua vifaa.

a) Mnakumbuka kwamba hivi karibuni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alifanya ziara nchini Marekani, na tumearifiwa hapa kwamba ziara hiyo zilipatikana kompyuta 250, kwa nini kompyuta hizo hazigaiwi katika skuli hizo na badala yake kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta hizo.

b) Kwa sababu kompyuta hizo zipo na zimeletwa kwa ziara hii ya Makamu wa Pili wa Rais, huoni kwamba kutenga fedha kwa ajili hiyo ni kufanya matumizi mabaya kwa fedha za umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ni kweli hivi karibuni kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu langu mama nililojibu tulipatiwa kompyuta, lakini kompyuta zile kabla ya kuletwa zilikuwa tayari wale ambao wametufadhili zile kompyuta walitupa na mgao wao, kwa sababu ni skuli wenyewe husika ambao wali- *apply* katika kampuni husika na mgao wake Mhe. Spika, ulikuwa kama hivi ifuatavyo.

Katika kompyuta 230 *Collegeof Health* ilipata kompyuta 50, Chuo cha Utalii kilipata kompyuta 20, Zetech ilipata kompyuta 20, Utaani ndio hizo kompyuta 10 ambazo nimesema wamepata karibuni, Vikokotoni (Skuli) walipata kompyuta 10, Haile Sellassie kompyuta 10, Kengeja ufundi kompyuta 10, Kitope kompyuta 10, Kwamtipura kompyuta 10, Lumumba kompyuta 10, Mchangamdogo kompya 10, Tumekuja kompyuta 10, Mtende kompyuta 10, PLSI kompyuta 10, Jongowe kompyuta 10, Makunduchi kompyuta 10 na Raudha kompyuta 10, jumla ni kompyuta 130.

Mahitaji ya kompyuta Mhe. Spika, ni makubwa katika skuli zetu, kwa sababu hata zile skuli ambazo hazina michepuo ya kompyuta hivi sasa masomo ya kompyuta tunaweka kama masomo ya lazima, kwa hivyo kama ambavyo nilizungumza mwanzo kama hii bajeti tumeweka, na hii bajeti haitotosheleza lakini itaondoa tatizo, na vile vile Wizara inajitahidi kufuata kampuni mbali mbali kuomba ili tuweze angalau kupunguza nusu na robo ya tatizo.

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Namnukuu tena Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake aliyotoa jana kwamba "Waziri makini anatakiwa ajue suali mama litazaa masuali gani mengine", kwa hivyo nampongeza sana Mhe. Zahra Ali Hamad kwa kujibu swali la msingi na kutoa takwimu za skuli zilizopelekwa hizo kompyuta pamoja na kuwa halimo katika swali la msingi, hongera sana Mheshimiwa.

a) Pamoja na hayo naomba kuuliza swali moja lenye kifungu "a" na "b" kama ifuatavyo, suali dogo tu.

Tumeweza kupitia misaada mbali mbali pamoja na msaada wa World Bank kujenga skuli nzuri sana kimajengo pamoja na ile Skuli ya

Mchangamdogo ambayo nilibahatika kuitembelea, wakati katika msaada ule je hivi vifaa vya *laboratory* hamuwezi kuingiza kwenye mikataba ambayo inafanyika kwa ajili ya msaada ule, kwa sababu tunajua kwamba vifaa hivi vya *laboratory* vinakuwa na umuhimu zaidi hata kuliko uzuri wa jengo, kutokana na taaluma inayotolewa na vifaa hivyo wakati wa mitihani.

b) Lakini hawa wakandarasi wetu tunaowapa kama Uholanzi na wengine wanapopewa mikataba hawawezi kuombwa kama wazalendo katika mikataba ile ile nao wakaweka *labo* ndani kwa ajili ya kusaidia, kwa sababu kila wakiweka na wao itawasaidia katika misaada yao, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mheshimiwa kwanza nataka nimthibitishie Mhe. Mahamoud Thabit Kombo, kama katika skuli zetu hizi 16 ambazo alizizungumza ambayo moja kaitembelea Mchangamdogo, skuli hizi zimekamilika kwa maabara zote; zimejaa vifaa vya maabara zote ijapokuwa vifaa hivi vinaweza kuharibika, lakini kwa hivi sasa vipo na sisi tutahakikisha kwa sababu skuli hizi tuliziweka ni skuli za mfano ziwe kweli ni skuli za mfano.

Suala la kuomba wakandarasi ni suala zuri na naomba niyachukue mawazo haya, na kama wizara tutayasimamia na kuyafanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu kidogo hususan katika eneo hili la kuchangia katika sekta ya elimu.

Mhe. Spika, kuchangia ni imani, na kila mmoja wetu na sio tu kwa wakandarasi bali hata sisi viongozi na wananchi wengine na makampuni mbali mbali ni vyema katika kuchangia sekta hii ya elimu hasa katika suala la maabara ambayo bado kuna upungufu mkubwa katika nchi yetu.

Kwa hivyo nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi wananchi wote wenye uwezo na makampuni mengine yote, si kwa wakandarasi peke yao, ili waone umuhimu wa kuchangia katika sekta ya elimu ili kuongeza nguvu za kutoa taaluma zaidi na hasa hasa kuwa na elimu bora katika sekta yetu ya elimu. Hivyo niombe wananchi wote na Wajumbe waone hilo ahsante sana.

Nam. 34.

Udhibiti Usioridhisha wa Waganga wa Jadi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni Zanzibar imekumbwa na wimbi la waganga wa kienyeji wanaojitangaza kutibu magonjwa yote ikiwemo magonjwa sugu kama UKIMWI, SARATANI, KISUKARI n.k. Hali hii imesababisha wagonjwa wengi kuachana na utaratibu wa tiba ya Hospitali na kukimbilia kwa waganga hao na baadhi yao kuzidiwa na maradhi hatimaye kupoteza maisha.

(a) Kwa nini Serikali haisimamii na kutilia mkazo Sheria ya Tiba Asili na Mbadala, Nambari 8 ya Mwaka 2008, iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa kuwadhibiti waganga hao wanaovunja Sheria.

(b) Tokea kutungwa kwa Sheria hiyo mwaka 2008 hadi sasa ni waganga wangapi wa kienyeji wanaojihusisha na vitendo hivyo, wamefikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

(c) Kwa nini waganga hao wanaongezeka na baadhi yao wanatumia vyombo vya habari hata vya Serikali kujitangaza wakati imeshatungwa Sheria ya kudhibiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna mganga wa kienyeji alowahi kufikishwa Mahakamani, ila wapo waliofikishwa Polisi na kupewa onyo. Kwa kawaida linapotokea kosa basi jamii yenyewe huripoti na hatua huchukuliwa kwa kuwafahamisha taratibu za kufanya.

Kwa kuwa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala lina utaratibu wa kufanya ukaguzi vilinge, kliniki na maduka ya dawa za kienyeji, wakikuta kuna matatizo hatua inachukuliwa na kuwapa onyo na ikiwa hawakujirekebisha huwafungia mpaka pale watapofuata masharti yaliyowekwa.

(b) Uganga wa kienyeji ni taaluma ya kujifunza au kurithiwa kutoka kwa watu wengine, kuongezeka hakuzuiliki, lakini utaratibu unaotakiwa kufuatwa ni ule wa kuwaorodhesha kwa Sheha waganga wote Zanzibar ili awajue. Kwa mujibu wa Sheria, Baraza haliruhusiwi kuwasajili waganga, viringe, duka la dawa au kliniki mpaka ipatikane barua kutoka kwa Sheha husika.

(c) Kwa bahati mbaya hao waganga wanaoleta matatizo hawapitii katika Baraza la Tiba Asili na jamii ndio inayowapa hifadhi katika majumba yao bila ya kuripoti kwa masheha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kabisa naomba nimuulize maswali 2 madogo tu ya nyongeza.

Ni chombo gani kinachopima viwango vya ubora wa dawa wanazozitangaza ili kujua ukweli wa dawa kama zinatibu au wanatapeli wananchi. Moja.

Pili, kwa kuwa hivi sasa biashara ya dawa asilia imezagaa na serikali ina mpango gani wa kutenga eneo maalum baada kushuhudia nyumba nyingi za ibada zinauzwa dawa hizo za kienyeji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala linafanya kazi na chombo cha ZFBD ambacho kinapima dawa zote na kutoa ruhusa kwa ile ambayo wanahisi haina matatizo kwa watu, sio kwamba inatibu au haitibu lakini kwamba ikinywewa haitotoa matatizo. Kwa hivyo chombo hicho ndicho kinachofanya kazi.

Lakini kwa vile hii ni sekta ambayo si ya kiserikali; ni sekta binafsi, serikalini hilo halijawahi kuletwa, kwa hivyo huwa wanafanya kazi katika hizo sehemu ambazo wao wanafanya katika majumba yao na katika misikiti. Lakini kutokana na matatizo ambayo yanajitokeza au huwa yamejitokeza, na mpaka sasa kwa ushahidi yamejitokeza kwamba chombo chao hicho ambacho ni Baraza limefanya utaratibu wa kuwaambia kwamba misikiti isiruhusu shughuli hizo kufanyika. Na kwa wale ambao wanafanya hivyo bila ya kuwa wamesajiliwa kwa hivyo wamekwenda na kuwafungia, ushahidi upo wa hilo.

Kuna kliniki 17 zilizokaguliwa 5 hazina usajili ikiwemo kliniki inayoitwa *Nirako Herbalist* iliyopo Mwanakwerekwe; ambayo baada mmiliki kukataa kujisajili pamoja na kutoa vitisho ilibidi itumike nguvu ya dola kuweza kuifunga kliniki hiyo mpaka hapo watakapofuata utaratibu wa kisheria.

Kuna wengine wanaitwa Hija Mchuku walioko kwenye msikiti uliopo *Empire*. Na mtu alijisema kuwa ni daktari anatoka Mombasa Kenya, na baada ya mzozo mkubwa kwa kisingizio cha tiba za sunna alikubali na alikiri makosa na alitakiwa afuate utaratibu. Kwa hivyo kazi hiyo inafanyika. Na ya ziada iliyofanya kwamba Baraza la Tiba ya Asili limefanya ziara maalum ya kutembelea vyombo vya habari 14, radio na TV ziliopo Zanzibar kwa sababu hao ndio imekuwa vichocheo cha matangazo ambayo hayafuati maadili, kwa hivyo wamekatazwa kufanya hivyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, na ninampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali yake kwa

umakini kabisa. Lakini napenda nimuulize, kwa kuwa wametembelea hospitali za tiba asilia, na kwa kuwa wanaotembeza dawa za tiba asilia ni wengi sana sasa hivi, na kwa kuwa Wizara yake ndio Msimamizi Mkuu je, anatuhakikishia au anawahakikishia wananchi kama dawa zile zinazouzwa mitaani za tiba asilia zinakuwa zishachunguzwa na Wizara yake. Na je kwa mwaka mmoja wanafanya uchunguzi mara ngapi kuchunguza hizo dawa ambazo ni za tiba asilia zikaonekana kama hazina madhara kwa binaadam.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, dawa za mitaani haziruhusiwi kuuzwa zinatakiwa kliniki, kiringe, ambapo wataweza kusajiliwa. Wanakatazwa, na kazi hiyo inaendelea lakini binaadamu ndio sisi sheria kufuata hapa kwetu kama ninavyosema, na jana nimesema kwamba tufuate sheria bila ya kushurutishwa, lakini watu wa hapa kama hawakushikiwa kigongo hawakubali kufuata sheria.

Kwa hivyo wanavunja sheria wakiwa wanajua lakini kazi inaendelea, watakapokutikana watakamatwa kwa sababu wanachokifanya si halali na Baraza halikubali. Kazi hiyo inafanywa na itaendelea kufanywa Unguja na Pemba kwa sababu ndio kwanza wameanza.

Kwa sababu Pemba nako kuna tatizo kubwa ni hili. Lakini dawa za mitaani hazichekiwi wala hatushughulikii kwa sababu hawajajisajili, kwa hivyo asiyejisajili hawezi kuangaliwa, kinachofanywa ni kuchukuliwa na zinaharibiwa pale kwa sababu hawana uhakika wa hicho kinachotendeka, kwa nini hawajisajili ina maana kwamba kuna tatizo. Kwa hiyo hizo wala hatuzishughulikii tunazichukua tunashughulikia kwa kuzimwaga halafu na kuwapa onyo kwamba hilo jambo lisirudiwe.

Mimi napenda nimpongeze Waziri wa Afya wa Tanzania Bara jana alitoa tangazo kwenye Bunge alipokuwa akiwasilisha bajeti kwamba anasema kapiga marufuku matangazo yote yanayohusu Tiba Asili kubandikwa mitaani, ninafikiri na Zanzibar tukifanya hilo litatusaidia kwa kiasi fulani.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, swali la mwisho fupi la nyongeza ni kama ifuatavyo. Kwa sababu swali mama linaeleza kuwa waganga hawa wa kienyeji huwa wanajitangazia kutibu maradhi mbali mbali ikiwemo ukimwi, saratani kisukari na kadhalika. Na kwa sababu katika ulimwengu mpaka hivi sasa bado hapajapatikna dawa sahihi ya kutibu ukimwi moja kwa moja isipokuwa kuna dawa za kurefusha maisha. Je kutokana na taarifa hizi za waganga ningelipenda Mhe. Waziri kumuuliza Wizara yake imechukua hatua gani kwa wale waganga ambao wanajitangazia madawa ya kutibu maradhi ambayo dunia nzima hivi sasa imeshindwa kupata dawa zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda nimjibu Mhe. Salim kuwa waganga wa kienyeji wako kwenye biashara; ile ni biashara yao wanayotafutia maisha. Na ili biashara itoke unatakiwa uitangaze ili ivutie. Na biashara itatoka utakapomvutia mteja. Na wateja wapo wana imani tofauti; kuna wanaoamini hospitali kuna wanaoamini dawa za kienyeji. Sisi wataalamu wa Hospitali tunasema dawa ya kutibu ukimwi haipo, tuna dawa ya kupunguza makali. Hao wengine wanasema dawa ya kutibu ukimwi ipo. Hatuwezi tukawazuia watu wasiende kutibiwa huko kwa sababu ni imani yao na hiyari yao. Kikombe cha Babu kiliambiwa kinatibu ukimwi lakini wangapi walikufa.

Kwa hivyo mteja anapoambiwa na yeye atumie akili yake, kwa sababu matangazo yanasema dawa ya Ukimwi haipo kwetu sisi wataalamu wa afya.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 – Wizara ya Katiba na Sheria

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na kazi iliyoko mbele yetu naomba tuwatambue wageni wetu wa leo waliokuja kututembelea nao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka; ambao jumla yao ni 40 wapo pale juu ambao naomba sana wasimame ili Waheshimiwa Wajumbe mutambue kuwepo kwao. *(Makofi).*

Karibuni sana katika shughuli zetu za bajeti kwa Wizara mbali mbali ambayo inaendelea. Ahsanteni sana karibuni.

Baada ya hayo basi sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Karibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kukutana tena katika utekelezaji wa jukumu letu muhimu la kujadili mambo yanayohusu maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo naomba nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk.

Ali Mohamed Shein, kwa kuiongoza nchi yetu vizuri na kuiwezesha kufikia hatua tunayoishuhudia ya maendeleo katika hali ya amani.

Mhe. Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, na Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi kubwa wanazofanya katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo kazi ya kumshauri Mheshimiwa Rais, ambayo wanaitekeleza kwa busara kubwa.

Mhe. Spika, napenda uniruhusu kutoa pongezi kwako wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Baraza letu. Vile vile, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza watendaji wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza kwa kuifanya kazi yako ya kuliongoza Baraza hili kuwa rahisi.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba nitoe shukurani maalum kwa Wajumbe wa Kamati za Baraza kwa jumla kwa umahiri wao katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuishauri ipasavyo Wizara yangu katika masuala mbalimbali, chini ya uongozi imara wa Mwenyekiti Mheshimiwa Ussi Jecha Simai. Pia napenda kuishukuru Kamati ya PAC kwa ushirikiano wanaotoa kwa Wizara yangu, ambao ni nyenzo muhimu inayosaidia uwajibikaji katika masuala ya fedha.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba uniruhusu niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni kwa kunipa ushirikiano mkubwa unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Serikali pamoja na ya jimbo kwa mafanikio.

HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 8,188,000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 4,480,499,000.00 zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na Shilingi 3,707,501,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2014 jumla ya Shilingi 5,852,828,345.00 (71%) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, Shilingi 4,326,176,582.00 (97%), kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 1,526,651,763.00 (41%) kwa matumizi mengineyo. Vile vile, Wizara yangu ilikadiriwa kutumia ruzuku ya Shilingi 730,000,000 ambapo hadi kufikia Machi 2014 imepokea Shilingi 450,512,849.00 (62%). Aidha, kwa kazi za maendeleo Shilingi 2,154,313,000.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 850,000,000.00 ni Mchango wa Serikali na Shilingi 1,304,313,000.00 ni msaada kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Shilingi 711,181,500.00 zimepatikana, ambapo Shilingi 447,584,000.00 (53%) ni mchango wa Serikali na Shilingi 263,597,500.00 (20%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Wizara pia ilikadiria kukusanya Shilingi 435,000,000.00 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi 2014, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 344,093,780.00 (79%). *(Viambatanisho nam. 1 &3 vinahusika).*

UTEKELEZAJI WA IDARA NA TAASISI ZA WIZARA

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe taarifa ya shughuli za Wizara yangu kwa mwaka 2013/14 kwa kueleza maendeleo ya utekelezaji wa taasisi moja baada ya moja kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kuratibu shughuli za Mipango, Sera na Utafiti. Katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Idara imetekeleza jukumu hilo kwa kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi za Wizara za kila robo mwaka na taarifa za usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuziwasilisha kwenye mamlaka na vikao vinavyohusika.

Vile vile, Idara imefanya maandalizi ya kazi za utafiti na sera. Miongoni mwa kazi zilizosimamiwa na Idara hii ni Utafiti wa Mahitaji ya Mafunzo (*Training Needs Assessment*) kwa taasisi za Wizara, utafiti wa Taarifa za Msingi za Sekta ya Sheria (*Baseline Study*) na utafiti kuhusu Njia Bora ya Utunzaji wa Kumbukumbu. Idara pia imeandaa sera ya Msaada wa Kisheria. Rasimu ya Sera hiyo imekamilika katika ngazi ya wataalamu na ngazi ya Wizara, na sasa iko tayari kuwasilishwa kwenye ngazi zinazofuata Serikalini.

Mhe. Spika, Idara pia imeratibu miradi mitano ya maendeleo inayotekelezwa na taasisi za Wizara, ukiwemo Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria; Mradi wa Kuimarisha Ofisi ya Wakala wa Biashara na Mali; Mradi wa Kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka; Mradi wa Kuimarisha Usajili na Upatikanaji wa Takwimu za Matukio ya Kijamii; Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Mahkama na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Wizara. Utekelezaji wa miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali. Ufafanuzi wa taarifa hizi uko kwenye taasisi husika.

Mhe. Spika**,** katika mwaka 2013/14 Idara ilipanga kukamilisha utayarishaji wa Mkakati wa Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria na kuanza utekelezaji wake. Matayarisho hayo yamekamilika katika hatua za awali na rasimu ya mkakati huo imeshawasilishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na kupitishwa.

Mhe. Spika, Idara imewapeleka mafunzoni wafanyakazi wake wanne katika ngazi ya Shahada ya Uzamili, Stashahada ya Uzamili na Shahada. Aidha, wafanyakazi wanne wameripoti kazini baada ya kumaliza mafunzo katika ngazi mbalimbali. Vile vile, Idara imetoa mafunzo ya upangaji na usimamizi wa miradi (*Project Management*) kwa Maafisa Mipango wa Wizara, ili kuwajengea uwezo zaidi katika utekelezaji wa shughuli zao.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa Shilingi 184,152,000.00. Hadi kufikia Machi 2014, Shilingi 109,382,046.00 (59%) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, Shilingi 86,302,400.00 (91%) zimetumika kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 23,079,646.00 (26%) kwa matumizi mengineyo. Shilingi 1,454,313,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, fedha zilizopatikana ni Shilingi 343,931,500.00 (24%). Kati ya fedha hizo, Shilingi 80,334,000.00 (54%) kutoka Serikalini na Shilingi 263,597,500.00 (20%) kutoka kwa washirika wa maendeleo. (*Viambatanisho Nam 1&2 vinahusika*).

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/15 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutekeleza kazi za uratibu wa shughuli za mipango, sera na utafiti za Wizara;
ii. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria; na
iii. Kutekeleza mradi wa kuzisaidia Jumuiya zisizo za Kiserikali Zanzibar.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 224,252,000.00 kwa matumizi ya kawaida, zikiwemo Shilingi 128,784,000.00 za mishahara, na Shilingi 95,468,000.00 za matumizi mengineyo. Vile vile, naliomba Baraza liidhinishe Shilingi 1,729,748,700.00 kwa kazi za maendeleo, zikiwemo Shilingi 150,000,000.00 kutoka Serikalini na Shilingi 1,579,748,700.00 kutoka kwa wahisani.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina dhamana ya kusimamia na kuratibu shughuli zote za uendeshaji na utumishi kwa idara na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Idara imetekeleza uratibu wa shughuli za Wizara, kwa kuandaa mikutano minne ya Kamati ya Uongozi, minne ya Kamati Tendaji, vikao 11 vya Bodi ya Zabuni na vikao vitatu vya Kamati ya Tathmini. Aidha Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Utumishi imefanikisha kazi za kurekebisha mishahara ya wafanyakazi wenye uzoefu

Mhe. Spika, pamoja na shughuli hizo, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inasimamia vitengo vinne vya Wizara vifuatavyo:- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Uhasibu, Kitengo cha Ununuzi na Kitengo cha Mawasiliano.

Mhe. Spika, kazi za ukaguzi wa ndani wa hesabu zimefanyika kwa ufanisi ambapo Ripoti za Ukaguzi za Julai-Septemba na Oktoba-Disemba 2013/14 zimewasilishwa kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Wizara na kujadiliwa. Ripoti ya Januari-Machi 2014 ipo kwenye hatua ya maandalizi. Kwa upande mwengine, Kitengo cha Uhasibu kimetekeleza kazi zake za kawaida ikiwemo kutoa ufafanuzi wa hoja za Ukaguzi wa Ndani na hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, ripoti ya mwaka ya upatikanaji wa fedha (*Financial Statement*) na taarifa za fedha za robo mwaka zimeandaliwa.

Mhe. Spika, idara imeratibu ushiriki wa Wizara katika maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushiriki katika michezo, maonesho, kutayarisha "*documentary*" na kuandika Kitabu cha Wizara kuhusu Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50. Idara pia imesimamia uendeshaji wa Afisi kwa kufanikisha manunuzi na upatikanaji wa huduma za mawasiliano, usafiri, vitendea kazi, safari za kikazi pamoja na kuratibu kazi za ujenzi wa Jengo la Wizara.

Mhe. Spika, katika kuratibu masuala mtambuka, idara imeendesha mafunzo maalum kwa maafisa wa wizara juu ya masuala yanayohusu shughuli za Watu Wenye Ulemavu, mapambano dhidi ya UKIMWI na mazingatio yake katika mipango ya kazi.

Mhe. Spika, idara imeratibu utekelezaji wa Ripoti ya Mahitaji ya Mafunzo kwa wafanyakazi wa Wizara (*Training Needs Assessment*). Mafunzo ya Usimamizi wa Raslimali Watu yalitolewa kwa Maofisa Utumishi na mafunzo ya Mawasiliano na Huduma Bora Kazini yalitolewa kwa wahudumu na wafanyakazi wengine wa taasisi za Wizara Unguja na Pemba. Hadi kufikia

mwishoni mwa mwezi Machi, 2014 jumla ya wafanyakazi 324 wa ngazi tofauti wamepatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo watumishi wa idara, kwa mwaka wa fedha 2013/14, idara imewapeleka masomoni wafanyakazi wawili katika Shahada ya Uzamivu ya Sheria na Shahada ya Raslimali Watu. Pia watumishi sita wanaendelea na masomo katika ngazi mbalimbali wakiwemo wawili wanaosomea Shahada, mmoja anayesomea Shahada ya Uzamili na watatu wanasoma Stashahada.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/14, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 591,141,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo Kati ya fedha hizo, shilingi 338,831,00.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki kwa watumishi na shilingi 252,310,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 fedha zilizopatikana ni shilingi 329, 951,941.00 (56%). Kati ya fedha hizo, shilingi 275, 360,350.00 (81%) zilitumika kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 54, 591,591.00 (22%) kwa matumizi mengineyo. *(Kiambatanisho Nam 1 kinahusika).*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha usimamizi wa kazi za uendeshaji wa Wizara;
ii. Kusimamia na kuratibu majukumu ya rasilimali watu;
iii. Kutekeleza kazi za utoaji wa taarifa za wizara; na
iv. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wake.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 716,160,600.00 kwa kazi za kawaida, zikiwemo shilingi 465,722,600.00 kwa mishahara na stahiki kwa watumishi na shilingi 250,438,000.00 kwa matumizi mengineyo.

MAHAKAMA

Mhe. Spika**,** Mahkama ina jukumu la kusimamia utoaji wa haki. Katika kufanikisha jukumu hilo Mahkama imeweza kusikiliza kesi mbalimbali za madai na jinai pamoja na rufaa za Mahkama Kuu. Kwa kipindi cha Julai -

Machi 2013/14 Mahkama imepokea na kusajili kesi 6,514 kutoka Mahkama zote Unguja na Pemba.
Mhe. Spika, katika kipindi hicho, Mahkama Kuu imepokea mashauri mapya 116. Ukijumuisha na mashauri 93, imekuwa na jumla ya mashauri 209. Mashauri 43 yametolewa uamuzi. Katika Divisheni ya Mahkama ya Kazi, yamepokelewa mashauri mapya saba na kuifanya divisheni hiyo iwe na mashauri 13 kwa kujumuisha na mashauri sita yaliyosajiliwa kabla. Mahkama hiyo imetoa uamuzi kwa mashauri sita.

Mhe. Spika, katika Mahkama za Mkoa, mashauri mapya 316 yamepokelewa na kufanya Mahkama hizo ziwe na jumla ya mashauri 649, kwa kujumuisha na mashauri mengine 333 yaliyosajiliwa kabla kipindi hicho. Mahkama za Mikoa zimetoa maamuzi kwa mashauri 58.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, Mahkama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 2,391 na kufikisha jumla ya mashauri 3,277 yanapojumuishwa na mashauri 866 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 1,516.

Mhe. Spika, Mahkama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 2,616 na kufikisha jumla ya mashauri 3,385 yanayojumuisha mashauri 766 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2014 Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 2,128.

Mhe. Spika, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa imepokea mashauri mapya 38, na kuifanya iwe na jumla ya mashauri 66 yanapojumuishwa na mashauri 28 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 10 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Vile vile, Mahkama za Kadhi wa Wilaya zilipokea mashauri mapya 994 na kuwa na jumla ya mashauri 1,905 yanapojumuishwa na mashauri 911 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 651 kati ya hayo yametolewa uamuzi.

Mhe. Spika, Mahkama ya Rufaa ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilikuwa na idadi ya mashauri manne yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Kufikia Machi 2014 Mahkama hiyo imepokea mashauri 10 na kufikisha jumla ya mashauri 14. Hakuna shauri lililotolewa uamuzi katika kipindi hicho.

Mhe. Spika, Mahkama ya Watoto ilianza mwaka wa fedha 2013/14 ikiwa na idadi ya mashauri 56 yaliyosajiliwa kutoka miaka ya nyuma na kupokea mashauri mapya 23, na hivyo kufanya idadi ya mashauri kufikia 79. Aidha, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 Mahkama ya Watoto imetoa uamuzi kwa mashauri manne tu kutokana na kukosekana kwa mashahidi.

Mhe. Spika, uchambuzi huo unatuonesha kwamba kwa wastani Mahkama zetu zimeweza kutoa uamuzi kwa asilimia 47% ya kesi 9,550 ambayo ni jumla ya kesi 6,514 zilizofunguliwa kwa mwaka 2013/14 na kesi 3,036 zilizosajiliwa kabla ya kipindi hicho na kesi 4,461 zimetolewa uamuzi. *(Viambatanisho vya 5a & 5b vinahusika).*

Mhe. Spika, katika kuelimisha jamii, Mahkama imeendesha vipindi vitatu vya elimu kupitia televisheni ya *ZBC*. Vile vile, imefanya mikutano katika Shehia ya Kwarara na kwa Wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Benbella; imeandaa kongamano la wananchi ili kutathmini utendaji wa Mahkama kwa kipindi cha miaka 50 ya Mapinduzi; na imetoa Toleo la 3 la Jarida la Mahkama na kulisambaza kwa wananchi.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wake, Mahkama imewapatia fursa ya masomo wafanyakazi watano katika ngazi ya Cheti na Stashahada za Sheria, Utawala wa Umma na Katibu Muhtasi Unguja na Pemba. Vile vile, Mahakimu wa Unguja na Pemba wamepatiwa Semina ya Teknolojia ya Habari na Sheria; Mahakimu wapya, Makadhi na Makarani wamepatiwa mafunzo ya namna ya uendeshaji wa kesi na utoaji wa haki; na Makarani wa Mahkama Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa kesi. Aidha, Mahkama imeandaa Mkutano wa Kimataifa wa Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki na kutoa fursa kwa Majaji na Mahakimu wetu kubadilishana mawazo na uzoefu na Mahakimu wenzao.

Mhe. Spika, Mahkama imeendelea kutekeleza mradi wa kuimarisha majengo yake. Majengo ya Mahkama Kuu Unguja, Mahkama ya Kadhi Mwanakwerekwe, na Mahkama ya Makunduchi yamefanyiwa matengenezo makubwa. Aidha, matayarisho ya matengenezo ya Jengo la Mahkama Kuu Chake Chake yameanza. Matengenezo hayo kwa kutayarisha michoro pamoja na makisio ya gharama za matengenezo ya jengo hilo, ambayo yanatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2014/15.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Mahkama iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3, 583, 000,000.00 kwa kazi za kawaida zikiwemo shilingi 2, 350, 100,000.00 kwa mishahara na stahiki, na shilingi 1, 232, 900,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya shilingi 150, 000,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo na shilingi 90, 000,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Mahkama iliingiziwa shilingi 3, 043, 785,541.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo shilingi 2, 421, 625,710.00 (65%) zilitumika kulipia mishahara na stahiki za wafanyakazi na shilingi 622, 159,831.00 (51%) kwa matumizi mengineyo.

Kwa kazi za maendeleo, Mahkama iliingiziwa shilingi 130, 000,000.00 (87%) kutoka Serikalini na shilingi 119,907,110.00(133%) zimekusanywa kuchangia mapato ya Serikali *(Viambatanisho nam. 1 & 3 vinahusika.)*
Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015 Mahkama imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kupunguza mrundikano wa kesi na kukuza upatikanaji wa haki; na
ii. Kuyafanyia matengenezo majengo manne ya Mahkama Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ili Mahkama iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 5,036,700,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 3,536,700,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 1,500,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Vile vile, naomba Mahkama iidhinishiwe jumla ya shilingi 700,000,000.00 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, Mahkama inakusudia kukusanya jumla ya shilingi 95,000,000.00 kuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Mhe. Spika, jukumu la msingi la Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni kuishauri Serikali kwa mambo ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya Sheria, kusimamia mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali na kuandaa hati na nyaraka za kisheria.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imetayarisha Miswada sita ya Sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi. (*Angalia Kiambatanisho Nam.6)*. Vile vile, Afisi imeandaa na kuchapisha kanuni 20 za sheria mbalimbali, matangazo 41 ya kisheria (*Legal Notice*) na imesimamia mikataba 24 kwa ajili ya Wizara na Taasisi za Serikali. Wakati huo huo, Afisi inaendelea kusimamia kesi 45 za madai zilizofunguliwa dhidi ya Serikali. Katika kuimarisha usimamizi wa kesi hizo, Afisi imewateua baadhi ya wanasheria kutoka katika taasisi mbalimbali ili kumuwakilisha Mwanasheria Mkuu kusimamia kesi zinazohusu taasisi zao.

Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliendesha Warsha juu ya Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu, Semina juu ya Sheria ya Bahari kwa Makatibu Wakuu na Semina kwa Wanasheria wa Taasisi za Serikali kuhusu Sheria ya Kuanzishwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa watendaji wa taasisi za Serikali. Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali yenye umuhimu kwa wakati huu.

Mhe. Spika, katika kutekeleza masharti ya Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Nam. 6/2013, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeanzisha vitengo vya Usimamizi wa Mikataba; Usimamizi wa Kesi; Uandishi wa Sheria; Maendeleo ya Afisi na Wafanyakazi; na Utawala. Vile vile, Afisi imeteua wasimamizi wa vitengo hivyo. Kuanzishwa kwa vitengo hivyo vitano kunakamilisha muundo wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, tuna heshima kulijulisha Baraza lako Tukufu kwamba kazi ya ujenzi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu imekamilika na jengo hilo lilifunguliwa wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jengo hilo liko eneo la Mazizini, jirani na Afisi ya Mufti. Kwa upande mwengine, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kuwasomesha watendaji wake ambapo wafanyakazi watano wamepatiwa mafunzo katika kiwango cha *LLB, BA* na Stashahada. Aidha, Afisi iliandaa mafunzo kwa watendaji juu ya utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14 Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 919,000,000.00 zikiwemo shilingi 245,400,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi

673,600,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kufikia Machi 2014, jumla ya shilingi 317,918,200.00 (99%) zilipatikana kwa ajili ya mishahara na shilingi 290,376,702.00 (52%) kwa matumizi mengineyo. *(Kiambatanisho nam. 1 kinahusika)*.

Mhe. Spika, katika mwaka 2014/2015, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa na kuwasilisha Baraza la Wawakilishi Miswada ya Sheria ya Hati ya Uwakala, Sheria ya Wasimamizi wa Amana na Wasii, Sheria ya Tafsiri na Masharti ya Jumla, na Sheria ya Kusimamia Hundi;

ii. Kuziweka pamoja na kuzichapisha sheria za Zanzibar za mwaka 1980 – 2010;

iii. Kukamilisha kazi ya kukusanya na kuyaweka pamoja Magazeti Rasmi ya Serikali kutoka 1910 hadi 1963; na

iv. Kutoa elimu kwa umma,kuijengea uwezo Afisi na kuimarisha uwezo wa watendaji.

v.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 999,300,000.00 kwa kazi za kawaida zikiwemo shilingi 461,899,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 537,401,000.00 za matumizi mengineyo.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu la kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake. Utekelezaji wa jukumu hilo unahusisha utafiti na kuwashirikisha wananchi katika hatua za awali hadi hatua za kupendekeza marekebisho ya sheria zinazohusika. Tume pia inatoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Zanzibar ili wananchi waweze kuelewa haki na wajibu wao.

Mhe. Spika, katika kipindi kifupi tangu kuimarishwa upya kwa Tume, sheria tano zifuatazo zimefanyiwa mapitio:-

Sheria ya Ushahidi Sura ya 5/1917, Sheria ya Vileo Sura ya 163, Sheria ya Rasilimali Mifugo Nam. 11/1999, Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Nam 16/1986 na Sheria ya Usafirishaji Bidhaa kwa njia ya bahari Sura ya 155/1926.

Aidha, Tume imefanya utafiti na kubainisha sheria 34 ambazo hazina utata, sheria 61 zisizotumika na zilizopitwa na wakati, na sheria 120 zilizofutwa. Utafiti huu umeiwezesha Tume kupanga utaratibu mzuri wa mapitio ya sheria.
Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14, Tume imepanga kufanya mapitio ya sheria 4, ambazo ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na 7 ya 2004, "*Limitation Decree*" Sura ya 12 ya 1917, "*The Legal Practitioners Decree*" Sura ya 28 ya 1941 na "*The Notaries Public Decree*" Sura ya 29 ya 1948.
Tume imezifanyia utafiti sheria hizo kwa kufanya uwiano na sheria za wenzetu, kwa kuzingatia mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na mazingira ya Zanzibar. Kupitia utafiti huo, Tume imegundua vikwazo viliopo katika utekelezaji wa sheria hizo na hatua iliyobakia ni kupata maoni ya wananchi ili iweze kuandaa ripoti ya mwisho.

Mhe. Spika, Tume imetayarisha na kurusha vipindi 10 vya *redio* na 10 vya televisheni ili kutoa elimu kwa umma kuhusu matumuzi ya Sheria za Zanzibar. Aidha, Tume imefanya Semina kuhusu mapitio ya Sheria kwa Mahakimu, Mawakili wa kujitegemea, Wanasheria wa Serikali, Askari Polisi, Viongozi wa Dini, Walimu, Wanafunzi, na Asasi za Kiraia.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kimataifa, Tume inaendelea kuwa mwanachama wa Tume za Kurekebisha Sheria wa Afrika Mashariki, Kusini na Kati (*ALRAESA*) na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria wa Jumuiya ya Madola (*CALRAs*). Vile vile, Tume inaendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi zilizo katika nchi mbalimbali kama vile Uganda, Uingereza na India, ili iweze kujifunza kutoka kwao.

Mhe. Spika, takriban kwa kipindi cha miaka miwili na nusu Tume ilikuwa ikihangaika na makaazi ya kudumu. Hivi sasa Tume imefarajika kwa kupatiwa jengo lilokuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hii ni hatua nzuri iliyoleta utulivu wa kufanya kazi na kuchangia maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, Tume imewapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi watendaji wake wanne katika kada tofauti kama ifuatavyo:- wafanyakazi watatu

wamepata mafunzo ya muda mafupi ya Utafiti na Uandishi wa Sheria na mafunzo ya Uongozi na Utawala nchini Afrika ya Kusini na India. Mfanyakazi mmoja amepatiwa mafunzo ya Cheti ya Uhifadhi na Uwekaji Kumbukumbu katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Aidha, wafanyakazi watatu wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu nchini katika kada ya Uhasibu, Kompyuta na Ukatibu Muhtasi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 483,000,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 147,000,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 336,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014 shilingi 212,278,735.00 (44%) zilipatikana, zikiwemo shilingi 113,153,750.00 (77%) kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 99,124,985.00 (30%) kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar zifuatazo:- "*The Succession Decree*" Sura ya 21/1917, "*The External Probates Decree*" Sura ya 22/1918, *The Vagrancy Decree* Sura ya 21/1962 na Sheria ya Utalii Nam 6 ya 2009 kama ilivyorekibishwa na sheria Nam 7/2012;
ii. Kutoa elimu kwa Umma; na
iii. Kuimarisha utendaji wa kazi za Tume.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 497,800,000.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 157,900,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 339,900,000.00 kwa matumizi mengineyo.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina jukumu la Usimamizi wa Mashtaka ya Jinai Zanzibar, isipokuwa katika Mahkama za Kijeshi.

Mhe. Spika**,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2013/14 imeendelea kusimamia kesi za jinai na kutoa ushauri wa kisheria kwa Jeshi la Polisi na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na raia.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2014 jumla ya Kesi za Jinai 1,522 zimefunguliwa katika Mahkama za Zanzibar katika ngazi tofauti. Kati ya kesi hizo, kesi 621 zimeshatolewa uamuzi na kesi 901 zinaendelea katika Mahkama mbalimbali kwa hatua tofauti. Aidha, majalada ya uchunguzi wa jinai 108 kutoka Jeshi la Polisi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Jumla ya kesi za jinai za rufaa 49 zimesimamiwa na Afisi katika Mahkama mbalimbali na zimetolewa uamuzi. Vile vile, malalamiko 83 kutoka kwa wananchi yamepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/14 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilipanga kuimarisha na kuendeleza uendeshaji wa Mashtaka Kiraia kwenye Wilaya ambazo bado hazijafikiwa na huduma hiyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Afisi imeajiri Wanasheria watano wapya na imetekeleza mradi wa kuwapatia nyumba za makaazi Waendesha Mashtaka watakaofanya kazi katika Mahkama za Makunduchi, Mwera na Mkokotoni.

Mhe. Spika, kazi ya Uendeshaji wa Mashtaka inahitaji mashirikiano baina ya Taasisi zinazosimamia haki za jinai. Afisi imeongeza ushirikiano na Jeshi la Polisi, Mahkama, Mawakili wa Utetezi na Jamii kwa ujumla na imeweza kuandaa mikutano 10 inayohusisha Waendesha Mashtaka na Wapelelezi.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuendeleza taaluma zinazohusu uwanja wa sheria, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kupitia Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria, inaendelea kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Sheria kwa watendaji mbalimbali wa Serikali na taasisi binafsi wakiwemo Wanasheria. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa ni Uandishi wa Sheria (*Legislative Drafting*) na Usimamizi wa Sheria ya Wafanyakazi wa Umma (*Public Service Law Training*).

Katika kipindi cha mwaka 2014/15 Kituo kinatarajia kutoa mafunzo ya Stashahada ya Kawaida, Stashahada ya Sheria pamoja na Cheti. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai mwaka 2014. Pia Kituo kinatarajia kutoa mafunzo juu ya Uchunguzi, Usimamizi na Uendeshaji wa Mashtaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendelea na hatua ya kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbali mbali ya haki za jinai kwa lengo la

kuelimisha jamii. Afisi imechapisha na kusambaza Toleo la 11 la Jarida la Shahidi na maandalizi ya Toleo la 12 yanaendelea. Katika kipindi hicho, vipindi vinane vya redio vimerushwa hewani.

Katika kukuza uwezo wa Afisi kiutendaji, jumla ya wafanyakazi 34 wamepatiwa mafunzo katika nyanja mbalimbali zikiwemo Sheria, Utawala na Maktaba.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,103,000,000.00 kwa kazi za kawaida, ambapo shilingi 612,000,000.00 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za wafanyakazi na Shilingi 491,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Pia Afisi iliidhinishiwa Shilingi 150,000,000.00 kwa kazi za maendeleo na Shilingi 80,000,000.00 za ruzuku. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni Shilingi 814,303,150.00 (74%). Kati ya fedha hizo, Shilingi 560,003,150.00 (92%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 254,300,000.00 (52%) kwa matumizi mengineyo.

Kwa upande wa kazi za maendeleo, zilipatikana jumla ya Shilingi 150,000,000.00 (100%) na Shilingi 67,500,000.00 (84%) zimepatikana kwa ajili ya ruzuku. *(Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imejiwekea malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na Uendeshaji Mashtaka Kiraia;
ii. Kukuza na kuimarisha kazi za Uendeshaji Mashtaka; na
iii. Kukuza uwezo wa rasilimali watu.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,288,500,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo Shilingi 871,900,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 416,600,000.00 za matumizi mengineyo. Vile vile, naliomba Baraza liidhinishe Shilingi 200,000,000.00 kwa ajili ya kazi za maendeleo na Shilingi 77,500,000.00 kwa ajili ya ruzuku ya kukiendeleza Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhamana kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu, ikiwemo kutoa fat-wa na kusimamia miongozo kuhusu masuala ya kidini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/14, Afisi ya Mufti imetekeleza malengo yake ikiwemo kufanya Mikutano ya Baraza la Maulamaa, Kuratibu na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi, Kufanya ziara za Misikiti na Vyuo vya Qur-ani, kujibu masuali ya wananchi, kutatua migogoro ya kidini pamoja na kuhamasisha amani na utulivu.

Mhe. Spika, katika kuimarisha uratibu wa shughuli za kidini, jumla ya vyuo vya Qur-ani 44 na misikiti 21 vimetembelewa Unguja na Pemba, kwa lengo la kushauriana juu ya maendeleo ya taasisi hizo. Vile vile Misikiti 60 na Vyuo 173 vya Qur-ani vimesajiliwa. Katika juhudi za kupata takwimu sahihi za misikiti na vyuo vya Qur-ani, Afisi ya Mufti imeandaa utaratibu wa kugawa fomu kwa Masheha kupitia kwa Wakuu wa Wilaya za Unguja ili wazijaze. Fomu hizo zinaendelea kukusanywa. Kazi hiyo pia itafanyika kisiwani Pemba.

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti imeendelea kutoa elimu kwa umma. Jumla ya masuala 166 yamejibiwa kupitia *ZBC* Redio. Aidha, vipindi 26 vya nasaha na mawaidha ya dini vimetolewa. Vipindi hivyo zaidi vilihusu mambo yanayoathiri jamii yakiwemo masuala ya ndoa na talaka, mmong'onyoko wa maadili katika jamii, udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji. Aidha, afisi inaendelea kuimarisha Maktaba ya Kiislamu kwa kuiongezea vitabu.

Mhe. Spika, Baraza la Maulamaa ni chombo chenye jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Mufti kutoa fat-wa kitaalamu zaidi. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2013/14, Baraza hilo limekutana mara moja na kuzungumzia, pamoja na mambo mengine, masuala ya ubakaji.

Mhe. Spika, kazi nyengine inayofanywa na Afisi ya Mufti ni kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Kuthibitisha Kuandama kwa Mwezi ili iweze kutoa taarifa kwa wakati. Kamati imefanya vikao vitatu na kutoa taarifa za kuandama kwa mwezi. Wakati huo huo, Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Kamati ya Zafa ya Kitaifa na Jumuiya ya Miladunnabii, iliandaa sherehe za kuukaribisha mwaka mpya wa Kiislamu 1435 Hijriya na kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W).

Mhe. Spika, katika kuweka utulivu ndani ya jamii, kwa mwaka 2013/14 Afisi ya Mufti imepokea migogoro ya ndoa 83 ambapo migogoro 80 kati ya hiyo

imepatiwa ufumbuzi na mitatu imepelekwa Mahkamani. Aidha, Afisi imepokea migogoro 13 ya misikitini. Kati ya migogoro hiyo, 12 imetatuliwa na mmoja umepelekwa Mahkamani. Katika kupunguza migogoro hiyo, Afisi ya Mufti imekuwa ikifanya ziara na mikutano kwenye misikiti mbalimbali ili kutoa maelekezo juu ya njia bora za uendeshaji wa misikiti na kuondoa migogoro.

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na *World Islamic Call Society* kutoka Libya ilifanya mkutano uliojumuisha Maimamu 150 kutoka Wilaya zote za Unguja, kwa lengo la kuhamasisha maelewano baina ya waumini na kuondoa migogoro. Vile vile, Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Kituo cha Kiislamu cha Misri kilichopo Dar es Salaam, imefanya mkutano kwa Masheikh, Maulamaa, Maimamu, Walimu wa Madrassa na Waumini kwa ujumla, kwa lengo la kukumbushana na kuhimizana umuhimu wa kuepuka migogoro misikitini na katika jamii. Mkutano kama huo unategemewa kufanyika Pemba hapo baadae.

Mhe. Spika, mashirikiano mema na viongozi wa dini wa ndani na nje ni msingi wa kukuza undugu na maendeleo ya waumini na dini yao. Kwa mwaka wa fedha 2013/14, Afisi imepokea wageni kutoka nchi mbalimbali, wakiwemo Mheshimiwa Mufti wa Oman, Mufti wa Burundi na Mashekhe wawili kutoka Taasisi ya Sultan Qaboos ya Kituo cha Utamaduni na Sayansi.

Mhe. Spika, katika kuendeleza mashirikiano ya kidini, kikao kimoja kilifanyika baina ya viongozi wa Dini ya Kiislamu wakiongozwa na Mufti wa Zanzibar na viongozi wa dini ya Kikristo waliopo Zanzibar wakiongozwa na Askofu Shao, ili kuhamasisha ushirikiano na kuvumiliana kidini.

Mhe. Spika, ili kujiimarisha kitaaluma, Afisi ya Mufti kwa mwaka wa fedha 2013/14, imewapeleka masomoni wafanyakazi wawili katika ngazi ya Shahada na Stashahada.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Afisi ya Mufti iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 485,666,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 302,639,000.00 zilitengwa kwa mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 183,027,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, jumla ya Shilingi 255,574,206.00 (53%) zilipatikana. Kati ya fedha hizo, Shilingi 222,616,160.00 (74%) zimetumika kulipia mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 62,958,046 (34%) kwa ajili ya matumizi mengineyo. *(Kiambatanisho Nam.1 kinahusika.)*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Mufti imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha shughuli za dini;
ii. Kuimarisha Afisi Kitaaluma; na
iii. Kuimarisha shughuli za Utawala.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mufti wa Zanzibar itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 500,609,400.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 367,544,400.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 133,065,000.00 kwa matumizi mengineyo.

WAKALA WA USAJILI BIASHARA NA MALI

Mhe. Spika, Afisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali '*Business and Property Registration Agency'* (*BPRA*) ina jukumu la kufanya usajili wa biashara, hati za mali za ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:- Kuimarisha mazingira ya kazi kwa ajili ya kutoa huduma bora; kuandaa kanuni za sheria za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali; kufanya Usajili wa Taasisi za Biashara na Usajili wa Dhamana za Mali zinazohamishika; na kuendelea na uwekaji wa mifumo ya kisasa ya usajili.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai - Machi 2013/14 *BPRA* imesajili Kampuni 160, Majina ya Biashara 280, Alama za Biashara 430, Nyaraka 528 na Jumuiya za kiraia 67. Kimsingi, kazi za *BPRA* zinalenga kwenye utekelezaji na usimamizi wa sheria na haki mbalimbali za wananchi kwa kutoa huduma za usajili kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yanayotokea ulimwenguni, *BPRA* inaendelea kuimarisha miundombinu ya usajili ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, afisi imekamilisha rasimu ya Kanuni za Sheria ya Tasnia za Mali za Ubunifu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mali za Ubunifu Ulimwenguni *"World Intellectual Property Organization" (WIPO)* na Shirika la Mali za Ubunifu la Afrika *"Africa Regional Intellectual Property Organization (ARIPO).*

Aidha, wakala *BPRA* kwa kushirikiana na Shirika la Mali za Ubunifu Ulimwenguni (*WIPO*) wametayarisha rasimu ya Sera ya Mali za Ubunifu Zanzibar. Rasimu hiyo imetumwa *WIPO* kwa kufanyiwa mapitio na baadae kurudishwa serikalini kwa hatua za kuikamilisha. Vile vile, afisi imekamilisha marekebisho na tafsiri ya Sheria ya Usajili wa Kampuni. Sheria hiyo tayari imeshapitishwa na Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wake, *BPRA* inaendelea kusomesha wafanyakazi wanne katika ngazi ya Shahada; Stashahada ya Ugavi na Manunuzi; Shahada ya Takwimu na Shahada ya Uzamili ya Sheria.

Aidha, wafanyakazi watatu wamepata mafunzo ya muda mfupi ya mchakato wa kubuni biashara kwa nchi za Afrika; mafunzo ya kikanda ya Utawala na Usajili wa Alama za Biashara na Mali za Ubunifu na mafunzo ya Ulinzi wa Kijiografia kwa Viashiria vya Mali Bunifu yaliyofanyika nchini Zimbabwe.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, *BPRA* iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 289,006,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 139,008,000.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 149,998,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014 fedha zilizopatikana ni Shilingi 146,499,400.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 105,016,400.00 (76%) zilitumika kulipa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 41,483,000.00 (31%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 100,000,000.00 ziliidhinishwa kutoka serikalini kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014 fedha zilizopatikana ni Shilingi 25,680,000.00 (26%). Vile vile, afisi ilikadiriwa kukusanya Shilingi 125,700,000.00. Hadi kufikia Machi 2014, iliweza kukusanya Shilingi 97,695,170.00 (78%). *(Viambatanisho nam. 1,3 na 4 vinahusika).*

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wakala wa Usajili Biashara na Mali imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za usajili wa biashara, mali na usimamizi wa tasnia za mali ubunifu; na
ii. Kuijengea uwezo afisi kiutendaji

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 313,312,400.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 170,234,400.00 ni kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 143,078,000.00 ni kwa matumizi mengineyo. Aidha, afisi

inakusudia kukusanya jumla ya Shilingi 126,494,000.00 kuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

AFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO

Mhe. Spika, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo (AMVV) ina dhima kisheria ya kusajili Vizazi na Vifo pamoja na kutunza kumbukumbu zinazotokana na usajili huo. Afisi hii pia inawajibika kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Usajili wa Vizazi na Vifo, kutoa mafunzo yanayohusiana na usajili kwa watendaji na wakala wa usajili pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imesajili vizazi 36,826 ambapo wanawake ni 18,303 na wanaume ni 18,523. Pia Afisi imesajili vifo 2,228; wakiwemo wanaume 1,200 na wanawake 1,028. Kutokana na takwimu hizo ni wazi kwamba uandikishwaji wa vifo ni mdogo. Hali hiyo inatokana na mwamko mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kufanya usajili wa vifo. Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inaendelea na utaratibu wa kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa usajili wa vizazi na vifo. Pia, nawashauri Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kusaidia kuendeleza juhudi za kuelimisha wananchi katika maeneo yao.

Mhe. Spika, afisi pia inaendelea na marekebisho ya mfumo wa usajili ili kuachana na usajili wa *manual* na kuelekea kwenye usajili wa kompyuta. Hivi sasa afisi inafanya majaribio ya mfumo huo katika Wilaya ya Magharibi Unguja kwa ajili ya kutumia fomu mpya. Tayari afisi imetoa mafunzo ya kujaza fomu mpya za kizazi, kifo na kizazi mfu kwa Masheha, Makatibu Sheha pamoja na wauguzi.

Baada ya kazi hiyo, itafuata hatua ya kuingiza taarifa za miaka ya nyuma kwenye kompyuta, kutoa mafunzo kwa mawakala wa usajili kwenye wilaya zilizobakia na kuihamasisha jamii kupitia vyombo vya habari. Jitihada hizi zitakapokamilika zitasaidia upatikanaji wa kumbukumbu na vyeti kwa njia rahisi na ya haraka.

Mhe. Spika, katika maandalizi ya mfumo mpya wa usajili, afisi tayari imekamilisha ukarabati wa Afisi nne za Usajili za Wilaya za Unguja na Wilaya tatu za Pemba. Afisi hizo ni za Wilaya ya Mkoani, Chakechake, Micheweni, Kaskazini “A, Kaskazini “B”, Kati na Kusini. Lengo letu hivi sasa ni kukamilisha wilaya zilizobaki.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imempatia mfanyakazi mmoja mafunzo ya Stashahada ya Utunzaji na Uhifadhi wa Nyaraka na watumishi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya maadili ya utumishi katika Chuo cha Utawala wa Umma.

Aidha, afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, imewapatia mafunzo mafupi wafanyakazi wake wanne nchini Afrika ya Kusini, ili kuwaongezea ujuzi katika kuimarisha usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 353,460,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 145,221,000.00 zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 208,239,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi ni Shilingi 93,676,500.00 (65%) na Shilingi 30,532,000.00 (18%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi 300,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka serikalini na zilizopatikana ni Shilingi 61,570,000.00 (21%).

Afisi pia ilikadiriwa kukusanya mapato ya Shilingi 219,300,000.00. Kufikia Machi 2014, jumla ya Shilingi 126,491,500.00 (58%) zilikusanywa. *(Kiambatanisho nam 3 kinahusika)*.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma za usajili;
ii. Kuimarisha mazingira ya Afisi na Utawala; na
iii. Kujenga uwezo wa wafanyakazi kitaaluma.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 418,283,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 232,923,000.00 zitumike kulipia mishahara na stahiki na Shilingi 185,360,000.00, kwa matumizi mengineyo. Vile vile, naliomba Baraza lako liidhinishe matumizi ya Shilingi 50,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inakadiria kukusanya mapato ya Shilingi 221,000,000.00 kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar ina dhima kisheria ya kuhakikisha hadhi na maslahi ya wabunifu wa Zanzibar zinaimarika kwa kuthaminiwa na kupatiwa malipo yanayotokana na matumizi ya kazi zao kibiashara.

Afisi pia ina jukumu la kusajili kazi za hakimiliki, kutoa leseni kwa matumizi halali ya kazi hizo kwa watumiaji kibiashara, pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwa wasanii na wabunifu ambao kazi zao zimetumika katika maeneo mbalimbali kibiashara. Vile vile, afisi hii inawajibika kutoa taaluma kwa wabunifu, watumiaji wa kazi za ubunifu na hakimiliki na jamii, ili kuelewa matumizi halali na thamani ya hakimiliki kibiashara.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai- Machi, 2013/2014, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki imeingiza taarifa za kazi za usajili na uhifadhi wa kumbukumbu katika mfumo wa *WIPOCOS* (*WIPO Software for Collective Management Organization*), ambapo jumla ya kazi 140 za hakimiliki zilisajiliwa. Idadi hiyo inafanya jumla ya kazi zote za hakimiliki zilizosajiliwa kufikia 2,118. (*Kiambatanisho Nam. 8 kinahusika).*

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza tangu Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ianzishwe, imefanikiwa kugawa fedha za mirabaha zinazokusanywa kutokana na matumizi ya kazi za sanaa na ubunifu. Ugawaji huo ulisimamiwa na Kamati maalum ya ugawaji wa mirabaha. Jumla ya Shilingi 37,648,000.00 zilizokusanywa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2010, ziligawiwa kwa wabunifu na wasanii 726. Kati ya waliofaidika ni vikundi vitatu vya taarab, viwili vya muziki wa kizazi kipya, 12 vya maigizo na filamu, wamiliki wa kasida na mawaidha pamoja na wabunifu mmoja mmoja. Katika mgao huo mbunifu aliyepata kiwango cha juu ni shilingi 560,000.00 na kiwango cha chini kilikuwa shilingi 7,000.00. Hamasa iliyopatikana baada ya ugawaji mirabaha imepelekea kazi nyengine mpya 91 kusajiliwa.

Mhe. Spika, katika jitihada za kupunguza uhalifu na uharamia wa kazi za hakimiliki, afisi ilifanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya wakodishaji na wauzaji wa kazi hizo pamoja na mahoteli. Vile vile, afisi imesambaza hati za madai na barua za ukumbusho wa malipo ya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za Hakimiliki, ili kuiwezesha afisi kufanya mgao kwa wakati. Hata hivyo, bado kuna ugumu wa ulipaji wa mirabaha na afisi inaendelea kuchukua juhudi za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulipa.

Mhe. Spika, hatua nyengine iliyochukuliwa kupambana na uhalifu wa kazi za hakimiliki ni kuangamiza picha na vinasa sauti vya kielektroniki vilivyokamatwa.

Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Idara ya Mazingira, imeangamiza jumla ya nakala haramu 6,525 za *CD* na *DVD* zilizokamatwa. Vile vile, afisi imeendelea kufanya utafiti kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara, ili kugundua watumiaji wasio na leseni ya hakimiliki. Utafiti huo pia umebainisha kuwa kuna kiasi kikubwa cha usambazaji wa vinasa sauti na picha vya kielektroniki vinavyokiuka maadili.

Mhe. Spika, ili kupata taarifa sahihi juu ya kazi zilizotumika na zenye kutoa mwelekeo wa ugawaji mirabaha kwa wahusika, afisi iliendelea kusambaza fomu za marejesho ya kazi za hakimiliki (*log sheets*) kwa vituo vyote vya utangazaji vya umma na binafsi.

Aidha, afisi inaendelea kutatua migogoro inayojitokeza ya wabunifu na kutoa ushauri wa kisheria, pamoja na kuandaa na kupitia mikataba ya wamiliki na watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara.

Mhe. Spika, afisi kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar imeendelea kuwaelimisha watumiaji na wamiliki wa kazi za Hakimiliki juu ya haki za wabunifu na wasanii. Hadi kufikia Machi 2014, vipindi 11 vilitayarishwa na kurushwa hewani, vikiwemo vipindi saba vya televisheni na vinne vya redio. Vile vile, afisi imetoa elimu ya ana kwa ana kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar wanaofanya utafiti.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Afisi imewapeleka wafanyakazi wake wawili nchini Botswana na Malawi kwa mafunzo ya ugawaji wa mirabaha na mafunzo ya mbinu za upatanishi. Wafanyakazi wengine walipatiwa mafunzo ndani ya nchi kuhusu mbinu za ukusanyaji wa mirabaha na utoaji wa leseni, kwa watumiaji wa kazi za Hakimiliki kibiashara.

Mhe. Spika, Afisi inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uelewa mdogo wa jamii na taasisi za Serikali; juu ya umiliki wa Hakimiliki na mipaka ya uhalali wa matumizi ya kazi za Hakimiliki pamoja na mchango wa Hakimiliki kwa uchumi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki iliidhinishiwa ruzuku ya Shilingi 140,000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 63,347,000.00 zilitengwa kulipia mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 76,653,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, fedha zilizopatikana ni Shilingi 45,183,600.00 (71%) kwa ajili ya mishahara ya

watumishi na Shilingi 42,006,000.00 (55%) kwa matumizi mengineyo. *(Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Afisi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha usimamizi wa Hakimiliki;
ii. Kuendelea kuelimisha jamii juu ya masuala ya Hakimiliki; na
iii. Kuimarisha shughuli za uratibu na utawala.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Ruzuku ya Shilingi 170, 000,000.00 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 85, 647,600.00 zimetengwa kulipia mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 84,352,400.00 kwa matumizi mengineyo.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Mhe. Spika, jukumu la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni kusimamia Mali za Wakfu, Mali za Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi ya Kitaifa, Hijja, Zakka, Sadaka na Misaada ya kheri.

Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida, ikiwemo kukusanya na kugawa zakka, sadaka na misaada ya kheri.

Kwa kipindi cha Julai - Machi 2013/2014, misaada ya kheri yenye thamani ya Shilingi 506,250,000.00 imekusanywa na kugawiwa kwa wanufaika mbalimbali. Aidha, Kamisheni imefanya vikao 26 vya kuelimisha na kuhamasisha wanufaika wa mali hizo. Jumla ya vikundi 88 vya wajasiriamali vimetembelewa na kupewa ushauri katika kuzitunza mali hizo.

Pia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kidini kufanikisha upatikanaji wa misaada ya kheri na ugawaji wa misaada hiyo kwa jamii. Miongoni mwa misaada hiyo ni nyama ya kondoo na mbuzi, tende na nguo za Iddi kwa watoto yatima. Aidha, Kamisheni ilishirikiana na taasisi nyengine katika kuhudumia wananchi kwa kuziombea taasisi hizo misamaha ya ushuru kwa mujibu wa sheria na kusimamia ugawaji wa misaada hiyo.

Mhe. Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma za Wakfu, Kamisheni imeendelea kutoa taaluma kuhusu Wakfu na Mali ya Amana. Jumla ya vipindi vinane (8) vya redio na televisheni vimerushwa hewani na Muongozo wa Wakfu umechapishwa na kuanza kugawiwa.

Aidha, kazi ya utafiti wa kuzitambua mali za wakfu, kutafuta nyaraka zilizopotea, kujua wasia wa nyakfu hizo pamoja na kuwatambua wanufaika halali imeendelea. Kwa mujibu wa utafiti huo, nyaraka 1,008 zimepatikana, nyakfu mpya 20 zimesajiliwa na nyasia 13 zenye thamani ya Shilingi 8,669,500.00 zimetumika kutekelezea nyasia mbalimbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa nyumba za wakfu, Kamisheni imeendelea kuwawekea mazingira mazuri wapangaji ili waweze kulipa kodi vizuri na wanufaika kupata faida inayotokana na mali zilizowekwa Wakfu. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, nyumba 229 zimekaguliwa, kutambuliwa mipaka yake na zimejaziwa fomu maalum kusaidia zoezi la usajili wa ardhi. Aidha nyumba 19 zimefanyiwa matengenezo yaliyogharimu Shilingi 52,617,380.00.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine kazi ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi za Nyumba za Wakfu na Amana imeendelea na jumla ya kodi zenye thamani ya Shilingi 230,472,650.00 za nyumba za Wakfu, Shilingi 4,698,000.00 za mashamba na Shilingi 37,146,250.00 za nyumba za Amana zimekusanywa Unguja na Pemba. Fedha hizo tayari zimegawiwa kwa wanufaika.

Mhe. Spika, ili kutekeleza huduma za mirathi jumla ya tirka mpya 852 zilifunguliwa Unguja na Pemba. Aidha, tirka 202 zenye thamani ya Shilingi 2,715,610,597.44 zilifungwa na warathi kupatiwa haki zao.

Mhe. Spika, Kamisheni inalo jukumu la kusuluhisha mizozo inayotokezea wakati wa kutekeleza wajibu wake. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2013/14, jumla ya mizozo ya mirathi 15 imesuluhishwa na mizozo mitano inaendelea kushughulikiwa. Mizozo inayoshindikana hupelekwa Mahkamani ili kupatiwa ufumbuzi wa kisheria. Jumla ya kesi 39 zimepelekwa kwenye Mahkama mbalimbali Unguja na Pemba. Kati ya kesi hizo zipo zilizofunguliwa dhidi ya Kamisheni au Kamisheni kushirikishwa. Kesi 29 kati ya hizo zimetolewa hukumu na kesi 10 bado zinaendelea. Vile vile, Kamisheni kwa kushirikiana na Shirika la Denmark la *Dan Mission* imetunga kitabu cha Usuluhisho wa Mizozo kitakachosaidia utatuzi wa mizozo hasa katika masuala ya urithi.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pia ina jukumu la kusimamia Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa. Ili kuongeza ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za kitaifa, kwa mara ya kwanza, Sala ya Idd El Hajj imesaliwa kwenye mamlaka za Serikali za Wilaya na Wilaya ya Kati ilikuwa mwenyeji. Kwa upande mwengine Sala ya Idd El Hajj ilisaliwa kwenye kiwanja cha mpira katika kijiji cha Marumbi, na Baraza la Iddi lilifanyika Chuo Kikuu cha Taifa SUZA Kampasi ya Tunguu. Sala ya Idd El Fitri

ilisaliwa kwenye Kiwanja vya Maisara na Baraza la Iddi lilifanyika katika Ukumbi wa Salama Hoteli ya Bwawani, kama ilivyo desturi.

Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea na kazi ya kusimamia safari za Hijja na kama ilivyo kawaida na jumla ya mahujaji 1,059 walisafirishwa na vikundi tisa vya Zanzibar. Aidha, katika kufanikisha kazi hiyo, Kamisheni imeelimisha jamii na wadau wa Hijja kwa kurusha hewani vipindi tisa, semina moja na vikao 10. (*Kiambatanisho Nam. 7 kinahusika*).

Mhe. Spika, katika kuimarisha ofisi kiutendaji wafanyakazi wanane wamelipiwa mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao, mfanyakazi mmoja anasoma Shahada ya Uzamili, wanne Shahada, mmoja Stashahada, na wawili mafunzo ya Cheti. *(Kiambatanisho Nam. 9(b) kinahusika).*

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamisheni inakabiliwa na changamoto ya uelewa mdogo wa jamii juu ya umuhimu wa mirathi, amana, wakfu na zakka kwa wananchi walio wengi; na teknolojia isiyoendana na wakati katika usimamizi na utoaji wa huduma katika Kamisheni ya Wakfu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Kamisheni imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuelimisha na kuimarisha huduma za Zakka, Wakfu na Mirathi;

ii. Kuimarisha shughuli za uratibu na mahitaji ya kisheria; na

iii. Kuimarisha Ofisi kinyenzo na kitaaluma.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/14 Kamisheni iliidhinishiwa ruzuku ya jumla ya Shilingi 510,000,000.00. Hadi kufikia Machi, 2014 fedha zilizoingizwa ni Shilingi 295,823,249.00 (58%). Kati ya fedha hizo, Shilingi 177,092,450.00 (59.9%) zilitumika kwa malipo ya mishahara na stahiki za wafanyakazi na Shilingi 118,730,799.00 (40%) zilitumika kwa matumizi mengineyo. *(Kiambatanisho Nam. 1 kinahusika).*

Mhe. Spika, ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 512,070,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 378,634,000.00 ni mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 133,436,000.00 kwa matumizi mengineyo.

AFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba ni mhimili mkuu katika kusimamia shughuli za utendaji wa Wizara pamoja na taasisi zake kisiwani Pemba. Katika kipindi cha

mwaka 2013/14, Afisi Kuu Pemba imetekeleza majukumu yake ya kusimamia shughuli za Wizara kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Afisi imeendelea kuratibu masuala ya Idara zilizopo chini ya Wizara kwa upande wa Pemba kwa lengo la kuzidisha uwajibikaji. Vile vile, Afisi imefanya mikutano ya kila mwezi ya Taasisi na Idara za Wizara Pemba. Mbali ya majukumu hayo, Afisi Kuu Pemba pia imeshiriki vikao mbalimbali vya Wizara vinavyohusu shughuli za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na kutoa mwongozo kuhusu utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu za wafanyakazi na utayarishaji wa *Nominal Roll*.

Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za Afisi Kuu Pemba ni kuratibu shughuli za Jumuiya Zisizo za Kiserikali *(NGOs).* Afisi imekutana na viongozi wa jumuiya mbali mbali kwa lengo la kutathmini utendaji pamoja na kuwepo kwa jumuiya hizo, na kuhamasisha matumizi mazuri ya fedha wanazozipata katika miradi mbalimbali ili kuleta maendeleo kwa jamii. Jumla ya jumuiya 43 zimetembelewa; 18 ni za Mkoa wa Kaskazini na 25 za Mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, Afisi ilipokea malalamiko kutoka jumuiya nne na tayari yamepatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo watendaji, Afisi imemlipia gharama za mafunzo mfanyakazi mmoja anayesoma Shahada ya Uzamili. Vile vile, kupitia Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria Afisi Kuu imetoa mafunzo ya mawasiliano bora kazini, kuwajali wateja na usimamizi wa miradi. Mafunzo kama hayo yataendelea katika robo ya nne ya mwaka 2013/14.

Mhe. Spika, pamoja na hatua hizo, Afisi Kuu Pemba inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa jengo la Afisi. Hali hii inatokana na kuwa bajeti ya Afisi hairuhusu kufanya matengenezo makubwa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14 Afisi Kuu Pemba ilikadiria kutumia jumla ya Shilingi 196,575,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 105,704,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 90,871,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2014, jumla ya Shilingi 132,507,489.00 zimepatikana, ambapo Shilingi 99,053,562.00 (94%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 33,453,927.00 (37%) kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/15, Afisi Kuu Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutekeleza kazi za uratibu wa shughuli za mipango Pemba;
ii. Kusimamia na kuratibu majukumu ya rasilimali watu na uendeshaji; na

iii. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wake na kulifanyia matengenezo jengo la Wizara.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Afisi Kuu Pemba inakadiria kutumia jumla ya Shilingi 248,382,600.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 157,791,600.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 90,591,000.00 kwa matumizi mengineyo.

SHUKRANI

Mhe. Spika, baada ya maelezo, napaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo alionijaalia wa kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

Naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau na washirika mbalimbali wa maendeleo kwa kuipa mashirikiano mazuri Wizara yangu na kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Wizara. Miongoni mwao ni:- *UNDP*, Jumuiya ya Ulaya *(EU), UNICEF*, *UNFPA*, Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu *(WIPO)*, Shirika la Mali Bunifu la Afrika *(ARIPO)*, Benki ya Dunia, *African Muslim Agency*, Benki ya Maendeleo ya Kiislam *(IDB)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, *Save the Children*, Wizara za Wakfu za Oman na Qatar, Taasisi ya Al-Rahma ya Falme za Kiarabu *(UAE)* na Shirika la *Dan Mission* la Denmark; Saud Arabia, Oman na Egypt; Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano zikiwemo Mahkama, Tume ya Kurekebisha Sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Jeshi la Polisi; Chama cha Wanasheria Zanzibar *(ZLS)*, Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar *(ZLSC)*, na Chama cha Wanasheria Wanawake *(ZAFELA);* Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji, Jumuiya na Taasisi mbalimbali za kidini; Masheha na wananchi wote kwa jumla.

Mhe. Spika, vile vile, kwa ujumla naomba kuwashukuru wote walioisaidia Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano wanaonipa. Naomba kuwaambia washirika wetu kwamba Wizara yangu inathamini sana michango yao ya hali na mali pamoja na kushukuru kwa ushirikiano wanaotupatia kila tunapowahitaji. Ninachoweza kusema kwao ni ahsanteni na tunawathamini sana na kushukuru kwa yote.

Kwa niaba ya Wizara yangu na Serikali kwa jumla tunaomba muzipokee shukrani zetu. Ahsanteni na Mungu awabariki.

HITIMISHO

Mhe. Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake vyema, naomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waidhinishe jumla ya Shilingi 11,002,870,000.00 kwa matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2014/15 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 7,045,680,600.00 zitumike kulipia

mishahara na Shilingi 3, 957,189,400.00 kwa matumizi mengine. Vile vile, naliomba Baraza lako liidhinishe Ruzuku ya Shilingi 735,300,000.00. Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe Shilingi 2,679,748,700.00 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, 1,100,000,000.00 ni kutoka Serikalini, na Shilingi 1,579,748,700.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Naomba pia Baraza lako liikubalie Wizara yangu ichangie Shilingi 442,494,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Viambatanisho Nam. 2, 3 & 4 vinahusika.)*

Mhe. Spika, baada ya kuelezea hayo naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kujadili makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara yangu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha na Matumizi, 2013/14

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIYOTENGWA	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara na Stahiki	94,596,000	86,302,400	91%
	Matumizi Mengineyo	89,556,000	23,079,646	26%
	Jumla	**184,152,000**	**109,382,046**	59%
	Maendeleo Serikali	150,000,000	80,334,000	54%
	Maendeleo - UNDP	1,304,313,000	263,597,500	20%
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara na Stahiki	338,831,000	275,360,350	81%
	Matumizi Mengineyo	252,310,000	54,591,591	22%
	Jumla	**591,141,000**	**329,951,941**	56%
Mahkama	Mishahara na Stahiki	3,698,210,260	2,421,625,710	65%
	Matumizi Mengineyo	1,209,000,000	622,159,831	51%
	Jumla	**4,907,210,260**	**3,043,785,541**	62%
	Maendeleo Serikali	150,000,000	130,000,000	87%
	Makusanyo	90,000,000	119,907,110	133%
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	Mishahara na Stahiki	245,400,000	317,280,200	129%
	Matumizi Mengineyo	673,600,000	265,314,608	39%
	Jumla	**919,000,000**	**582,594,808**	63%
Tume ya Kurekebisha Sheria	Mishahara na Stahiki	147,000,000	113,153,750	77%
	Matumizi Mengineyo	336,000,000	99,124,985	30%
	Jumla	**483,000,000**	**212,278,735**	**44%**
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	Mishahara na Stahiki	612,000,000	560,003,150	92%
	Matumizi Mengineyo	491,000,000	254,300,000	52%
	Jumla	**1,103,000,000**	**814,303,150**	74%
	Maendeleo Serikali	150,000,000	150,000,000	100%
	Jumla Kuu	**1,253,000,000**	**964,303,150**	**77%**
Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	Mishahara na Stahiki	139,008,000	105,016,400	76%
	Matumizi Mengineyo	134,015,000	41,483,000	31%
	Jumla	**273,023,000**	**146,499,400**	54%
	Makusanyo	125,700,000	97,695,170	78%
	Jumla Kuu	**398,723,000**	**267,907,220**	67%
Afisi ya Vizazi na Vifo	Mishahara na Stahiki	104,704,000	93,676,500	89%
	Matumizi Mengineyo	174,055,000	30,532,000	18%
	Jumla	**278,759,000**	**124,208,500**	45%
	Makusanyo	219,300,000	126,491,500	58%
	Maendeleo Serikali	300,000,000	61,570,000	21%

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIYOTENGWA	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Afisi ya Mufti wa Zanzibar	Mishaharana stahiki	302,647,500	222,616,160	74%
	Matumizi Mengineyo	183,027,000	62,958,046	34%
	Jumla	**485,674,500**	**255,574,206**	53%
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	Mishahara na Stahiki	303,474,700	145,323,104	48%
	Matumizi Mengineyo	459,525,300	289,474,717	63%
	Jumla ruzuku	**763,000,000**	**434,797,821**	57%
	Makusanyo	253,000,000	285,834,089	113%
	Jumla Kuu	**1,016,000,000**	**720,631,910**	71%
Afisi ya Hakimiliki	Mishahara na Stahiki	63,347,000	45,183,600	71%
	Matumizi Mengineyo	76,653,000	42,006,000	55%
	Jumla ya Ruzuku	**140,000,000**	**87,189,600**	62%
Afisi Kuu Pemba	Mishahara na Stahiki	133,378,262	99,053,562	74%
	Matumizi Mengineyo	85,531,000	33,953,927	37%
	Jumla	**218,909,262**	**130,007,489**	59%
Jumla ya Wizara (Mishahara, Stahiki na OC)		**8,188,000,000**	**5,852,828,345**	**71%**
Jumla Mishahara		**4,480,499,000**	**4,326,176,582**	**97%**
Jumla Matumizi Mengine		**3,707,501,000**	**1,526,651,763**	**41%**
Jumla Maendeleo SMZ		**850,000,000**	**4447,584,000**	**53%**
Jumla Maendeleo Wahisani (DPs)		**1,304,313,000**	**263,597,500**	**20%**
Jumla ya Wizara Maendeleo		**2,154,313,000**	**711,181,500**	**33%**
Jumla Kuu ya Wizara		**11,072,313,000**	**6,564,009,845**	**63%**
Jumla Makusanyo		**435,000,000**	**344,093,780**	**79%**
Jumla Ruzuku		**730,000,000**	**450,512,849**	**62%**

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2014/15

FUNGU/ IDARA	KAZI ZA KAWAIDA (000)					KAZI ZA MAENDELEO (000)			JUMLA KUU
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	
14 – Mahkama Kuu	5,036,700	3,536,700	1,500,000	3,864,702	1,171,998	700,000	0	700,000	5,736,700

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2014/15

FUNGU/ IDARA	KAZI ZA KAWAIDA (000)					KAZI ZA MAENDELEO (000)			JUMLA KUU
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	
15 – Afisi ya M/ Mkuu	999,300	461,899	537,401	999,300	0	0	0	0	999,300
46 - Tume ya K/ Sheria	497,800	157,900	339,900	497,800	0	0	0	0	497,800
35 - Afisi ya M/Mashtaka	1,288,500	871,900	416,600	1,049,350	239,150	200,000	0	200,000	1,488,500
36/03 - Afisi Kuu Pemba	248,383	157,792	90,591	0	248,383	0	0	0	248,383
36/04 - Idara ya MSU	224,252	128,784	95,468	224,252	0	150,000	1,579,749	1,729,749	1,954,001
36/05 - Afisi ya Mufti	500,609	367,544	133,065	322,189	178,421	0	0	0	500,609
36/06 - Idara ya Uendeshaji na Utumishi	716,161	465,723	250,438	716,161	0	0	0	0	716,161
36/11Wakala wa UBM	313,312	170,234	143,078	294,650	18,662	0	0	0	313,312
36/901 - Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo	418,283	232,923	185,360	330,405	87,878	50,000	0	50,000	468,283
Ruzuku - DPP	77,500	30,000	47,500	0	0	0	0	0	77,500
Ruzuku - KWNMA	512,070	378,634	113,436	400,040	112,030		0		512,070
Ruzuku- Afisi ya Hakimiliki	170,000	85,648	84,352	170,000	0	0	0	0	170,000
JUMLA Ruzuku	**759,570**	**494,282**	**265,288**	**570,040**	**112,030**	**0**	**0**	**0**	**759,570**
VOTE 36	**2,421,000**	**1,523,000**	**898,000**	**1,887,656**	**533,344**	**200,000**	**1,579,749**	**1,779,749**	**4,200,749**
Votes 14, 15, 35, 46,	**7,822,300**	**5,028,399**	**2,793,901**	**6,411,152**	**1,411,148**	**900,000**	**0**	**900,000**	**8,722,300**

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2014/15

FUNGU/ IDARA	KAZI ZA KAWAIDA (000)					KAZI ZA MAENDELEO (000)			JUMLA KUU
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	
JUMLA KUU	**11,002,870**	**7,045,681**	**3,957,189**	**8,868,848**	**2,056,522**	**1,100,000**	**1,579,749**	**2,679,749**	**13,652,619**

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato na Makadirio ya 2014/2015

IDARA/TAASISI	MAKADIRIO 2013/14	MAKUSANYO HALISI 2013/14	%	MATARAJIO JUNI 2014	JUMLA HADI JUNI 2014	%	MAKADIRIO 2014/15
36/11 WAKALA WA USAJILI BISHARA NA MALI	125,700,000	97,695,170	78%	23,712,650	121,407,820	97%	126,494,000
14MAHKAMA	90,000,000	119,907,110	133 %	13,323,012	133,230,122	148%	95,000,000
36/902 MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO	219,300,000	126,491,500	58%	50,075,000	176,566,500	81%	221,000,000
JUMLA KUU	**435,000,000**	**344,093,780**	**79%**	**87,110,662**	**431,204,442**	**99%**	**442,494,000**

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2014/15

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Mchango wa Wahisani	Mhisani	Jumla Kuu
74017	Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Katiba na Sheria	0			0
74018	Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria	150,000,000	1,579,748,700	UNDP/EU	1,729,748,700
74019	Mradi wa Mageuzi katika Usajili na Takwimu za Kijamii	50,000,000	0		50,000,000
72212	Mradi wa kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	200,000,000	0		200,000,000
72234	Kuimarisha Majengo ya Mahkama Kuu	700,000,000	0		700,000,000
	JUMLA KUU	**1,100,000,000**	**1,579,748,700**		**2,733,938,592**

Kiambatanisho 5a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani Julai hadi Machi 2013/2014

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mahkama ya Rufaa Tanzania	10	0	0	0	0	6	0	4	0
M/Kuu Vuga	111	39	23	11	9	30	7	9	1
M/kuu Pemba	5	2	0	0	0	3	0	0	0
Mahkama ya kazi	7	7	0	0	0	0	0	0	0
M/Kadhi Rufaa Z'bar	33	0	0	0	0	33	10	0	0
M/ Kadhi Rufaa P	5	0	0	0	0	5	0	0	0
M/ Mkoa Vuga	134	28	13	104	4	2	0	0	0
M/Mkoa Mfenesini	63	2	0	54	3	1	0	6	2
Mkoa Mwera	45	1	0	44	1	0	0	0	0
Mkoa Wete	40	1	0	39	15	0	0	0	0
Mkoa Chake	34	0	0	33	4	0	0	1	0
Wilaya Mw/kwe	1082	24	4	1058	794	0	0	0	0
Wilaya Mwera	490	2	0	487	268	1	0	0	0
Wilaya Mkokotoni	209	1	0	207	139	1	0	0	0
Wilaya Mfenesini	253	2	0	251	138	0	0	0	0
Wilaya Makunduchi	100	4	1	95	28	1	0	0	0
Wilaya Mkoani	38	0	0	38	36	0	0	0	0
Wilaya Chake	64	3	0	61	33	0	0	0	0
Wilaya Wete	69	0	0	69	41	0	0	0	0
Wilaya Konde	86	0	0	86	79	0	0	0	0
Watoto Vuga	18	0	0	18	4	0	0	0	0
Watoto Chake	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Watoto Wete	5	0	0	5	0	0	0	0	0
Jumla	**2901**	**116**	**41**	**2660**	**1596**	**83**	**17**	**20**	**3**

Kiambatanisho 5b: Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo na Kadhi 2013/14

Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo						**Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Kadhi**		
Mahkama ya Mwanzo	**Kesi za Madai**			**Kesi za Jinai**		**Mahkama za Kadhi Wilaya**	**Kesi za Madai**	
	Jumla (Madai+Jinai)	**Zilizo funguliwa**	**Zilizo tolewa uamuzi**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizotolewa uamuzi**		**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa uamuzi**
Manispaa Malindi	584	0	0	584	584			
Mwanakwerekwe	1138	98	41	1040	970	Mjini	693	517
Mwera	144	21	0	123	75	Mwera	63	27
Mfenesini	173	15	2	158	124	Mfenesini	31	15
Mkokotoni	87	13	4	74	34	Mkokotoni	38	10
Makunduchi	99	16	1	83	38	Makunduchi	17	6
Chwaka	128	3	0	125	96	Chwaka	2	1
Mkoani	117	3	1	114	84	Mkoani	19	8
Kengeja	16	0	0	16	13	Kengeja	12	3
Chake chake	61	0	0	61	5	Chakechake	59	22
Wete	36	0	0	36	29	Wete	28	17
Konde	40	5	1	35	26	Konde	32	25
JUMLA	**2623**	**174**	**50**	**2449**	**2078**	**JUMLA**	**994**	**651**

Kiambatanisho 6: Miswada – Afisi ya Mwanasheria Mkuu 2013/14

Nam	**Miswada ya Sheria iliyoandaliwa**
1.	Mswada wa Sheria ya kukinga na Kusimamia mambo ya UKIMWI Zanzibar
2.	Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya barabara Zanzibar
3.	Mswada wa Sheria ya kuanzisha sheria ya hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea
4.	Mswada wa Sheria ya kufuta sheria ya karafuu namba 11 ya 1985
5.	Mswada wa sheria ya kuanzisha Shirika la nyumba Zanzibar

Kiambatanisho 7a: Mapato – Wakala wa Usajili Biashara na Mali 2013/14

KASMA	ENEO LA MAPATO	ZILIZOIDHINISHWA	ZILIZOKUSANYWA	PUNGUFU/ ZIADA	MAKADIRIO 2014/15
142233	Usajili Alama za Biashara	55,800,000	34,705,000	21,095,000	51,250,000
142234	Usajili Kampuni	31,750,000	39,837,870	(8,087,870)	40,604,000
142235	Usajili Majina ya Biashara	18,900,000	9,268,000	9,632,000	15,000,000
142237	Ada za Usajili wa Nyaraka	19,250,000	13,884,300	5,365,700	19,640,000
	JUMLA	**125,700,000**	**97,695,170**	**28,004,830**	**126,494,000**

Kiambatanisho 7b: Mapato – Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo 2013/14

KASMA	ENEO LA MAPATO	ZILIZOIDHINISHWA	ZILIZOKUSANYWA	PUNGUFU	MAKADIRIO 2014/15
114602	Estate Duty	3,000,000	240,000	2,760,000	2,000,000
142207	Vizazi na Vifo	180,000,000	108,268,093	71,731,907	180,000,000
142208	Ndoa na Talaka	27,000,000	17,775,000	9,225,000	36,000,000
142236	Admin. General Fee	3,000,000	208,407	2,791,593	3,000,000
142234	Vyeti vya Ndoa	6,300,000		6,300,000	0
	JUMLA	**219,300,000**	**126,491,500**	**88,083,500**	**221,000,000**

Kiambatanisho 8: Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2013 - KWNMA

S/N	JINA LA KIKUNDI	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
1	AHLU SUNNA WALJAMAA	32	11	43
2	AHLUDAAWA HAJJ&TRAVEL AGENCY	36	23	59
3	ZANZIBAR HAJJ TRAVEL AGENCY	64	61	125
4	TAWHEED	6	9	15
5	AL-BUSHRA	3		3
6	ISTIQAAMA HAJJ MLANDEGE	76	67	143
7	ZANZIBAR ISTIQAAMA HAJJ(MOTHER CARE)	76	64	140
8	JUMAZA HAJJ GROUP	31	24	55

Kiambatanisho 9: Usajili wa Kazi za Hakimiliki

S/N	AINA YA KAZI	IDADI YA KAZI
1	Taarab	44
2	Zenji Flavor	14
3	Qasida	38
4	Injili	9
5	Filamu	3
6	Vitabu	14
7	Miradi	3
8	Vipindi	1
9	Michoro	14
	JUMLA	**140**

9	ALHARAMAIN HAJJ	35	28	63
	JUMLA	**359**	**287**	**646**

Kiambatanisho: 10a Idadi ya Wafanyakazi wa Wizara 2013/2014

Idara/Taasisi	Jumla	Unguja		Pemba		Wafanyakazi Kielimu		
		W/me	W/ke	W/me	W/ke	Cheti au chini	Stashahada au zaidi	Stashahada au zaidi%
Mahkama	**379**	163	95	83	38	258	121	**32%**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	**54**	32	22			26	28	**52%**
Tume ya Kuchunguza Sheria	**17**	11	6	0	0	8	9	**53%**
Mkurugenzi wa Mashtaka	**95**	**49**	**27**	**16**	**3**	27	68	**72%**
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	**16**	8	8	0	0	2	14	**88%**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	**50**	29	21	0	0	33	17	**34%**
Afisi Kuu Pemba	**29**	0	0	17	12	21	7	**25%**
Idara ya Mufti wa Zanzibar	**43**	18	11	10	4	27	16	**37%**
Mrajis Vizazi na Vifo	**30**	6	20	2	2	14	16	**53%**
Wakala wa Usajili Biashara na Mali	**42**	19	13	6	4	23	19	**45%**
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	**7**	4	3	0	0	1	6	**86%**
Kamisheni ya Wakfu	**83**	36	16	22	9	56	27	**33%**
Jumla	**845**	**375**	**242**	**156**	**72**	**496**	**348**	**41%**

Kiambatanisho 10b: Idadi ya Wafanyakazi Waliopo Mafunzoni 2013/14

IDARA	**SHAHADA YA UZAMILI**		**STASHAHADA YA UZAMILI**		**SHAHADA**		**STASHAHADA YA JUU**		**STASHAHADA**		**CHETI**		**JUMLA**
	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Mahkama									3	1			**4**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu					1				2				**3**
Afisi ya M/ Mashtaka		3			2	2					4	1	**12**
Tume ya Kurekebisha Sheria					1				3				**4**
Idara ya Mipango na Sera		1	1	1	1	3			1				**8**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1	1				2			1	2	2		**9**
Afisi Kuu Pemba		2											**2**
Afisi ya Mufti wa Zanzibar					2				1				**3**
Wakala wa Usajili Biashara na Mali		1				1							**2**
Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo										1			**1**
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	1	1								1			**3**
Kamisheni ya Wakfu na MA		1			1	3			2			1	**8**
JUMLA	**2**	**10**	**1**	**1**	**8**	**11**			**13**	**5**	**6**	**12**	**59**

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa kutumia saa moja barabara muda tuliokubaliana. Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wajumbe, sasa hoja hiyo ijadiliwe.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, natanguliza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutubariki neema ya afya na uzima hadi tukaweza kukusanyika katika ukumbi huu kutekeleza wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Nikushukuru na wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mbele ya Baraza lako.

Mhe. Spika, nichukue wasaa huu mfupi kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria ambaye pia ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mgogoni, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ambaye mashirikiano yake na Kamati yetu ni makubwa lakini zaidi kwa kutekeleza maagizo na ushauri wa Kamati yetu kwa lengo la kufanikisha utekelezeaji wa kazi mbali mbali za Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, nina wingi wa heshima kumshukuru pia Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu Mdungi Makame Mdungi pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao na Kamati yetu wakati wote tukiwa kwenye kazi za Kamati.

Mhe. Spika, nawasilisha hotuba hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika ukumbi huu nikiwa na fahari ya kufanikisha kazi za Kamati hii kwa mashirikiano makubwa na Wajumbe wote wa Kamati ambao kwa heshima na taadhima kubwa naomba kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ussi Jecha Simai	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdallah Juma Abdalla	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
4.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
5.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
6.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Mjumbe

Mhe. Spika, shughuli na kazi za Kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, zinaratibiwa na Makatibu wetu kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi ambao ni:-

1. Ndugu Aziza Wazir Kheir; na
2. Ndugu Khamis Hamad Haji

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi naomba sasa nieleze maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa kuangalia Idara na Taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imesikitishwa na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria lililopo Mazizini, Zanzibar. Awali ujenzi wa jengo hili ulitarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2013 ambapo haukukamilika kwa muda uliopangwa. Kutokana na taarifa ya Wizara ujenzi huo sasa unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2014.

Mhe. Spika, ujenzi huo unasuasua kutokana na kuchelewa kuingizwa fedha za ujenzi, hali hiyo inapelekea kuongezwa muda wa ujenzi ambao nao pia unasababisha hasara kwa Serikali, kwa vile gharama za ujenzi zinaongezeka. Kamati yetu inashauri Wizara ya Fedha kuingiza fedha za ujenzi kwa wakati ili kukamilisha ujenzi huo na kuepuka hasara ya gharama za ziada kutokana na muda wa ujenzi kuongezeka.

Mhe. Spika, Kamati yangu imefurahishwa na hatua ya matengenezo ya jengo la Mahkama Kuu Vuga ambalo sasa lipo katika hali nzuri na tunaipongeza Wizara kwa kufanikisha matengenezo hayo. Aidha, Kamati pia inaipongeza Wizara kwa kuzifanyia matengenezo makubwa Mahkama za Kadhi; Mwanakwerekwe na Makunduchi.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, pamoja na majukumu mengine, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaratibu masuala mtambuka kwa kuendesha mafunzo maalumu kwa maafisa wa Wizara kuhusu shughuli za watu wenye ulemavu na UKIMWI.
Kamati yetu inapongeza hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuongeza wigo wa kushughulikia masuala haya kwa kuangalia maradhi mengine mbali mbali kama vile sukari na presha ambayo yameongezeka na kuathiri wafanyakazi wengi. Ingawa ni muhimu lakini kampeni ya maradhi ya UKIMWI imefanyika vya kutosha na karibu kila mtu ana uelewa kuhusu janga hilo.

MAHKAMA

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakati inawasilisha ripoti yake ya mwaka 2014 ilitoa mapendekezo mengi na ushauri kuhusu mambo mbali mbali ya kiutendaji wa shughuli za Mahkama. Nia yetu ilikuwa ni kuikumbusha Wizara kuongeza ufanisi katika eneo hili na kuchunga haki za wananchi.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukubali na kutekeleza ushauri na mapendekezo mengi ya Kamati katika ripoti yake, ingawa hatusemi kuwa changamoto hizo zote zimemalizika, bali Kamati inaendelea kutoa msisitizo kwa Wizara kuendelea kukabiliana na changamoto hizo ili kuirejesha hadhi ya Mahkama zetu ziendelee kuwa eneo la matumaini na haki kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nilitangulia kuipongeza Wizara kwa kufanikisha ukarabati wa majengo ya Mahkama, lakini bado kuna changamoto ya ubovu wa jengo la Mahkama ya Chake Chake. Kamati yangu ilitembelea jengo hilo na kulikuta katika hali ya uchakavu mkubwa. Mahkama hiyo haina eneo la kuhifadhi mahabusu lenye viwango vinavyozingatia haki za binadamu.

Mhe. Spika, katika Mahkama hiyo ya Chake Chake jengo la kuhifadhia mahabusu wanaongojea kesi zao halina paa na choo wanachotumia ni kibovu. Kamati yetu imeshuhudia jinsi mahabusu wanavyowekwa bila ya udhibiti wa uhakika, hali hiyo inaweza kusababisha hatari kwa usalama wao na wa askari wanaowalinda.

Kamati yangu inarejea tena kuitaka Serikali kwa mwaka ujao wa fedha ijitahidi kutoa fedha za kutosha na kwa wakati ili ukarabati mkubwa ufanyike kwenye jengo la Mahkama hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu bado hairidhishwi na kasi ndogo ya utoaji wa maamuzi ya kesi katika Mahkama zetu. Wakati Mhe. Waziri anawasilisha hotuba yake ametueleza takwimu za kesi zilizopokelewa na kutolewa maamuzi katika kipindi cha Julai hadi Machi 2014; ambapo kwenye maamuzi ya kesi za Mahkama ya Watoto kati ya kesi 79 zilizopokelewa ni kesi 4 tu ndio zimetolewa maamuzi. Takwimu hizo bado ni ndogo na haziridhishi ukilinganisha na idadi ya kesi zilizopokelewa.

Mhe. Spika, Kamati inatambua baadhi ya changamoto zinazosababisha kasi ndogo ya utoaji wa maamuzi katika kesi. Hata hivyo, bado Kamati inasisitiza ushirikiano wa kweli na wa matendo ufanyike kwa wadau wote wa kesi, kuanzia Mahkama, Polisi, Waendesha Mashtaka na Mawakili ili kuitatua changamoto hii. Kamati yangu inaagiza Vikao vya Kutathmini Uendeshaji wa Kesi *(Case Flow Management*) vifanyike mara kwa mara na Kamati ipewe taarifa ya maazimio yake ili ifuatilie utekelezaji wake.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, Kamati yangu inatoa wito kwa jamii kushiriki na kujitokeza Mahkamani kutoa ushahidi ili kufanikisha uendeshaji wa kesi wa haraka. Aidha, vyombo vya kusimamia sheria navyo kama vile Polisi

na Mahkama vifanye kazi kwa uadilifu na kufuata taratibu ili kuwajengea imani wananchi waje kutoa ushahidi kila wanapohitajika.

Mhe. Spika, wimbo wa kutafutwa mashine ya *DNA* umeshakuwa maarufu masikioni mwetu na ahadi nyingi tumeshapewa na Serikali ya upatikanaji wake. Kamati yangu ina mashaka kama kweli Serikali imeweka utafutwaji wa mashine ya *DNA* kuwa miongoni mwa vipaumbele vyake. Kamati yangu imesharipoti mara nyingi shida inayopatikana katika kutafuta ushahidi hasa kwenye kesi za udhalilishaji wa kijinsia kwa kutumia utaratibu wa kizamani wa kuona na kusikia.

Mhe. Spika, tunaomba maelezo kutoka Serikalini ya lini wimbo wa kutafutwa mashine ya *DNA* utakamilika. Kamati yangu wakati inafanya maandalizi ya hotuba hii imepata taarifa kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo vya Serikali kuwa vipo vielelezo vingi vinavyohusu kesi za udhalilishaji vimewekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja vyengine vikiwa vinaharibika vikisubiri kupelekwa Dar es Salaam kufanyiwa vipimo vya *DNA.* Katika hali kama hiyo ya kusikitisha, Kamati yangu inahoji je, bado Serikali haioni haja ya kuwa na mashine ya *DNA* hapa kwetu?

Mhe. Spika, Kamati yangu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili kusimamia maamuzi na maazimio ya Baraza yaliyotolewa kwenye hoja binafsi ya kupinga vitendo vya udhalilishaji iliyowasilishwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwenye Mkutano wa Kumi na Tano wa Baraza hili, ambayo pamoja na mambo mengine ilitaka Serikali kuharakisha kutafutwa mashine ya DNA itakayosaidia uchunguzi katika kesi za udhalilishaji na kuitaka serikali itekeleze maazimio hayo, ikiwemo hili la mashine ya *DNA* imefikia wapi?

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kukamilisha ujenzi wa jengo lake na kuhamia. Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kulitunza jengo hilo vizuri ili lidumu kwa muda mrefu. Vile vile kamati inaipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kutekeleza kwa vitendo masharti ya sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu; kazi na majukumu yake Sheria Nam. 6 ya 2013 ambapo afisi hiyo imeanzisha vitengo vya usimamizi wa mikataba, usimamizi wa kesi, uandishi wa sheria, maendeleo ya afisi na wafanyakazi na Kitengo cha Utawala pamoja na usimamizi wa vitengo hivyo.

Tumezoea kuona sheria nyingi zinapitishwa Barazani na utekelezaji wake unasuasua. Tunaomba taasisi nyengine ziige mfano mzuri wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kutekeleza sheria kwa vitendo.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*):

Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi yenye ustaarabu na inafuata utawala wa sheria. Haipendezi tuendelee na utaratibu wa kuendesha mashtaka kwa kutumia Polisi. Kamati yangu inaunga mkono na kupongeza juhudi kubwa ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuendeleza mpango wa kuendesha mashtaka kiraia katika wilaya zote za Zanzibar.

Mhe. Spika, tutambue kuwa serikali yoyote duniani inakuwa na malengo. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilielezwa katika kifungu cha 9 (2) (d) ambalo ni usalama na hali nzuri kwa wananchi. Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka popote pale duniani ni miongoni mwa vyombo muhimu vya kidola vinavyofanikisha lengo hili kuu la serikali.

Mhe. Spika, bahati njema Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar imepata kiongozi mwenye uwezo mkubwa kiutendaji Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim pamoja na mawakili wake anaowaandaa vizuri kuitumikia serikali yao. Katika kufanikisha lengo hilo kuu la Katiba, Kamati yetu inapata mashaka makubwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wa Zanzibar kuweza kufanikisha lengo kuu la serikali kwa ufanisi kutokana na afisi hiyo kutengewa fedha kidogo kwenye bajeti yake. (*Makofi*).

Mhe. Spika, bajeti hiyo ndogo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka inarudisha nyuma mipango mizuri ya afisi na kweli inavunja moyo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na mawakili wetu. Kamati inaitaka serikali kukaa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kutizama vipaumbele vya afisi ili mipango ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itekelezwe kwa ufanisi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, ijapokuwa fedha zinazoingia kwenye bajeti hii ni ndogo, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni miongoni mwa taasisi ambazo kamati yetu ni namna inavyofanya matumizi ya fedha kwa umakini na kwa kuzingatia tathmini ya fedha. Ni dhahiri kuwa iwapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itapatiwa bajeti ya kutosha itaweza kutekeleza mipango yake mingi kwa muda mfupi tu. (*Makofi*).

Afisi ya Msajili wa Haki Miliki.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako katika eneo hili ninataka nizungumze kwa maneno marefu ambayo kidogo ni makali mno. Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza Afisi ya Msajili wa Haki Miliki ambayo mnamo wa mwezi Oktoba, 2013 iliweza kugawa mirabaha kwa wasanii na wabunifu wetu. Hayo ni mafanikio makubwa ya kazi inayofanywa na Afisi ya Msajili wa Haki Miliki. Kamati inawapongeza wadau wote waliochangia na kufanikisha zoezi la ugawaji wa mirabaha na kuchukua hatua hii kuwataja kama ifuatavyo.

Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*), *Vodacom, Zanzibar Cables and Television*, *Zenji FM Radio*, *Coconut FM Radio.* Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Nassor Salim Ali Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo, Dkt. Mahadhi Juma Maalim-Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Muyuni. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kamati pia inavipongeza vituo binafsi vya redio na televisheni vya hapa Zanzibar ambavyo vimekuwa vikilipa vizuri mirabaha. Vituo hivyo ni:-

1. *Chuchu FM*
2. *Hits FM*
3. *Zanzibar Cables and Television*

Kamati yangu inaomba vituo hivyo kuendelea kushirikiana na serikali katika kuinua wasanii wetu wanufaike na kazi zao. Aidha tunaviomba vituo vyengine binafsi kuiga mwenendo huo mzuri wa kuthamini nguvu za wasanii wetu.
Mhe. Spika, sambamba na hilo, Afisi ya Msajili wa Haki Miliki imeanza kufuatilia haki za wasanii kupitia hoteli mbali mbali ambazo zimekuwa zikitumia kazi hizo na kazi hiyo inaendelea vizuri. Changamoto inayoikabili afisi hii katika ufuatiliaji huo ni uhaba wa watendaji. Kamati inaitaka wizara kusaidia afisi hii kupata nafasi za kuajiri watendaji wa ziada katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015.

Kamati yangu inatoa shukurani na pongezi maalum kwa uongozi wa Hoteli ya Serena kwa kukubali kufanya malipo ya kazi za wasanii kwa mwaka mzima; 2014/2015. Tunazikumbusha hoteli nyengine zinazotumia kazi za wasanii na wabunifu kufanya hivyo.

Mhe. Spika, wakati tunapongeza mafanikio hayo, naomba nieleze masikitiko makubwa ya Kamati yangu kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Shirika lake la Utangazaji la *ZBC* ambalo kwa muda mrefu sasa limeshindwa kulipa deni la mirabaha ya shilingi milioni 50 huku vituo vyake vya *ZBC* na *TV* pamoja na redio vikiendelea kutumia kazi za wasanii hao bure.

Mhe. Spika, katika kikao kama hichi cha bajeti cha mwaka jana 2013/2014, Mjumbe mahiri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Wanu Hafidh Ameir alisimama kuzuia kifungu katika bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, akitaka maelezo ya lini deni la mirabaha litalipwa. Mhe. Waziri alitoa ahadi kuwa deni hilo litalipwa ifikapo mwezi wa Oktoba mwaka jana. Ninasikitika kusema kuwa mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

Mhe. Spika, sote tunafahamu ukweli kuwa serikali hii haiwezi kumuajiri kila mtu. Vijana wetu wameamua kujiajiri katika kazi za sanaa mbali mbali na ubunifu kwa nia ya kujipatia kipato, na serikali imeamua kwa dhati kuwaunga mkono kwa kuanzisha Afisi ya Kusajili Kazi zao ili wasanii hao waweze kufaidi matunda ya kazi hizo.

Mhe. Spika, Shirika la *ZBC* kupitia vituo vyake ni watumiaji wakubwa wa kazi za wasanii kila siku lakini wamekuwa ni wadaiwa sugu wa malipo ya kazi za wasanii tangu mwaka 2012. Kati ya shilingi milioni 50 ambazo *ZBC* inadaiwa ni shilingi milioni 1 tu imelipwa. Fedha hizo chache zimepatikana baada ya mazungumzo kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, jambo linalosikitisha zaidi ni kuona *ZBC* ni shirika ambalo lipo chini ya wizara ambayo ndio baba na mama wa wasanii. Tulitegemea *ZBC* ingekuwa mstari wa mbele kufanya malipo ya mirabaha kwa wasanii hao hasa ukizingatia kuwa vituo vyake vimekuwa vikitumia kazi za wasanii kwa kiwango kikubwa, na ndio shirika hilo hilo linalotoa elimu kuhusu kulindwa kwa haki za wasanii na wabunifu huku lenyewe likitenda kinyume chake.

Mhe. Spika, Kamati yangu inastaajabu kwa kuona kuwa hata vituo vidogo vya *libraries* vinavyokodisha kazi za wasanii vinaweza kulipa mirabaha huku vituo hivyo hivyo vikitumia sehemu nyengine ya mapato yao kulipa kodi serikalini. Tunashindwa kufahamu ni vipi Shirika la Utangazaji la Serikali linaloendeshwa kwa kodi hizo hizo kushindwa kulipa mirabaha na huku likiendelea kunywa jasho la wasanii wetu.

Mhe. Spika, hili halikubaliki, linaitia aibu serikali yetu inayotaka kuinua haki za wasanii wetu. Ninachukua fursa hii kuwataka Waheshimiwa Wajumbe tuungane kwa pamoja kuitaka Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; ambayo *ZBC* ipo chini yake kuwalipa wasanii na wabunifu fedha zao mara baada ya bajeti hii kupita na kabla ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haijaletwa hapa Barazani.

Mhe. Spika, Kamati tumeamua kuweka wazi ukweli huu sio kwa nia mbaya bali kuungana na juhudi za Mhe. Rais wa Zanzibar ambaye siku zote amekuwa mstari wa mbele kututaka tubadilike na tusifanye kazi kwa mazoea. Tunalitaka Shirika la Utangazaji la Zanzibar kwenda sambamba na kauli mbiu ya kiongozi mkuu wa nchi ya kututaka tubadilike na kuacha mazoea ya kutumia kazi za wasanii bure, au kama shirika hilo haliwezi kulipa haki za wasanii liache mara moja kutumia kazi za wasanii hao. (*Makofi*).

Mhe. Spika, malipo haya ya mirabaha sio ya hiyari bali ni matakwa ya sheria Nam. 14 ya 2003 tuliyotunga sisi wenyewe hapa Barazani. Inashangaza kuwa sheria hiyo inavunjwa na taasisi ya serikali ambayo ilitakiwa kuwa mfano kwa taasisi nyengine kwa kufanya malipo ya mirabaha hiyo kwa wakati. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba nilikumbushe Baraza lako umuhimu wa taasisi za serikali na jamii kwa kutekeleza sheria kwa vitendo kwa kutumia maneno ya busara ya Jaji Bhagwati, katika kesi moja maarufu nchini India ya Bandhua *Mukti Morcha Vs Union of India (1983) 3:* dhidi ya Muungano wa India ambayo ilitolewa maamuzi mwaka 1984 na ilikuwa ni kesi Nambari 3 ambayo alisema maneno yafuatayo, kwa ruhusa yako naomba niyanukuu. *"We must not be content with law in the books, but we must behave the law in action it necessary that law must not only speaks justice but also deliver justice".*

Mhe. Spika, kwa lugha rahisi na ya kawaida, maana yake ni kwamba tusiridhirike na sheria zetu kuwa katika vitabu tu, bali inatulazimu kutekeleza sheria hizo kwa vitendo, na ni vyema kufahamu kuwa haitoshi kuona sheria kuzungumzia kuhusu haki tu, bali inalazimu pia kuonekana sheria hiyo inatoa haki hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaiagiza Afisi ya Msajili wa Haki Miliki kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria ya Hati Miliki Nam. 14 ya 2003 kuvifungia vituo na taasisi ambazo zinatumia kazi za wasanii bila ya kulipa mirabaha.
Aidha tunaitaka taasisi hiyo kuendelea na juhudi za kuelimisha wasanii na wabunifu kutambua umuhimu wa kusajili kazi zao ili wanufaike na jasho lao.

Mhe. Spika, mbali ya kazi kubwa inayofanywa na Afisi ya Msajili wa Haki Miliki bado afisi hii haina afisi ya kutosha kufanya kazi zake. Jengo wanalotumia hivi sasa ni finyu na chakavu. Jengo hilo halina sehemu nzuri ya kuhifadhia nakala za kazi za wasanii zinazosajiliwa kama vile *CD*, nyaraka na kadhalika.

Aidha, afisi imekuwa inakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi ambapo kwa mwaka ujao wa fedha imetengewa nafasi tano za ajira.

Mhe. Spika, Kamati yangu inatoa ombi maalum kwa serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kuwa mara baada ya ujenzi wa jengo jipya la wizara liliopo Mazizini kukamilika, Afisi ya Msajili wa Haki Miliki inapatiwa nafasi ya kuweka afisi zake katika jengo hilo jipya.

Mhe. Spika, Kamati pia inalipongeza Shirika la Ubunifu Ulimwenguni kwa kukamilisha mapitio ya sheria ya Haki Miliki Nam. 14 ya 2013 ambayo imo katika utaratibu wa wa kufanyiwa marekebisho. Shirika hilo liliwapa nafasi

wataalamu kutoka Afisi ya Haki Miliki na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwenda Geneva kujadili rasimu ya marekebisho ya sheria hiyo hadi kukamilika kwake.

Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Spika, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imepiga hatua kubwa ya kupongezwa. Kamati imeshuhudia jitihada zinazofanywa na Mrajis za kuongeza wigo wa huduma za usajili katika wilaya zote za Unguja kwa kufanya matengenezo ya ofisi za usajili, na juhudi hizo zinaendelea Kisiwani Pemba kwa mafanikio makubwa.

Kamati inampongeza Mkurugenzi wa Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo Ndugu Shaaban Ramadhan Abdalla. Juhudi zake na watendaji wake zinaonekana katika kuimarisha huduma za usajili wa vizazi na vifo nchini.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa takwimu za usajili wa vizazi kwa mwaka unaomalizika, afisi imesajili vizazi 36,826 na vifo 2,228. Takwimu zinaonesha usajili wa vifo ni mdogo. Kamati inatoa wito kwa jamii kuona umuhimu wa kusajili vifo.

Aidha, tunawaomba Waheshimiwa wa Baraza hili Tukufu kufanya juhudi za kutoa elimu kwa wananchi majimboni mwao kuhusu umuhimu wa kusajili vizazi na vifo.

Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mhe. Spika, Kamati tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya utendaji wa kazi ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Tunampongeza Mwenyekiti wa Tume Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakari na Katibu wake. Uteuzi wao umeshuhudia mageuzi makubwa ya Tume hii ambayo sasa matunda ya uwepo wake yameanza kuonekana.

Aidha, Kamati inawapongeza watendaji wote wa Tume kwa juhudi zao za kuinua hadhi ya Tume hii muhimu kwa maendeleo ya sheria za nchi yetu.

Mhe.Spika, licha ya kazi nzuri inayofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya Mhe. Waziri bado fedha wanazoingiziwa kwa shughuli zao ni kidogo. Tukumbuke kuwa Tume hii kabla ya kufanya mapitio ya sheria inazunguka kufanya utafiti maeneo mbali mbali nchini ili kujua mapungufu ya sheria inayopitiwa.

Tunaishauri serikali kuhakikisha kuwa Tume inatengewa fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi za utafiti na mapitio ya sheria na kuiwezesha nchi yetu kuwa na sheria bora zinazotekelezeka. Ninachukua fursa hii kupongeza juhudi za wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuwapatia jengo la kudumu kwa ajili ya kufanya shughuli zao baada ya kuhangaika kwa muda wa miaka miwili bila ya kuwa na ofisi ya kudumu.

Afisa Msajili wa Mali na Biashara.

Mhe. Spika, moja ya malengo ya utekelezaji wa ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kuijengea ofisi uwezo kiutendaji. Kamati inapata wasi wasi wa utekelezaji wa lengo hili, kwani licha ya shughuli nyingi na kubwa za Afisi ya Msajili wa Mali na Biashara, mwaka jana imeingiziwa asilimia 31 tu ya fedha za kazi za kawaida huku wenyewe ikiwa imekusanya asilimia 78 ya mapato yaliyokadiriwa.

Kamati yangu imewahi kupendekeza kuwa Afisi ya Msajili wa Mali na Biashara ipatiwe fungu lake (*vote*) na ipewe uwezo wa kubakisha sehemu ya mapato inayokusanya ili iweze kufanikisha malengo ya utekelezaji wa kazi zake. Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake huo ufanyiwe kazi.

Afisi ya Mufti.

Mhe. Spika, Kamati yangu inatambua mchango mkubwa wa Afisi ya Mufti na inampongeza Mufti na afisi yake kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji wa maadili ya jamii, kutatua migogoro ya misikiti, misaada kwa madrassa zetu pamoja na kuhamasisha jamii kulinda amani na utulivu wa nchi.

Kamati inashauri Afisi ya Mufti kupitia Baraza la Maulamaa kufanya juhudi mara kwa mara za kuyafikia makundi mbali mbali ya jamii na kutoa elimu zaidi ya mporomoko wa maadili unaoendelea kuleta athari katika jamii yetu.

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, tumeelezwa katika hotuba ya Mhe. Waziri kuhusu changamoto zinazoikabili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ambazo ni uelewa mdogo wa wananchi wengi juu ya umuhimu wa mirathi, amana, wakfu na zakka pamoja na teknolojia isiyoendana na wakati katika usimamizi na utoaji wa huduma katika Kamisheni.

Kamati inaitaka wizara kueleza hatua ilizozichukua kutatua changamoto hizo hasa ile ya mapungufu ya utaalamu wa kisasa. Mhe. Spika, tumekuwa na matatizo mbali mbali yanayowakabili wananchi wanaokusudia kwenda Makka kuhiji kila msimu wa Hijja unapofika. Hasa upatikanaji wa taarifa sahihi kwa Mahujaji.

Taasisi nyingi zimekuwa zikitoa ahadi kwa Mahujaji ya kuwapatia huduma za ukaribu huku kukiwa na malalamiko baadhi ya huduma zao kutopatikana au kutotosheleza. Mhe. Spika, tunaitaka Kamisheni ya Wakfu kuhakikisha vikundi vyote vinavyosafirisha Mahujaji kutoa taarifa za uhakika na kuhakikisha kuwa huduma zinazoahidiwa kwa Mahujaji zinapatikana na zipo kwenye uwezo wa vikundi husika. Vyenginevyo vikundi vitakavyoshindwa visipewe kibali cha kusafirisha Mahujaji.

Afisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaendelea kusisitiza kwa wizara kuhakikisha kuwa Afisi Kuu Pemba inapatiwa fedha za kawaida kwa wakati na kwa kasma iliyopangiwa ili kuhakikisha shughuli za uratibu wa kazi za wizara zinafanyika kwa ufanisi. Taarifa ya Waziri imeonesha kwa mwaka unaomalizika ni kiwango kidogo cha fedha za *other charges (OC)* yaani matumizi ya kazi za kawaida zilizoingizwa ambapo ni asilimia 37 ya makadirio hadi kufikia mwezi Machi, 2014.

Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati yangu inaunga mkono hotuba na bajeti ya Mhe.Waziri na inawataka Wajumbe kuchangia, kushauri, kupendekeza na hatimaye kupitisha bajeti hii ili wizara itekeleze kazi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Siku zote Wizara ya Katiba na Sheria imekuwa watiifu kwa Baraza na Kamati zako, hii inatokana kuwa watendaji wa wizara hii wengi ni wanasheria na walimu kitaaluma ambao nidhamu yao kiutendaji ni ya kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja ya Mhe. Waziri sambamba na kuomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri kwa hoja mbali mbali nilizozitoa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru na sasa tunaendelea na uchangiaji wa jumla. Nimkaribishe basi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadaye afuate Mhe. Hamza Hassan Juma na hatimaye Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, kabla sijainuka nashangaa sana hii spika yangu imejiwasha yenyewe *automatically*, kwa kweli inaonesha ni suala la kushangaza sana, *Wallah* sijapata kuona. Sijabonyeza nainuka na spika inawaka, nashukuru sana kwa baraka zake Mwenyezi Mungu leo hii.

Mhe. Spika, nianze katika ukurasa huu wa 10, lakini kwanza nataka niseme hivi, kusema kwangu sina madhumuni mabaya sana, lakini nina lengo zuri la kujenga Ofisi hii iwe ina ufanisi mzuri katika utendaji wake wa kazi, kwa sababu ni muhimili mmoja mkubwa sana.

Mhe. Spika, nitazuwia fungu na kuna mambo mawili au matatu niweze kupewa, halafu baadaye fungu hilo nitaliwachia la mipango na sera au nitamnyang'anya shilingi yake Mhe. Waziri, asipate kutumia mshahara wake. Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu kuna mambo lazima tuseme. Kwanza waziri namtaka aje kunijibu. Je, amefanya ziara ngapi katika *Departments* zake, nakata hilo aje kuniambia na huo ndio mtiririko ambao nitakwenda nao sasa hivi, kwa sababu nataka kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Shein.

Mhe. Spika, maana yake unajua watu wanapewa vyeo, mawaziri, makatibu na wengineo, lakini wanakuwa mawaziri meza, makatibu meza hawatembelei katika sehemu zao wakajua yale matatizo na ndio maana wanampa kazi kubwa sana Mhe. Rais katika utendaji wake wa kazi.

Mhe. Spika, katika bango kitita na yeye Mhe. Rais atakapowaita awaulize, jamani nyinyi mmefanya ziara ngapi katika *Departments* zenu ili kutafuta matatizo. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lisikilize hili suala ni muhimu sana na kama wataweza Waheshimiwa Mawaziri kufanya hivyo, basi sidhani kama Wajumbe wenzangu hapa Baraza la Wawakilishi wataweza kuja kupiga buti baadaye, lakini wanafanya kutokana na hivyo, wao wanakaa kama hivyo, waziri anakaa kwenye kiti na masuala yamekwisha. Sasa kasoro zinakuwa zinatokana na hivyo.

Mhe. Spika, Mahakama tunajua kama ni muhimili mkubwa sana, lakini kuna mambo yanasikitisha Mhe. Waziri, atanisaidia na sidhani kama ni yeye, yeye kwa sababu anajenga hoja ya bajeti yake ya kuendesha ile wizara yake, lakini wizara husika inayozitilia fedha zinawatilia pesa ambazo hazitimii hata ile asilimia. Sasa leo Mahakama Kuu ambayo ni muhimili mkubwa inafanyiwa hivi, halafu tunasema rushwa, watakula nini, jamani tusikimbilie kutizama rushwa, hebu tizameni utendaji wao ukoje? Lazima kesi ziende kidogo kidogo, kwa sababu hata karatasi wanashindwa kuwa nazo, unafikiri iwe vipi?

Mhe. Spika, tuwe *serious* na hiki chombo, tusifanye masihara, tuwe *serious* na hizi Mahakama zetu. Hii mihimili sio kitu cha kuchezea Wenzetu Ulaya mihimili kama hii, basi ni wengi ambao utawakuta katika wizara zao na hata katika bajeti zao hazipungukiwi hata senti tano, lakini tumefanya kosa moja kubwa sana na hili kosa ndio linalotufanya mihimili hii isiheshimiwe.

Mhe. Spika, tulileta sheria ya kuunda Tume ya Utumishi, lakini hapo hapo ndani yake hii Mahakama kuna Tume yao hii ambayo haifanyi kazi yoyote, Katiba hii hapa, *Supreme* Katiba hii hapa, lakini tumeiwacha, ndio maana hawa wanapata tabu, kwa nini wasiwe na mfuko wao Mahakama? Wizara inavaa koti la Mahakama kwa sababu ni kitu kinyume na utaratibu na atafanya nini wizara, ni lazima itavaa koti la Mahakama. Suala hili linasikitisha sana.

Mhe. Spika, naomba sana serikali iwatengee mfuko maalum wa Mahakama katika mambo yake ya kuendesha Mahakama, utaziomba Mhe. Abubakar Khamis pesa chungu nzima, huna kimoja utakachokipata, kwa sababu ya kuidharau na kutokufahamu madhumuni ya Mahakama kuwa nayo. Jamani muhimili uheshimiwe kwa mujibu wa utaratibu na tumeambiwa hapa kila muhimili husika uheshimiwe kwa mujibu wa sheria zake. Baraza la Wawakilishi, Mahakama na muhimili mwengine.

Mhe. Spika, kwa kweli kasma zao hazijanifurahisha sana na ndio maana nikasema nazuia fungu uje kuniambia ni nani hasa haku-*complete* mambo ya bajeti zako, niambie yeye nitamsema, ukishaniambia wewe umenawa na fungu lako mimi nitaliachia, lakini usipomsema nitakuzuilia fungu lako, kwa sababu sio kitu cha kufanyia masihara hiki. Mmejitahidi sana katika kitabu chenu, tumeona baadhi ya Mahakama, tizama basi Mahakama hii imetengenezwa imekuwa nzuri sana, *Wallah* imetulia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wanashindwa hata kulipa fedha za wale ma-*assessors*, mashahidi niambie unafikiri wataendeshaje sheria hizo, watafanya vipi kazi zao hizo wakati hawa ambao ni wahusika mashahidi hawaendi kule Mahakamani, kesi ni lazima itazoroteshwa, lakini shahidi akijua kuwa fedha zipo, ma-*assessors* wakijua fedha zipo watakwenda kwa wingi tu na kwa wakati, lakini sasa wakipungua hao kwa mujibu wa taratibu kesi haziwezi kwenda.
Mhe. Spika, kwa hivyo, tusiwatafutie wachawi hawa majaji wetu, bado tunaye huyu mchawi hatujataka kumsema, kwa sababu tungeweza kumsema, basi na hawa wangeweza kufanikiwa katika utendaji wao wa kazi. Kwa kweli suala hili linasikitisha sana, tena linasikitisha sana na ni suala ambalo sio zuri sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Jaji Mkuu wetu anatakiwa awe na nyumba na gari nzuri, lakini mazingira yake Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar, mimi nashangaa sana wala hana yale mazingira ya Kiujaji, maana mnampa jina tu Jaji Mkuu, kila jambo lina mambo yake kwa mujibu wa utaratibu, mpeni haki yake. Tungemchukua mtaalamu kutoka nje, basi mngempa nyumba nzuri, mngempa gari nzuri kamili na kila kitu ndani mngemtilia, lakini leo Mhe. Jaji Mkuu wetu hapa Zanzibar, kwa kuwa mtoto wa hapa kazaliwa tunamfanya hivi. Sio utaratibu unaotakiwa, twende na wakati na ni lazima haya mambo afanikiwe kutokana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa tuko katika mchakato wa Katiba na katika Katiba ambao inayotarajiwa *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akijaalia uhai na uzima italetwa tu, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Nina imani hiyo binadamu kapewa akili na Mwenyezi Mungu sio mnyama aliyekuwa kanyimwa akili, hicho kitu kitakuwepo, lakini nataka nimuulize Mhe. Waziri na yeye kasoma sheria na jambo lolote unaanza kuandalia mapema hasa nguo ya Ijumaa unaanza kuiandaa mapema, unaanza kuiandaa Jumatano wala usingoje Alhamis, pengine ikaja mvua hatimaye ukaikosa.

Mhe. Spika, je, tumejiandaa vipi katika masuala haya, maana yake huko tutakuwa na *Supreme court* tutakuwa na *Court of Appeal* huko, kutakuwa na mambo mengine. Sasa hayo matatizo leo ukiangalia tuna mtu mmoja tu Mhe. Mbarouk, huyo akifa, ndio basi tena kwa Zanzibar hatuna mtu mwengine. Sasa tuona mambo haya sasa hivi tujiandae mapema, tuwatafute watoto tuwapandishe tusione tabu kuwapandisha, hata kama hamna mshahara, mpandisheni cheo mshahara mtamfanyia baadaye. Nakuomba sana Mhe. Waziri uje unieleze huu utaratibu ambao tunakwenda nao sasa hivi tunajiandaa vipi na hawa watu.

Mhe. Spika, kawaida yetu siku zote tunachelewa kuandaa vitu kama hivyo, hatimaye likitokezea jambo hatuna pahapa pakwenda kutafuta. Naomba sana huu ushauri muupokee. Juzi Mhe. Ali Mzee alitoa ushauri mzuri sana kwamba mawaziri kuweni karibu na sisi na kupokea ushauri wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi siku zote nasema sikusoma kama walivyosoma watu, lakini nimejifunza nimetambua. Wala sina haja ya kujisifu, niletee mtu mwenye *PhD*, niletee mtu gani halafu unilinganishe na mimi, mimi nampita tu sio masihara, kwa sababu natoa vitu vyenye kina na vina kabisa vyenye uhakika, sitowi vitu vya kubahatisha. Nikisema natoa vitu vya uhakika kabisa kutokana na hali halisi ilivyo. Sasa leo tumeshakubaliwa Katiba ile kupita na kama hatukujiandaa hawa Majaji wa Mikoa tukaanza kuwapandisha juu na wengine tukawatafuta tukaanza kuwafanyia majaribio, jambo likitokezea ndio tunaanza kukamatana, hatimaye nafasi hakuna tunabakia kukaa pembeni tukalia. Jamani mimi naomba sana Mhe. Waziri, hili suala tulione kwa uangalifu kabisa ili kuweza kusaidia hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, kuhusu Mahakama zetu za wilaya zote ni mbovu, kwa sababu ya kusema ni mbovu, hizi Mahakama kama nilivyokuambia mimi ni mihimili ambayo inatakiwa iende na wakati, lakini nashangaa sana na sijui, sheria inasemaje. Sheria kwanza unatakiwa wewe mwendesha mashtaka uwe na akili pale unapoendesha ile kesi, lakini leo wewe unajichanganya utasema hili jengo wakati wowote litaanguka kesi hiyo utahukumu vipi, tuangalieni sio kitu cha masihara kwa sababu unatakiwa muendesha mashtaka pale ambapo ni Jaji, lakini Hakimu unaweza kumuweka katika mazingira mazuri, Mahakama yake ikawa nzuri na akatoa maamuzi yake kwa uhakika kabisa bila ya kuwa na wasi wasi wowote.

Mhe. Spika, hilo nalo tuliangalie kutokana na kumchanganya mtu akili na kutokana na hali halisi ilivyo. Naomba sana Mahakama zetu zimekuwa mbovu kabisa, naomba tuziendeleze na tuzitengeneze ili tuweze kwenda na wakati na huu muhimili wenyewe kama umo kwa mujibu wa Katiba yetu inayosema ya Zanzibar, kwa sababu imo ndani ya Katiba ya Zanzibar, tumeupa nguvu kabisa.

Mhe. Spika, kuhusu kesi za ubakaji, kesi hizi hasa za kudhalilisha watoto wadogo wanaume, suala hili linasikitisha sana. Naomba sana ikiwa kama ni Tume au ni nani, lakini nitakuja kuona, nimewaambieni mwaka fulani wa bajeti nilisema sheria jamani zimeshapitwa na wakati, sheria zinataka kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, kuna hiki chombo kinaitwa *DNA*, kuna vitu ambavyo viki-*weak* tu katika ule uchunguzi wao, basi ule ushahidi wote unapotea. Hatujavipa kipaumbele, serikali hii kweli tunawataka hawa watoto wawe wa Taifa la kesho, tuko *serious* katika utendaji wake kweli jamani.

Mhe. Spika, nataka nikuambie mimi nadhani Mhe. Rais hawakainaye kama rafiki, hamkai naye mawaziri, mnamuogopa Mhe. Rais. Mbona Mhe. Rais mtu mzuri, jana tu *Alhamdulillah* nimempa mkono tukapiga picha mimi na yeye vizuri tu anacheka kabisa, nikajua *Alhamdulillah* kumbe wanamuonea bure, mnamuogopa bure Mhe. Rais wenu. Hata mimi nilikuwa namuogopa mwanzo Dkt. Shein, sikufichi, lakini jana *Alhamdulillah Rabil Allamina* ametaka nafasi maalum ya kupiga picha mimi na yeye, basi tulikaa pahala pazuri tukapiga picha, basi nikajua kwamba mawaziri wetu hawakai na yeye kirafiki kumueleza hali halisi za mawizara yao.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Aa! Mhe. Spika, naendelea najua utaniongeza tu leo, mimi ndio wa mwanzo. Hiki chombo ni kitu muhimu sana, mimi naamini kama wangekwenda kumwambia Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili nendeni kwa Mhe. Rais katoweni maelezo haya, hamuwezi kufanikiwa, sio kitu cha mchezo, watoto wetu wadogo wanadhalilishwa.

Mhe. Spika, mimi nimeona mwenyewe kwa jicho langu, vidume viwili vishabash, mtwana huyo kenda kuwadhalilisha, halafu leo tunaona ni rahisi. Jamani tumezaa, hakuna mtu asiyezaa humu, sote tuna watoto, tusifanye mchezo. Usione leo mnamnyooshea vidole wewe na vyako wewe vinakuelekea, sio kitu cha mchezo watoto wadogo. Mimi hapa sikubaliani napo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, kinachokukwaza ni nini Mhe. Waziri njoo tuambie tukusaidie hapa, ama faima, lakini hiki kitu kipatikane sio kitu cha mchezo.

Mhe. Spika, na azimio hilo, halafu isitoshe Mhe. Mgeni aliitoa hii hoja, uchungu wa mwana ulimuuma, mama ambaye ndio yeye anayebeba ile mimba mpaka akazaliwa yule mtoto, uchungu alionao kwa kuona yule mtoto anadhalilishwa. Hii hoja imefikia wapi? Naomba sana lifanikishwe haraka hili suala ambalo linauma sana.

Mhe. Sipika, nimalizie haraka haraka Tume ya Kurekebisha sheria naomba sana itume haraka ituletee sheria, kwa sababu tayari sheria zipo zinaonesha wazi zina mapungufu, kwa mfano leo mtu mwenye madawa ya kulevya sio rahisi kumtia ndani hata siku moja ukamfunga, kutokana na ile sheria kuwa na mapungufu. Mimi nimeshasema sana kuhusu hili suala na nitaendelea kulisema.

Mhe. Sipika, vile vile, katika ukurasa wa 20 kuhusu Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Nawaomba na hawa, pengine wana mapungufu ya usafiri. Siku nyengine inawezekana kesi inaweza isiende kwa sababu hawana vitendea kazi, wanabidii nzuri ya kazi na wanauzoefu mzuri wa kazi, lakini wana upungufu wa vitendea kazi, uzoefu unaondoka, hayo tunasema ukweli. Hebu tuwaondolee matatizo madogo madogo hawa watu ili waweze kufanyakazi.

Mhe. Spika, nilikuambieni zamani mambo ya mishahara ndio muhimu sana, tuwaone. Mhe. Abubakar Khamis, Majaji hawa mliowatengenezea *Scheme of service* zao zile, sijui zimefikia wapi fedha zao hawa? Msione tabu tuwapeni hizi fedha, ndio rushwa itaondoka, lakini leo mshahara wake mdogo, anaona donge la fedha liko pale kama shilingi milioni 10, hata mimi nitakula wala sitowacha, eeh, nina njaa sio masihara. Kwa hivyo, naomba sana hili suala liweze kurekebishwa haraka haraka.

Mhe. Spika, nikimalizia kabla hujanipigia kengele niseme kuhusu Mrajis wa Vifo. Suala hili Wajumbe wengi walipiga kelele sana kuhusu vyeti vya kuzaliwa vya watoto, jitihada ni kubwa, watu wanakwenda wengine wanatoka mashamba na kwengineko. Kwa kweli hili suala naomba sana hapa hanapa marekebisho ya jambo lolote, isipokuwa naomba watu waweze kupewa *speedup* ili waweze kufanikisha katika malengo yao waliyokusudia.

Mhe. Spika, katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nimsifu sana Katibu kwa jitihada zake, namuomba sana anapoletewa *documents*, wakati mwengine aziangalie vizuri, ili maafisa wake wasije wakafika pahali wakamuweka pabaya, tatizo ni hilo tu kwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, namuomba sana Katibu wangu awe msikivu.

Mhe. Spika, vile vile, niende katika Hati Miliki kwa kumalizia. Kwa kweli nimsifu sana huyu Mkurugenzi wake. Mkurugenzi huyu kama ingekuwa Wakurugenzi wote Wazanzibari Wakurugenzi hawa wanafanyakazi, basi ingekuwa hakuna matatizo yoyote. Mkurugenzi huyu anajitahidi sana katika kulinda zile Hati Miliki za Wasanii wetu.

Mhe. Spika, katika sehemu za kuuzwa kanda zile anakwenda mwenyewe, anafuatilia mwenyewe na anafika pahala analetewa *message* za vitisho, lakini hababaiki anafanyakazi zake kwa umahiri. Mimi naomba sana tumpe mashirikiano na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu Mhe. Rais amuone sana huyu mama kwa kuwa anajitahidi sana Mkurugenzi huyu kutokana na hali halisi ya kazi zake nzuri sana.

Mhe. Spika, kwa kumalizia sasa, naomba sana...

Mhe. Spika: Haya, muda wako umemalizika nashukuru sana. Muda umemalizika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, haya nakaa kitako, lakini siungi mkono mpaka nipate maelezo yangu kamili. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Namuomba sasa Mhe. Hamza Hassan Juma, aendelee na mchango wakati Mhe. Ismail Jussa anaendelea kujitayarisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii nikazungumza machache sana kwenye Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka niungane na Mhe. Waziri kutoa pongezi kwa viongozi wetu wote wakuu, lakini vile vile, kuwapongeza na wao kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya, lakini vile vile, nampa pole Mhe. Waziri kwa kupewa taasisi ambazo ndio zinazosimamia haki kwa upande wa Zanzibar. Sasa namuomba Mheshimiwa ajitahidi kuzisimamia taasisi hizi, lakini vile vile, awape nafasi yao ya Kikatiba kuweza kusimamia hizo haki kwa mujibu wa Katiba.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwa kumwambia Mhe. Waziri, nitazuia fungu la Mahakama Kuu ya Zanzibar, lakini vile vile nitazuia fungu katika Ofisi ya Mufti kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nitaanza moja kwa moja katika hoja hizo kwa sababu najua sasa hivi muda wetu umeukamata sana.Kwa hivyo, nataka nianze hili la mwanzo, halafu niendelee yale ya mwisho.

Mhe. Spika, nakusudia kuzuia mafungu ya maeneo haya mawili kwa sababu moja kubwa, kuna kesi ya watoto wa muasisi wetu Marehemu Khamis Daruweshi ambayo kesi hiyo kuna nyumba ambayo waliiwacha Wakfu kwa bahati Wizara hii ina walimu wangu watupu, maana yake mpaka huyo Jaji wa Mahakama Kuu mimi ni mwalimu wangu, sasa mtu kumkosoa mwalimu wake kwa kweli pana kazi kubwa sana, lakini ndio wajibu. Kuna watu hapa ambao ni warithi wa Marehemu wameachiwa na Marehemu baba yao na wameeleza vizuri kwamba urithi ule amewataja watoto wake hapa na orodha karibu ya watu 15, sasa kitu cha kushangaza Wakfu ule imetoka amri ya Mahakama kwamba nyumba ile iuzwe pamoja na lile eneo.

Mhe. Spika, sasa mimi najiuliza kwa sababu na sisi ndio tupo hai hapa na sisi vile vile tunategemea Wakfu kwa watoto wetu na tunategemea unapoandika Wakfu unarithiwa na vizazi na vizazi na vijukuu na ndio hata huu Wakfu ulivyoelezea.

Mhe. Spika: Mhe. Hamza, naarifiwa kwamba suala hilo lipo Mahakamani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, Mahakamani limesharudi na nakala nnayo hapa.

Mhe. Spika: Sijui, lakini nimearifiwa kwamba lipo Mahakamani na kama lipo kweli Mahakamani, basi Kanuni zinakataza tusilijadili hapa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, lakini naomba dakika zangu unilinde nataka kutoa ufafanuzi kidogo nimekutana na warithi wa Marehemu na wamenipa *ruling* za Mahakama, tayari Mahakama imeshatoa maamuzi na mali yao imeshauzwa kinyume cha taratibu, sasa Mahakama ikishatoa maamuzi na tendo limeshafanyika, mimi nafikiri maamuzi yameshafanyika, sasa labda muongozo wako kidogo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa kweli sina uhakika kama maamuzi yametolewa au nini, labda tumsikilize aseme, lakini tunaweza kupata taarifa baadae.

Mhe. Spika: Hakuna uhakika Mhe. Hamza endelea, lakini uwe na tahadhari na mchango wako.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na ndio maana nikasema hata Jaji wa Mahakama Kuu mimi ni mwalimu wangu na haya mambo ya mirathi yeye ndiyo aliyenisomesha, lakini sasa yeye sio hakimu wa Mahakama ya kazi, yeye ni Hakimu wa Mahakama Kuu, lakini hili suala lina ncha mbili, lakini kitu ambacho ninachokisema na mimi

kitu cha mwanzo walipokuja niliwauliza, je, hili suala haliko Mahakamani? Wakanambia Mahakamani tumeshamaliza na *ruling* imeshatoka, sasa hii *ruling* ndio wao kwa kweli iliwapa mashaka kwa sababu hili suala lilizungumzwa kwenye Mahakama ya Kadhi, kulikuwa na mgogoro wafamilia kama unavyojua familia zetu, lakini baada ya kutolewa hukumu hawa warithi wakenda kukata rufaa na ile *ruling* ya Mahakama ya Rufaa hapa pia ninayo ambayo ilitoa muongozo mzuri kwamba hata kama mauzaji yatafanyika, basi kuna masharti maalum yafanyike.

Mhe. Spika, labda kwa ruhusa yako niyataje anasema rufaa hii inakubaliwa kwa kiwango Fulani, nyumba iliyowekwa Wakfu huko Migombani pamoja na eneo lake liuzwe na pesa zake zitakazopatikana inunuliwe nyumba nyengine yenye hadhi kama hii na iwekwe Wakfu badala ya hii ya sasa.

jengine *ruling* ya tatu inasema masharti ya Wakfu yawe yale yale ya Wakfu wa mwanzo, lakini *ruling* ya nne inasema fedha zitakazobakia zigawanywe miongoni mwao wanufaika au wale warithi sawa kati ya wanawake na wanaume na *ruling* ya tano inasema kwa maslahi ya watu kwa ajili ya kuleta amani kati ya wanafamilia, kati ya wafaidika na Mahakama hii inaletwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa kusimamiwa na ile mirathi yake.

Mhe. Spika, sasa hii nyumba imeuzwa bila ya ridhaa ya pande hizo za hao warithi, hilo ni kosa la mwanzo, lakini nyumba kabla ya kuuzwa ilitakiwa ifanyiwe tathmini, nyumba haikufanyiwa tathmini na kama nyumba ile ingelifanyiwa tathmini, wale warithi wangelisema kwamba tathmini hiyo tumekubaliana nayo au hatujakubaliana nayo, hicho kitu hakijafanyika, leo matokezeo yake nyumba imeshauzwa, miti yao imeanza kuharibiwa inakatwa, lakini kama Jaji wa Mahakama ya Rufaa alimueleza kwamba hii nyumba itakapouzwa, inunuliwe nyumba nyengine yenye thamani kama ile.

Mhe. Spika, sasa mimi leo naomba kama Mahakama ina nguvu yake, lakini na Baraza lina nguvu yake, mimi naomba Baraza lako Waheshimiwa Wajumbe muniunge mkono mniridhie kwamba kesi ile na maamuzi yale ya Mahakama yasimamishwe ili pande hizi za femilia zikae pamoja na Kamisheni ya watu wa Mali ya Amana wafanyiwe ile tathmini, yale mauzo kama yamefanyika kihalali, kama yamefanyika kihalali, huko mbele tunaweza tukaja tukaruhusu, lakini kwa sasa hivi, kwa jinzi nilivyoiona hiyo kesi, kwa sababu kutokana na muda siwezi nikasoma vielelezo vyote.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi ninavyohisi na kwa elimu niliyofundishwa na mwalimu wangu wa madrasa, kwa kwekli hapa haki haikutendeka na unajua mambo ya mirathi hayo, kuna leo na kesho, sasa huko kesho ndio tunakuogopa zaidi kuliko hapa leo, kwa kuwa hata Mhe. Waziri jina lake Shekhe Abubakar, ni jina kubwa.Kwa hivyo, naomba vile vile katika hizi sheria zetu za Kiislam na hii Mahakama ya kazi ikifanya kazi vizuri hata wale wenzetu kule Tanzania Bara ambayo wanaipigia kelele na wanaitaka Mahakama ya kazi, wataweza kuvutiwa.

Mhe. Spika, lakini wakiona Mahakama yetu ya Kadhi huku inakwenda songombingo kwa kweli hata na wale watasema aa, unasikia na kule Zanzibar wanauza mali za watu kinyume cha sheria za Kiislam, sasa hilo naamini Mhe. Waziri atakaa na timu yake wataweza kuniletea jawabu, kama nitaridhika nitaweza kuzuia fungu, lakini mimi hoja yangu ni kwamba kwanza yale maamuzi yasimamishwe ili haki itendeke, halafu baadae warithi wakisharidhika tena huku mbele tutaweza kuelewana.

Mhe. Spika, nikiondokana na hapo siridhiki na utaratibu wa Mahakama zetu zinavyoingiziwa fedha, tunataka *Separation of power* katika utawala bora, vyombo hivi vya Serikali Mahakama na Baraza la Wawakilishi kila kimoja kinatakiwa kiheshimu mwenzake na katika suala zima la kuheshimiana, basi kupewa nyenzo za kuweza kufanyia kazi.

Mhe. Spika, safari hii mmetuletea ile *PBB, PBB* hili kwa utaratibu huu tunaokwenda nao Mahakamani halitekelezeki kwa sababu ya utaratibu wa uingizaji wa fedha.

Mhe. Spika, kwa hivyo, na ilikuwa naomba ili hili liweze kuanza, nilikuwa naomba kwa mara nyengine kupitia kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ije sheria yetu ya Utawala wa Baraza kama ambavyo katika kipindi kilichopita tulilitolea taafira na serikali tunashukuru imekubali ili tulete sheria yetu ya Utawala wa Baraza na baadae kwa sababu kama sisi hatuna sheria hatuwezi kuleta sheria ya Utawala wa Mahakama. Kwa hivyo, tumalize sheria yetu ya Utawala wa Baraza na baadae kwa kushirikiana na Ofisi ya Mahakama Kuu ya Zanzibar tuandae mswada

mwengine wa sheria wa Utawala wa Mahakama ya Zanzibar, tukiweza kufanya hayo Mahakama zetu zitafanya kazi vizuri tena kwa ufanisi.

Mhe. Spika, ili *performance* ya Mahakama iweze kupatikana, kwanza inategemea uingizwaji wa fedha kwa utaratibu huu, Mahakama zetu kesi zitaendelea ku-*delay*, siku zote tutakuja hapa kazi yetu itakuwa kuwalaumu.

Mhe. Spika, lakini vile vile, tunataka Mhe. Waziri kwa sababu Mahakama ni chombo tofauti na serikali, Mahakama ina mdomo wake, Baraza la Wawakilishi lina mdomo wake na Serikali ina mdomo wake, tunamuomba Mhe. Waziri ajipunguzie majukumu ya kuisemea sana Mahakama, ashauriane na Mahakama ili aweze kutoa ufafanuzi ambao utakaokuwa unatosha, sasa hivi wenzetu hata Tanzania Bara kuna msemaji wa Mahakama, Serikali leo kila siku Waziri akiwa anatoa ufafanuzi wa mambo ya Mahakama itakuwa sasa serikali kama inaingilia maamuzi ya Mahakama.

Mhe. Spika, sasa mimi nilikuwa naomba, basi Mahakama yetu wawe na msemaji wao, sasa sijui katika utaratibu wa sasa hivi ambao hata hiyo sheria Utawala wa Mahakama pengine haipo, lakini hata kama haipo, mimi nadhani wakati umefika Mahakama iwe na msemaji wake ambae ataweza kuzungumzia moja kwa moja kutoka kwa bosi wake Jaji Mkuu.

Mhe. Spika, kwa sababu kuna mambo ambayo Jaji Mkuu anaweza kutofautiana na maamuzi ya serikali sasa, lakini msemaji anakuwa ni Waziri, sasa atasema vipi, hawezi kusema na akisema atatafuna maneno, lakini ikiwa kuna msemaji wa Mahakama, basi yeye ataweza kutoa sauti ya Kimahakama na kisheria, tunataka ile *Separation of power* ipatikane.

Mhe. Spika, lakini vile vile, kwamba majengo ya Mahakama sasa hivi hali kama tunavyoziona, kwa kweli vyumba vya kuendeshea kesi vinakuwa vichache na pengine vinapelekea hata uchereweshaji wa Mahakama, lakini ndio kama hivyo nilivyosema, tukishapitisha sheria yao Mahakama na wao wataweza kuwa na vianzio vyengine vya mapato ili kuweza kuendesha Mahakama yao, lakini kitu cha kushangaza mimi ninavyojua Mahakama Kuu wana kiwanja chao kule Tunguu kuna kiwanja cha Mahakama Kuu Tunguu, lakini kwa utaratibu huu tunaokwenda nao, kile kiwanja kitaendelea kuota mwani na baadae wajanja wachache watakuja kukijenga. Unajua tena siku hizi watu watakuja kukijenga, halafu mambo yaje yawe shaghalabaghala. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri, akija atwambie hichi kiwanja cha Tunguu kitaaza ujenzi lini wa Mahakama Kuu.

Mhe. Spika, lakini vile vile, kulikuwa na kiwanja Mwanakwerekwe ambacho cha Mahakama ya Kadhi, sasa ni zaidi ya miaka 20 kiwanja kipo na kwa utaratibu wa sasa hivi kama nilivyosema kwamba watakuja wajanja wachache ili waweze kukichukua, halafu baadae Mahakama sijui itakuja kumshtaki nani, maana yake Mahakama itakuwa imeibiwa, lakini vile vile, utaratibu wa sasa hivi wa uendeshaji wa kesi, Mahakama haina hata *database*, leo inapokuwa Mahakama haina hata *database*, sasa utegemee takwimu za kesi zitakuwa sahihi siku zote.

Mhe. Spika, sasa mimi nadhani ili twende na wakati, basi *database* ya Mahakama iweze kupatikana na kimsingi kama ninvyosema kwamba sasa hivi tunataka sheria ya Utawala wa Mahakama ili haya mambo waweze kujipangia wao wenyewe kama alivyosema mfano hapa kuna *PBB* ambayo inategemea *programme* mnayoipanga na utekelezaji wake sasa hii Mahakama inataka *database, PBB* itakuwapo wapi hapo.

Mhe. Spika, sasa mimi nadhani masuala haya ni muhimu tuweze kuyachukulia hatua na tukiweza kufunga mashine za kisasa katika Mahakama zote ili suala la usikilizwaji wa kesi, yaani *Court recording system* ambayo itaweza kusaidia kusikilizwa kesi kwa haraka haraka, tuliona Afrika ya Kusini yule mwanariadha pale ambaye alipata matatizo kidogo ya kumshuti mpezi wake. Kwa hivyo, ile kesi ilikuwa inakwenda kisayansi na haraka haraka.

Mhe. Spika, sasa eneo jengine ambalo ningetaka kusema kwamba ningelizuia fungu la Mahakama, kuhusu suala la Mahakama kusaidia wale watu wabadhirifu kuzuia kutumia haki zao zaidi katika kutumia *Court junction*, nilikuwa nikizungumza sana, *Court junction* inachukua zaidi ya mwaka mmoja au miaka miwili huku mtu anaathirika, mtu amekalia mali ya watu, sasa hili Mhe. Waziri nilikuwa naomba sana hebu aje atuelezee hizi *Court junction* zina muda gani kama ile kesi haiendi, kwa sababu *Court junction* zipo, lakini hakuna kesi yoyote ambayo inakwenda.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa nataka nizungumze suala la hatimiliki, kwa kweli wasanii wetu wanajitahidi sana na sisi viongozi tunapokwenda pahala popote kama hawapo wasanii hatujisikii, lakini je, haki zao tunazilinda Wizara ya Habari imeshatoa angalizo na mimi nawapa angalizo tunataka *ZBC, TV* na Redio kwa kweli wanatumia sana nyimbo au kazi za wasanii wetu na kama keshokutwa wanakuja baada ya wiki mbili tatu mwezi wa Ramadhani unakuja, kasida nzuri kila pahala, yaani ile Ramadhani inaingia hasa na ile futari inateremka, lakini nyuzi tupu hamna kitu na hawa watu wa madrasa, sitaki kusema wasanii, wale sio wasanii, wale wanafanya vitu vya kimoyo na kiroho vya kiimani, nao tuwawezeshe, lakini kama mwenzangu anavyonichomekea nao zinauzwa kazi zao. Kwa hivyo, kama zinauzwa kazi zao, basi waweze kupata hizi haki zao.

Mhe. Spika, hawa wasanii kwa nchi za wenzetu ni watu wakubwa wanakuwa kama mabalozi wa nchi, hata hivi juzi tumekwenda katika *function* fulani "Siti Binti Sadi" tukapigiwa nyimbo yake, basi ule ubwabwa tulioalikwa pale wa Makamu wa Pili wa Rais *Wallah* ulikuwa unateleza kwa sababu za nyimbo za Siti Bint Saadi, lakini sijui pale ile familia yake imepata nini sasa, lakini kimsingi mimi nadhani sasa hivi sote tushirikiane kulinda haki za hawa wasanii wetu.

Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria, mimi nilikuwa naomba sana Tume ya Kurekebisha Sheria watusaidie sana hasa sisi Baraza la Wawakilishi, Tume hii ya Kurekebisha Sheria tumeona hapa kuna sheria tokea mwaka elfu moja mia ngapi, wanataka kurekebisha, lakini wasiwe wanaangalia kurekebisha sheria tu, lakini kurekebisha na Katiba, hii Katiba yetu sasa hivi inatubana na Katiba ikikubana sijui unatakiwa kufanya nini, wenzangu hii kama wanaweza kujibu wangejibu hapa hapa. Kwa hivyo, Katiba inatubana kuna vifungu ambavyo havitupi nafasi vya kumnyima bajeti yake Mhe. Waziri mpaka tumuadhibu Makamu wa Pili wa Rais, sasa kifungu hiki hakitupi raha tunafanya kazi ya wananchi, lakini kazi yenyewe inaishia hivi hivi tu, ukishapigwa maneno unaondoka. Sasa tunaomba uangalie na vifungu vya Katiba.

Mhe. Spika, lakini vile vile, hata ule uhuru wa Baraza la Wawakilishi, bado suala zima la uteuzi wa Katibu hautupi raha wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, tunaitaka hii Tume ya Kurekebisha Sheria, sasa Mhe. Waziri akija atwambie hizi kero zetu za Baraza la Wawakilishi watatusaidia vipi, maana yake sisi tulileta mswaada hapo mnausokota, lakini tunaamini hii Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuwa ni yenu wenyewe huko inaweza kutusaidia ikatupa ile nafasi ambayo wananchi wanahitaji tupate nguvu ili kuweza kuwasimamia haki zao vile vile.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuna kesi hizi za madawa ya kulevya, tunaona tabu sana juzi yamekamatwa mapolo hapo uwanja wa ndege, picha uso hauonekani kamera na tunasubiri wizara husika waje watwambie ule uso uko wapi na madawa ya kulevya yamefikia hatua gani? Sasa hili hebu aje atusaidie Mkurugenzi wa Mashtaka, kwa nini hizi kesi za madawa ya kulevya zinakuwa hazina jawabu ya kufikia mwisho?

Mhe. Spika, namalizia malizia.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, muda wako umemaliza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, umemaliza baada ya haya machache, naomba katika *Hansard* iingie vile vile na zile stahiki nilizokuwa nimezidai kwa bajeti ya miaka mitatu kuhusu haki za *ma-assessors, ma-assessors* mpaka leo wanadai na inaweza kupelekea kwamba *ma-assessors* wakagoma kesi zikaendelea kusita. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru muumba wetu *Allah Subhanahu Wataallah* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na tukaendelea shughuli zetu katika chombo hiki muhimu cha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia machache katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria. Tatu, nimpongeze Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake kama ulivyomsifu mwenyewe ametumia muda wa saa moja kamili katika kuwasilisha hotuba yake.

Mhe. Spika, Wizara hii ya Katiba na Sheria kama jina lake linavyojieleza linasimamia moja ya Katiba yetu na pili sheria na mifumo yake yote katika Zanzibar na Katiba yoyote ya nchi na pengine hata zisizokuwa za nchi za

Jumuiya nyengine huwa zina utangulizi na wataalamu wa Katiba, wanavyotwambia unaeleza dhamira ya wenye Katiba. Kwa hivyo, ninavyoamini mimi kwa sababu Katiba hii wenyewe ni Wazanzibari utangulizi uliomo ndani ya Katiba hii unaeleza dhamira ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa katika utangulizi wa Katiba hii kuna kifungu kadhaa kinachoelezea madhumuni ya kuwepo Katiba hii. Cha tatu ambacho naomba nikinukuu kinasema;

"Na kwa kuwa tunazingatia na kuthamini nzuri ya Kimapinduzi iliyofanywa na viongozi wa Mapinduzi wakiongozwa na muasisi wa Chama cha *ASP* na Mapinduzi ya Zanzibar 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ambaye fikra zake zitaendelezwa na kudumishwa daima kizazi baada ya kizazi katika kupambana na ukoloni, ubepari, unyonge, uonevu na dharau na badala yake kudumisha uhuru na umoja, haki na usawa, heshima na utu".

Mhe. Spika, haya ni miongoni mwa malengo ya wenye Katiba hii ya Zanzibar. Sasa hiyo ni dhamira, lakini baadae dhamira hii imefasiriwa katika vifungu mbali mbali vya Katiba hii na Ibara ya kwanza Katiba yetu ya Zanzibar inasema;

"Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyoizunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar".

Mhe. Spika, naomba niyasisitize maneno kwamba eneo lake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vilivyoizunguka na bahari yake. Sasa nimeomba nianze hapa kwa sababu kuna suala zima la mipaka ya Zanzibar hasa kuhusiana na Kisiwa cha Fungu Mbaraka au kama ambapo kimezoea kuitwa kwa Kiengereza *Latham Island*.

Mhe. Spika, Katiba hii tuliyonayo ilitungwa mwaka 1984, lakini kabla yake ilikuwepo Katiba ya mwaka 1979 na kabla hiyo zilikuweko *decrees* kadhaa zilizotungwa kuanzia tarehe 12 Januari, 1964 ambazo ndio zilikuwa zikitoa muongozo wa Kikatiba kwa nchi yetu. Sasa zile zilikuja baada ya nchi yetu kufanya Mapinduzi na Mapinduzi yalikuja yalirithi mfumo fulani wa Kikatiba ambao iliuondosha, lakini imeondosha mfumo wa utawala haikuondosha mipaka na milki ya Zanzibar iliyokuwepo hadi Mapinduzi yanafanyika.

Mhe. Spika, wakati Mapinduzi yanafanyika Katiba ambayo ilifutwa ilitaja nini mipaka ya Zanzibar ambayo sasa imemilikiwa na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1963 katika Ibara ya 136 inasema;

"*The State of Zanzibar means the Island of Zanzibar, Pemba and Latham including the territory water thereof and any Islands within those water".*

Mhe. Spika, sasa eneo hili lilitambuliwa na Katiba ya Zanzibar 1963, Katiba iliondoshwa, lakini kukatungwa *decrees* ambazo zilikuwa zinatumika katika eneo la mipaka ya Zanzibar ambalo ndilo hili lililotajwa katika Katiba hii. Sasa nimeona nianze na hili kwa sababu katika vikao vilivyopita vya Baraza, Wajumbe mbali mbali tuliwahi kuhoji juu ya suala la hatima ya Kisiwa cha Fungu Mbaraka ambacho ni sehemu ya miliki ya Zanzibar na wakati fulani Mhe. Mwanasheria Mkuu alitueleza kwamba kulikuwa na madai kutoka kwa ndugu zetu wa damu upande wa Tanganyika, wakisema kwamba Kisiwa kile ni chao, lakini tangu wakati ule hatujapata taarifa zozote tena na mara ya mwisho tulipopewa taarifa katika Baraza hili Mhe. Mwanasheria Mkuu alitwambia kwamba walikuwa wanalizungumza hili.

Mhe. Spika, nikastaajabu kwamba tunazungumzaje kuhusu haki yetu, halali ambayo sheria zote zimethibitisha hivyo na kama Mhe. Mwanasheria Mkuu alivyotuthibitishia ndani ya Baraza hii kwamba ushahiri wa kihistoria wa nyaraka nzito unathibitisha kwamba hii ni mali ya Zanzibar. Sasa nimeona niliulize tena leo kwa sababu nilipata wasiwasi wakati fulani tulipokuwepo Dodoma katika Bunge la Katiba nilibahatika katika Kamati moja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Tanzania Bara na akalitaja suala hili. Sasa nimesema hebu Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa sababu tunajadili Wizara hii atusaidie tumefikia wapi juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni wajibu wetu kusimamia haki zetu, ni wajibu wa kila Mzanzibari si kiongozi tu, Ibara ya 23(4) ya Katiba ya Zanzibar inasema;

"Kila Mzanzibari ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi, kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Zanzibar".

Mhe. Spika, nataka niyasisitize maneno mamlaka na ardhi, hata kikiwa ni kichuguu cha mchanga, kama ni miliki ya Zanzibar ni haki yetu kukilinda ni wajibu kulinda. Sasa nilikuwa nataka Mhe. Mwanasheria Mkuu akija aje atusaidie katika hili kwamba tumefikia wapi na nini msimamo wa serikali mpaka sasa na hili ni muhimu kwa sababu kuna suala vile vile la kulinda mali ya Zanzibar na ukiangalia mgao wa zile *blocks* za mafuta ambalo ni suala mpaka leo tunabishania hapa.

Mhe. Spika, tumezoea kuwaambiwa kwamba *blocks* za mafuta za Zanzibar kwa upande wa bahari ni *blocks Number* 9, 10, 11 na 12, lakini hiyo ukiichukua hii mipaka waliotaka ndugu zetu wa damu, tuamini kwamba ndio mipaka yetu, lakini ukenda mpaka Fungu Mbaraka (*Latham Island),* maana yake *blocks number* 7 na *number* 8 ni sehemu ya mamlaka ya Zanzibar, lakini yashagawiwa na sasa hivi utafutaji unaendelea huko kilichositishwa ni kuanzia *block number* 9, 10, 11 na 12. Sasa nilitaka Mhe. Mwanasheria Mkuu aje atusaidie kwamba hili wakati vibali vimetolewa wanaendelea, sisi tunasema tunaendelea kuzungumza na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu upande wa Tanzania Bara, nini itakuwa baadae maslahi na hatma ya haki ya Wazanzibari katika suala hili. Hilo moja.

Mhe. Spika, la pili, nikilisisitiza kule kule kwenye utangulizi wa Katiba ya Zanzibar tuliposema kwamba lengo ni kuendeleza fikra za Mzee Karume na waasisi wenzake katika kudumisha kizazi baada ya kizazi kupambana na ukoloni, ubepari, unyonge, uonevu na dharau na badala yake kudumisha uhuru na umoja, haki na usawa, heshima na utu.

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari 1964, nchi yetu palifanyika Mapinduzi yaliyoiweka madarakani Jamhuri, kwa maana serikali inayoendeshwa na wananchi wenyewe wa Zanzibar na kwamba viongozi wake wanachaguliwa na watu, tarehe 25 Januari, 1964 kupitia gazeti kuu la serikali *The Zanzibar Gazette*, nakala yake ninayo hapa ilitangazwa Serikali ya Kwanza ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na katika hiyo palitangazwa kwanza Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, Wajumbe wake wakiwa ni watu wafuatao. Naomba niwanukuu:

1. *President* Abeid Karume
2. *Vice President* Abdalla Kassim Hanga
3. *Honourable* Abdulrahman Mohammed Babu
4. *Honourable* Hasnu Makame
5. *Honourable* Aboud Jumbe
6. *Honourable* Saleh Saadalla
7. *Honorable* Idrissa Abdulwakil
8. *Honourable* Othman Shariff
9. *Honourable* Abdulazizi Twala
10. *Honourable* Hassan Nassor Moyo
11. *The Commission of Police* Mr. Edington Kissassi
12. *Field* Mashal John Okelo
13. *Honourable* Yussuf Himid
14. Honourable Seif Bakari
15. *Honourable* Ramadhan Haji
16. *Honourable* Abdalla Said Natepe
17. *Honourable* Pili Khamis
18. *Honourable* Khamis Hamed
19. *Honourable* Hamid Ameir Ali
20. *Honourable* Said Iddi Bavuai
21. *Honourable* Said Washoto
22. *Honourable* Mohammed Abdalla
23. *Honourable* Abdalla Mfarinyaki
24. *Honourable* Hafidh Suleiman

25. *Honourable* Khamis Darweish
26. *Honourable* Khamis Abdalla Ameir
27. *Honourable* Mohammed Mfaume Omar
28. *Honourable* Muhsin Bin Ali
29. *Honourable* Mohammed Juma
30. *Honourable* Daud Mahmoud

Mhe. Spika, hawa ni Wajumbe 30 wa awali wa Baraza la Mapinduzi na tangazo hili limetolewa na limetiwa saini tarehe 24 Januari na mtu anayeitwa Salim Said Rashid *Secretary to the Cabinet of Ministers and Revolutionary Council.*

Mhe. Spika, madhumuni yangu nini kunukuu hivi kwamba hawa waliasisi Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na ili kuhalalisha Mapinduzi wakapitisha sheria waliyoita *Legislative powers law* ya mwaka 1964. Imepitishwa na ikaandikwa ndani ya Gazeti Rasmi la Serikali tarehe 6 Februari, 1964 na kwa uzito wake waka-*sign* hawa niliowataja wote tofauti na sheria nyengine hii wame-*sign* wote kwamba wanalianzisha Baraza la Mapinduzi kama ni chombo halali cha kusimamia sheria za nchi hii. Katika sheria hii kifungu cha 2 kinasema;

"The power to make law for the Government of the People Republic of Zanzibar is hereby vested and the present of the Republic acting by and advice and consent of the revolution country".

Mhe. Spika, yaani madaraka ya kutunga sheria kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar yanawekwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri akifanya kazi kwa ushauri na ridhaa au idhini ya Baraza la Mapinduzi na kifungu hiki baadae kikawekwa vizuri zaidi katika *decree* Nam. 5, hii ndio sheria pekee iliyoitwa *Law* ni *Legislative powers law*, kwa sababu inahalalisha Mapinduzi zilizofuata zote zikaitwa *decrees*. *Decree No*. 5 ya 1964 ikasema hivi kifungu cha 2;

"The people Republic of Zanzibar is a Democratic State delicated to the rule of law. The President as a Head of State validates Legislation by his assent as interim measure Legislative Power recite in the Revolution Council and is exercise on its behalf in accordance to the law by the President".

Mhe. Spika, kwa ufupi ni kwamba Mhe. Rais ndie mkuu wa nchi na ndie atakayehalalisha sheria kwa kutoa idhini yake kwa maana *assent* na kama utaratibu wa muda madaraka ya kutunga sheria yapo mikononi mwa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, sasa kwa nini nimezinukuu sheria hizi, tarehe 26 April, 1964 tunaambiwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar iliunganishwa na Jamhuri ya Tanganyika, lakini nchi yetu inafuata mfumo wa sheria za Kiengereza na ndio maana nchi zote mbili zimeungana ziliweka sharti kwamba ili mfumo ule uloingizwa Zanzibar ambayo imekabili sheria chini ya mamlaka yake, basi lazima kufanyike tendo la kutungwa sheria ya Zanzibar, *decree* ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ninajua imebakia dakika tano tu nimalizie hilo, wala sikusudii kuchangia jambo jengine kwa leo.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninazimalizia Ibara ya 8, inasema ya Mkataba ya Muungano, Mkataba huu utahitaji kuthibitishwa kwa kutungiwa sheria na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapiduzi la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kwa kushirikiana na Baraza lake la Mawaziri na Mkataba kupitishwa na kuundwa na Serikali ya Muungano ya Zanzibar na Tanganyika kwa kufuata masharti yaliyokubaliwa.

Mhe. Spika, sasa hoja yangu kwa miaka mingi tumehoji, naomba Mhe. Waziri akija hapa atwambie iko wapi *decree* ya Baraza la Mapinduzi iliyoridhia Muungano kwa upande wa Zanzibar. Hili ni muhimu sana kwa Zanzibar na tumejitahidi mno kupekuwa sheria za Zanzibar magazeti yote ya Serikali sheria hii hatuioni. Tunachokiona ni kitu kinachoitwa *Legal notice* kilichapishwa katika Gazeti Rasmi la Tanganyika tarehe 1/5/1964, sheria ambayo inaambiwa eti ndio sheria ya Baraza la Mapinduzi kuridhia Zanzibar kusalimu mamlaka yake makubwa katika mfumo wa Muungano.

Mhe. Spika, lakini hii inayoambiwa sheria ya Zanzibar imesainiwa na mtu anayeitwa P.R.Lenius Kaimu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanganyika wakati sheria nilizozisoma hapa zinasema kwamba wa kuidhinisha mfumo wa utungwaji sheria itatunga Baraza la Mapinduzi na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, utaratibu wake, *decree* zote ukizitizama zina *assent* ya Mzee Karume kwa miaka ya mwanzo na chini Katibu wa Baraza la Mapinduzi. Naomba Mhe. Waziri akija aje atwambie iko wapi *decree* ya Baraza la Mapinduzi yenye *assent* ya Mzee Karume na chini iliyosainiwa na aliyekuwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi Salim Said Rashid kuridhia Baraza la Mapinduzi kuhalalisha kitendo cha Zanzibar kusalimisha mamlaka yake katika Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, hili ni muhimu sana katika kipindi hiki, yapo tuliyohoji kule kunakohusik,a hili linatuhusu sisi kwa sababu hizi ni sheria za Zanzibar. Ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ikiwa Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza kumsaidia aje atwambie Wazanzibari wanahitaji kujua sheria hii iliyopokonya mamlaka ya msingi ya Zanzibar kwa kupitia mfumo wa Muungano iko wapi? Naomba atutolee nakala yenye *sign* ya Mzee Karume, yenye *sign* ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi ili tujiridhishe na wananchi wa Zanzibar waridhike.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nasema sitoridhika kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kama hakuniletea Nakala ya sheria hii Baraza la Mapinduzi yenye *signs* ya Mzee Karume na Salim Said Rashid Katibu wa Baraza la Mapinduzi, kuhalalisha kitendo hicho cha mwaka 1964.

Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi ya kuweza kuwepo katika Baraza hili tukufu ukiwa wewe ndio muongozaji wetu. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwenyekiti wake kwa kutupa fursa nzuri ya bajeti hii ambayo aliyoisoma muda mfupi, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii vile vile kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na taasisi zake zote zilizokuwa chini yake kwa kazi ngumu ya vitendea kazi, kwa kazi ambazo wanazotumia hekima na busara na kuweza kufanikisha masuala kama haya. Kutokana na bajeti ya serikali hahe hahe, serikali ingelipenda kuona mambo mengi yanaweza kufanyika, lakini kutokana bajeti mapungufu ya fedha, uchumi wetu uliokuwa mdogo wakati mwengine serikali inaongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein wangelipenda sote na sisi kuona sehemu zote hizi muhimu zingeliweza kupata nafasi nzuri ya kutekeleza kazi zake. Kwa hivyo, mimi nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe.Waziri kwa kazi yake.

Mhe. Spika, ninamuomba kwa heshima zote Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria kwamba nina masuala yangu matano ningelimuomba kwa uwezo wake na wasaidizi wake kwa imani niliyokuwa nayo haya masuala hayatakuwa yanatafunwa tafunwa maneno, lakini tutapata maneno ambayo yatakuwa ya moja kwa moja kwa faida ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ninalo gazeti hapa la Uhuru, gazeti la Chama cha Mapinduzi la tarehe 6 Mei ilikuwa siku ya Jumanne mwaka 2014.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka ufafanuzi kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Shekhe Mkuu wa Dar-es-salaam Al-Haji Mussa ambaye tunamuheshimu sote, mimi ninamuheshimu anaposema anatoa msimamo wa Zanzibar, hili hapa gazeti la uhuru anatoa msimamo wa Zanzibar. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri, Shekhe huyu sasa haya mambo yamo ndani ya Muungano na *in fact*, amemzungumza Mhe. Lukuvi kwa maneno yake ambayo Zanzibar hatujapatapo kutamka sisi, anasema kwamba Zanzibar wanataka kujitenga na dola ya Kiislamu, hili halipo kwa Zanzibar. Sasa na Shekhe akakubali kumfata.

Mhe. Spika, kwanza Mhe. Lukuvi mipaka yake mwisho Chumbe hana mipaka Zanzibar kuzungumza kama Lukuvi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu. La pili, je, Mhe. Waziri anataka kutwambia kwamba *Fatwa* zinazotolewa sasa kwa Mashekhe wa Dar-es-Salaam Zanzibar ndiyo tunaikubali. Je, Zanzibar haina Mufti au haina Ofisi ya Kadhi

Mkuu ambaye yuko ndani ya Katiba? Je, Shekhe Mkuu uwezo wake wa kusema na Mufti wetu na Kadhi Mkuu wetu, nani mwenye nguvu zaidi.

Mhe. Spika, nilisema miaka 20 iliyopita, nataka ninukuu nilisema cheti cha ndoa tutachukua Dodoma. Sasa hivi vitu tusipoangalia, hili suala linaweza kuleta vitu ambavyo havisaidii. Sasa nilitaka Mhe. Waziri, atakapokuja aje atueleze kadhia hiyo, ana uwezo wa kufanya hivyo.

Mhe. Spika, lakini katika hili hili kwa bahati Mzee wetu Mhe. Samuel Sitta alipata nafasi ya kukutana na Shekhe Mkuu wa Dar-es-salaam (BAKWATA) na kiongozi wa dini wa Kikiristo Kanal Pengo, hili hapa kwenye gazeti la Uhuru, picha zake zipo, gazeti la Zanzibar Leo la serikali lipo, gazeti la *Daily News* ziko hizo picha, naona magazeti yote ya serikali ya CCM zote mbili hizi zinazoongoza pamoja na magazeti haya kwamba alikwenda kuwatembelea ili kupata maoni ya hili Bunge la Katiba.

Mhe. Spika, sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, je, hapa palitosha Zanzibar, hatukuwa na haki kama kiongozi kuja kuwatembelea Mashekhe wetu na wakaonana na Shekhe gani Zanzibar? Na kama kuna jambo, basi waziri atwambie hili suala kwamba limefikia pale kwa huku Zanzibar, sasa ndiyo hakuna tena. Kwa hivyo, mimi nafikiri kama katembea huku na sisi Zanzibar tulikuwa na haki yakutembelewa na kutoa maoni yetu kupitia Kadhi Mkuu na Shekhe Mkuu.

Mhe. Spika, magazeti haya nataka niyazungumze ilikuwa siku ya Jumatano, April 9, sasa kafika Zanzibar alimuona Shekhe gani na Padri gani ili tupate tu maelezo yakuweza kutusaidia sisi Wawakilishi na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, la tatu, hili suala la Fungu Mbaraka. Fungu Mbaraka limekuja na limekuwa wazi wakati tunapochangia Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais mwaka jana na wakati nilipochangia Ofisi ya Waziri wa Maji, Nishati na Ardhi kwa bahati nzuri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Mohammed Aboud alimpa nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu kutopa ufafanuzi. Lilipokuja nilipolileta kwenye Wizara ya Maji na Ardhi waziri anayehusika akamsimamisha tena Mhe. Mwanasheria Mkuu kututolea ufananuzi.

Mhe. Spika, ndani ya Baraza hili *Hansard* zipo Mhe. Mwanasheria Mkuu napenda kumnukuu alisema hivi;

> "Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, amesema kwamba kisiwa cha Fungu Mbaraka kiko ndani ya ardhi ya Zanzibar itabakia ndani ya ardhi ya Zanzibar na serikali iko tayari kwenda kokote hili kulisimamia".

Mhe. Spika, baada ya maelekezo kama hayo kumetoka barua Ofisi ya Waziri Mkuu *paragraph* mbili imeandikwa inasema; kisiwa cha Fungu Mbaraka ni kisiwa cha Bara, siyo cha Zanzibar. Huu ndiyo ukweli, sasa tunataka tuambiwe tumekuja humu sote kuwawakilisha wananchi, serikali imetoa ufafanuzi, lakini juu ya fafanuzi zote mbili Ofisi ya Waziri Mkuu inaleta barua kusema kisiwa cha Fungu Mbaraka ni kisiwa cha Tanzania Bara.

Mhe. Spika, sisi ndiyo wananchi na tumesimama hata Mhe. Waziri wa Katiba aliposimama na kitabu hiki inatekelezwa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa maana yake tumekuja hapa kwa maslahi ya wananchi kabisa. Kwa hivyo, mimi ningelipenda kwamba serikali mara mbili imeshatoa kauli twende na tuko tayari kwenda popote na Katiba inatueleza, halafu baada ya majibu haya ndani ya Baraza hili la sheria Ofisi ya Waziri Mkuu inaleta barua *paragraph* mbili inampelekea Waziri wa Maji na wahusika wengine kusema kwamba kisiwa hiki ni chetu.

Mhe. Spika, sasa hofu ninachoomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tumefika wakati nafikiri *we go on trust*, lakini lazima imefika wakati hivi visiwa vyetu sasa vipate utaratibu mzuri wa kuingiza mipaka yetu.

Mhe. Spika, jana Mhe. Rais wa Malawi anasema atatoa usimamizi mkali kuhusu Ziwa Nyasa ambalo liko ndani ya ardhi ya Tanzania, gazeti la jana hilo la Jumanne tarehe 3. Hofu yangu tunaweza pale kisiwa cha Chumbe ikawa inaonekana lulu kesho tukaambiwa siyo chetu kile. Sasa ninachoomba hivi vitu dalili ya mvua ni mawingi, sasa kama dalili ya mvua ni mawingu, ni uzuri sisi ndiyo tupo *generation* ambayo watoto wetu na wajukuu zetu ndiyo watakaokuja kuwaona wale. Kwa hivyo, kama tuko sisi angalau kuwe na *record* Zanzibar mipaka yetu yote ifanywe na iwekwe kwani Chumbe kiko katikati pale. Kwa hivyo, ikitoka lulu unaambiwa ile siyo yetu.

Mhe. Spika, Sasa mimi ningeliomba Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anisaidie suala hili na atatwambie najua Mhe. Waziri nilikuomba sana nakuheshimu sana. Kwa kweli naomba Mhe. Waziri vitu hivi vije wazi ili tusaidie na tuwasaidie wenzetu.

Mhe. Spika, vile vile, nilikuwa naipitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ukurasa wa 177, 177 na 178, ukurasa wa 176 mfuko wa pamoja wa mapato yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mfuko wa fedha. Ukurasa wa 176,177 na 178 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 hii imo ndani ya Katiba. Nataka Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa kweli haya ndiyo mambo ambayo yamo ndani ya Katiba, mimi nina hakika kwamba uchangiaji wa pamoja wa Muungano wetu na mfuko wa pamoja.

Mhe. Spika, halafu kuhusu fedha ya pamoja ya Jamhuri ya Muungono na kumalizikia, kwa kweli ni jambo la kusikitisha ambacho hiki kitu kimo ndani ya Katiba kwa zaidi ya miaka 20 mpaka leo Tume ya Pamoja imekaa, imefanya kazi yake, imo ndani ya Katiba masuala ya Muungano ya pamoja kuhusu misaada, ndiyo hayo matatizo, wakati mwengine wenzetu au kunakuwepo na manung'uniko huku na huku kama kila mtu anaona mzigo au mmoja anakaa anasema bwana nyinyi tunakusaidieni tu mmekaa kama yatima.

Mhe. Spika, sasa kama vitu hivi vimo ndani ya Katiba na kuweza kutekelezwa, kwa kweli inatutonesha sana sisi kama viongozi kwamba vitu vimo ndani ya Katiba na leo haviwezi kutekelezwa. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aje anisaidie hii Tume ya Pamoja imo ndani ya Katiba kuhusu mchango wa fedha wa pamoja na makusanyo, ni mara ngapi Mhe. Rais wa Zanzibar ameweza kuwaona, hii Tume ya Pamoja baada ya kuundwa, mara ngapi Mhe. Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweza kuona.

Mhe. Spika ninachotaka kukwambia na Mhe. Abubakar namuheshimu sana pamoja na wasaidizi wake. Mimi nasema hivi kwamba Tume imeundwa na mamilioni ya pesa ya kina Shelukindo yametumika pesa za walipa kodi kwa maslahi ya wananchi. Tume hii imeshamaliza muda wake na Mhe. Rais Mkapa ameikuta Tume hii na Mhe. Rais anakwenda nayo Tume hii.

Mhe. Spika, nataka nikwambie na Mhe. Waziri nataka nimsaidie katika jawabu ili nimrahisishie kwamba ni Mhe. Rais wa Zanzibar tu aliyeweza kukutana na Tume hii, Mhe. Rais wa Jamhuri hakuwa na hata na muda wa kukutana na Tume hii ambayo imepewa kazi na Marais wawili wa nchi hii. Sasa hivi vitu vingelikuwa Tume hii tungelijua Zanzibar tunadaiwa ngapi na huku tunadaiwa ngapi, halafu tunafanya hesabu, si tuna udugu, tuna mshikamano, tuna Muungano wetu wa imara na Muungano wetu wa kihistoria. Tunataka Muungano wetu wa kihistoria na kuheshimiana, mimi nafikiri ingelikuwa mambo haya yangeliwekwa na yangelifanyika Tume imeshakaza pande zote mbili, Marais wawili wameshaunda Kamati hizo za Tume na Tume mpaka leo hii haina jawabu imo ndani ya Katiba.

Mhe. Spika, sasa kuna vitu vyengine hivi au unaweza kuwa wasaidizi wake hawakuweza kumpa nafasi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, mimi ningelimuomba Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano namuheshimu sana kwa sababu ni bosi wangu, ni Mwenyekiti wangu wa CCM kiti hiki ni cha CCM siyo cha Mhe. Raza, nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi wa Uzini, nimekuja kwa kiti cha Chama cha Mapinduzi, basi tumuombe Mhe. Rais wa Jamhuri kabla hajateremka kilima akakutana na Tume hii ya Pamoja na ripoti hii ikatizamwa kuna nini halafu tungeliweza kupata ufafanuzi wa mambo mengi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri wa Katiba katika vitu hivi aje kwa ufasaha na kwa hekima, busara, usikivu atwambie na ili tuweze kulisaidia hili Baraza lako, tumekuja hapa kulisaidia Baraza humu ndani. Nataka hii *backbencher* unayoiona haina upinzani ni kwamba tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa huku hatuna tunazungumza kwa maslahi ya wananchi hakuna *backbencher* yenye upinzani bajeti zote tutazipitisha tunaita Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hiyo, hapa sote *backbencher* tuliobakia ni wale ambao tunasaidia nchi.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: *Wallahi,* baba yangu.

Mhe. Spika, katika kuchukua nafasi hii vile vile nimalizie mawili tu hili suala alilolizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, mimi namuunga mkono sana, namuheshimu sana mwenzangu, lakini nafikiri suala la Mahakama na Baraza zote zina uhuru. Sasa vitu kama hivi kama havijapatiwa ufumbuzi kwenye Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama ya Mkoa, kuna *Court of Appeal* (Mahakama ya Rufaa ya Tanzania).

Mhe. Spika, sasa ni vizuri nafikiri ukienda kwenye utaratibu ambao tusingelionekana tuko ndani tukachanganya mambo ambapo Mahakama zina taratibu zake, hujaridhika hapa kuna Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Kwa hivyo, vitu hivi tuwe na uangalifu mkubwa ili vyombo hivi viwe na uhuru na kuona kwamba vinaleta changamoto. Tumeona kilio vitu hivi vitaendelea, lakini mimi nafikiri taratibu tu za kuepuka kuingia uhuru wa jambo ambalo litaweza kuona kwamba vitu… Lakini kuna Mahakama ya Rufaa na baada ya Mahakama ya Rufaa, basi muamuzi wa mwisho ni Mhe. Rais vile vile. Sasa mimi nafikiri hizi taratibu kama kuna vitu mtu hajaridhika navyo au sehemu yoyote ziko Mahakama ya Rufaa na ziko taratibu zake katika hili.

Mhe. Spika, vile vile, la mwisho kwa heshima na taadhima hili suala la unyanyasaji ninamshukuru dada yangu Mhe. Mgeni alipeleka hoja binafsi mwaka jana anasema "mkaa na maiti haachi kulia kulia". Alipoleta hoja hii, kwa kweli hii hoja ina uchungu sana, siku nyengine vitendea kazi, lakini kuna vitu viko wazi.

Mhe. Spika, mwaka jana kuna mmoja katika Mkoa wangu wa Kusini alifanyiwa vitendo ambavyo si vya utamaduni wa Zanzibar, kwa bahati nzuri aliyefanya vile ni moja katika taasisi wanaotulinda sisi nchi. Basi ile familia ikapata *communication*, nao mimi nikawaambia basi nendeni kwa Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba mtapata taratibu. Walipokwenda kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria Mwenyezi Mungu ampe umri mkubwa Mhe. Abubakar mzee wangu ninayemuamkia shikamoo kwamba alipokwenda akapata taarifa ile yeye kama waziri aliyemteua ni Dkt. Ali Mohammed Shein (Mhe. Rais wa Zanzibar) kama ni Mhe. waziri alimuandikia Kamanda barua wa Mkoa wa Kusini. Eeh, bwana njoo kuna suala la kulizungumza la pamoja, yeye tena si waziri wa CUF, ni waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kamishna aliyepita nataka nieleze wazi Kamishna aliyepita yule Mussa kamuandikia barua anamwambia bwana wewe huna uwezo wa kumwita huyu Kamanda wangu, maana yake pale ameshachanganya siasa.

Mhe. Spika, sasa mimi nafikiri hii elimu lazima tuwe nayo ya kutua kwamba hawa viongozi wakati wanapofanya kazi yao mawaziri kwa sababu hapa tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, sasa ni jambo la kusikitisha sana kwamba ile haki inaendelea kunyimwa aliyefanya ni sehemu yake, lakini yule Kamishna vitu ambavyo aliandika barua Mhe. Abubakar, naamini kama Muislamu mwenzangu atakiri kwamba kweli alipokea barua na kupewa hiyo, lakini ninavyojua yeye kwa sababu yeye ni Waziri wa Sheria na Katiba, sasa kuna vitu vingi, hivi vinavyofanywa na watu maskini wengine hawana sauti, wengine ambao hawafiki pahala ambapo panapohitajika.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi nilitaka kutolewa utaratibu zaidi hili suala la elimu na suala la pamoja na kwa kweli tuwafanyie vitu ambavyo tulizungumza *machine* mwaka jana juu ya utaratibu huu mzima na Mhe. Salmin Awadh, tulikubali hapa kwamba hii *machine* ni muhimu kwa nchi na wenzetu wanaumia sana kutokana na umasikini kwa sababu unamwambia mtu ukapate ushahidi aende Bara akalipe shilingi laki mbili au laki tatu...

Mhe. Spika: Mheshimiwa, muda umemalizika.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi kuweza kueleza machache, kwa sababu mambo haya ya sheria, mimi siyajui sana huwa nasema mambo madogo madogo tu kwenye sheria. Sasa naomba nichukue fursa hii kuzungumza mambo machache sana.

Mhe Spika, nianze na ukurasa wa 38, Ibara ya 113, inayozungumzia habari ya Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana. Kwa idhini yako naomba uniruhusu ninukuu hii Ibara ya 113.

Kifungu cha 113 kinasema kwamba;

"Jukumu la Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana ni kusimamia Mali za *Wakfu*, Mali za Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi ya Kitaifa, Hijja, Zakka, Sadaka na Misaada ya kheri".

Mhe. Naibu Spika, zaidi nataka nizungumze hii habari ya Mirathi ya Waislamu. Kama kuna taasisi inayotakiwa iwe makini na muhimu sana katika kufanya kazi zake, basi ni hii Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana. Hawa ni kama minzani wanatakiwa watende haki katika Jamii ya Kiislamu katika kufanya hii mirathi. Hawa hawatakiwi waegemee upande mmoja, wala kuwa na upendeleo kwa upande wowote, hawa wanatakiwa siku zote katika kufanya kazi zao wawe katikati.

Mhe. Spika, kama kuna chombo kilichokuwa hakiko makini sana, basi katika kufanya shughuli zake ni hii Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana kule kisiwani Pemba ambako mimi natoka. Ofisi hii inasikitisha sana, Ofisi hii inashughulikia sana mambo ya Mirathi ya Waislamu, lakini haiko makini. Ofisi ya Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana ya Pemba haiko makini hata kidogo katika kufanya shughuli zake. Naomba sana Mhe. Waziri katika hili atupe jicho sana katika Ofisi ile ili iweze kutenda haki kwa Waislamu wote.

Mhe. Spika, mimi sijafanya tafiti sana, lakini kuna Dawaa baina ya familia ya bwana mmoja alikuwa yeye ni Katibu wa *Afro*-Shirazi pale Tawi la Vitongoji alikuwa anaitwa Khamis Saateni. Huyu bwana alifariki na ameacha familia mbili. Sasa katika kurithisha hapa hii familia yake na mali zake zikazuka Dawaa ya nyumba na Mahakama ya Kadhi ikashindwa kutoa hukumu katika hii nyumba ikabidi suala hili lazima liende katika Mahakama ya Ardhi. Mahakama ya Ardhi walisema lazima wapate kibali cha uwakala kutoka Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana.

Mhe. Spika, inasikitisha sana Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana Pemba hadi leo hii hawajatoa kibali cha uwakala ili ikaenda kesi katika Mahakama ile kwa familia ya Mzee Khamis Saateni katika tumbo la Bi Mauwa Khamisi Saateni, upande mwengine wamewapa tumbo moja, lakini hili tumbo la Bi Mauwa Khamis Saateni hadi leo hii hawajawapa. *This is business*, nyinyi mnajua dini na mnasimamia dini.

Mhe. Spika, Mhe Waziri, tunaambiwa katika Uislamu kwamba, *"Waaqim-lwazna bilqistwi, walaa tukhirul-miizan*". Katika hili lazima wawe makini sana wasihitilafu minzani, hizi familia ni mbili lazima waziweke sawa na wao ndio watu wa dini, inakuwaje kwa upande mmoja wa familia ya Mzee Khamis Saateni wawape uwakala, lakini tumbo la Bi Mauwa Khamis Saateni wasipewe uwakala ili kesi ikaenda pale Mahakamani. Hili ni tatizo, naomba sana Mhe. Waziri katika hili alifuatilie kwa karibu sana kwa sababu yeye ndiye *mas-uul* katika uso wa ulimwengu na yeye ndiye atakuwa *mas-uul* mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu mfalme ni naibu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu huu kwa mujibu wa Shaaban bin Robbert mwana falsafa wa siku nyingi, mfalme ni naibu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, uadilifu wake unaangaliwa na unapimwa.

Mhe. Spika, sasa ikiwa huko makini wewe ni mwakilishi wa mfalme wa nchi, waziri ni mwakilishi wa Mhe. Rais, hapa katika nchi yetu hatuna mfalme tuna Mhe. Rais. Kwa hiyo, wewe ndiye mwakilishi wake unayemuwakilisha Mhe. Rais, unafanyakazi kwa niaba ya mfalme tuliyenaye hapa ambaye ni Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, unatakiwa uwe makini sana kwa sababu wewe ni naibu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, ili uweze kupata kheri hapa dunini na huko akhera tunakokwenda. Hilo niliache hapo kwanza.

Mhe. Spika, baada ya jamaa wa Waasisi wa *Afro*-Shirazi Bwana Khamis Saateni wa Vitongoji, naomba sasa niende katika Mahakama. Mahakama ni moja katika mihimili mitatu ya dola ukiachilia *executive* na *judiciary* ambao ndio sisi. Mihimili hii ni sawa katika kufanya kazi inatakiwa iwe sawa, inasikitisha sana kwamba sisi tunafuata utawala bora, kwa sababu tunayo Mahakama, tuna Bunge ndio humu tulimo sisi, tuna na serikali, *executive*. Sasa inasikitisha kwamba mpaka sasa hivi kinachoonekana katika nchi hii ni *political supreme*, ni hawa *executive* tu. Mahakama yetu kuu inasikitisha, hatutaki tuseme kwamba wawe sawa sawa na *executive* aa, lakini tofauti iliyopo ni kubwa mno.

Mhe. Spika, hebu tumuangalie Jaji Mkuu wetu katolewa mfano hapa, Hatutaki tuseme kama awe na *KG Motor* kama ile ya Rais *special motor* kama *president* lahasha, lakini unamkuta Jaji Mkuu unapita na gari hapa taa zimesimama na yeye inabidi asimame mpaka *traffic queue* ipite na Jaji wetu mkuu yuko barabarani tu kakaa kama nilivyokaa mimi na kigari changu aibu, hatutaki iwe ni *motor cable* kama ya Mhe. Rais, lakini Jaji Mkuu aibu kuona kwamba yuko katika *traffic queue* kakwama. Mhe. Spika wa Bunge kama hili kubwa la Zanzibar, yaani Baraza la Wawakilishi na yeye kumuona kakwama anasubiri *queue* ipite hili ni tatizo.

Mhe. Spika, nasema kwamba Jaji wetu Mkuu huu muhimili wa Mahakama uheshimiwe. Kama haitoshi Mhe. Jaji Mkuu pale tukienda kusali sala ya Alfajiri anakuja peke yake kidogo kidogo, yaani kama mtu wa kawaida tu,

uswahilini hapa jamani Jaji Mkuu unamuweka uswahili pale mnasali naye sala ya Alfajiri, anakuja na kanzu yake hivi. Mimi sikumoja nilitaka kumpiga kikumbo kumbe ni Jaji. Mwadhini alikuwa keshaadhini nakimbilia msikitini kumbe yule aliyeko mbele yangu ni Jaji nataka kumpiga kikumbo, tunakwenda msikitini pamoja Jaji hana hata uangalizi, inasikitisha. *Legislator* wana kila kitu wao, lakini hawa Mahakama na huu muhimili wetu hatujaufika huu, lakini nasema hili la Mahakama ndio hoja iliyoko mbele yetu sasa hivi, Mahakama kwa kweli inadhalilika sana,

Mhe. Spika, naomba ikiwa lazima kuwe na msafara japo wa gari tatu za Jaji Mkuu aonekane hasa kama yeye Jaji anapita hapa saa hizi, kuwe na msafara wa Jaji Mkuu, kwa nini tushindwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi juzi juzi nilikuweko Nigeria, basi nilikuwa nasikia ving'ora tu, naambiwa ni Meya anapita, Meya tu anapita kwa misafara. Kiasi kidogo nikapita mji mwengine, msafara mwengine ule pale, kwa nini serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar juzi tumesherehekea miaka 50 ya uhuru huu, Spika wa Baraza la Wawakilishi asiwe na msafara maalum, aibu! Mimi naomba sana serikali iangalie, kwa sababu Katiba zetu pale mwanzo mimi nakumbuka siku zile niko katika Bunge la Jamhuri, wangu wa Bunge alikuwa Mzee Msekwa, Mhe. Rais, alipata safari ya nje alipopata safari ile na Makamu wa Rais wa siku zile akapata safari ya nje vile vile, basi kwa muda wa siku tatu, Mzee Msekwa alikuwa akija na misafara pale wakati mwengine, kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa akihoji *dilute,* alikuwa kaimu Rais.

Mhe. Spika, sasa mambo kama haya mnaiondosha tu, lakini mimi naamini ikiwa hayupo Mhe. Rais anachukua nchi, ikiwa hayupo Jaji Mkuu anachukua nchi, leo tunamuona wetu anakwenda harusini kwa miguu tena na mitaani huko yuko na shoga yake na nini, jamani lazima tuone kwamba hawa ni watu wakubwa, leo wana kazu fupi zile kavaa mwenyewe anakwenda harusini.

Mhe. Spika, nataka anieleze Mhe. Waziri atakapokuja, kumuachia Mhe. Spika wetu Jaji wetu Mkuu kama watu wa kawaida tu mitaani hivi ni kwa sababu hamuwapendi, hamna uwezo au roho mbaya tu kwa serikali. Hili akija anieleze ili bajeti yake, nisije nikaikwaza, aje anijibu kwa kina. Niendelee hapo hapo Mahakama, lakini katika masuala ya majengo.

Waheshimiwa dharau nyengine inayodharauliwa Mahakama imezidi. Nimefanya *follow up feasibility study* kwa kushirikiana na Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe pale, tukaangalia majengo ya Mahakama yakoje, kumbe yote ni ya kurithi kutoka kwa Sultani tangu enzi za Ukoloni. Ukiangalia serikali hii wanakuwa *executive*, hebu jengeni hili jengo la Wizara ya Katiba na Sheria, kwa nini wapate pesa ya kujenga jengo kubwa kama lile, wasipate pesa ya kujenga jengo la kisasa la Mahakama Kuu. Hiyo si hasadi, ni hasidi. Wamepata pesa za kujenga jengo kubwa kama lile pale kwa ajili ya wizara tu ya Katiba na Sheria, lakini hadi leo hii Jaji wetu mkuu na joho lake jekundu lile apande ngazi mpaka juu wakati kulikuwa na *lift* pale anakwenda kwa *lift,* akifika anateremka anakaa kwenye kiti chake. Jengo lililopo lile la tangu ukoloni halina *lift* jamani, si aibu hiyo? *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama haitoshi nenda Mahakama ya Chake Chake inavuja, feni lile linazunguka tu hamna *AC*, Jaji anatakiwa atoe haki atulie, asikilize kesi na apime haki iko wapi, akishaangalia atoe hukumu, leo hilo zogo la feni liliopo atapataje utulivu. Sasa wanam-*disturb,* ile *great sort and understanding, high thinking ability, deep sort and understanding* ya hakimu wetu haipatikani kwa majengo mabovu kama haya waliyowekwa.

Mhe. Spika, juzi pale kulikuwa na shauri moja limefunguliwa Mahakamani katika jimbo langu, nikalazimika kwenda kusikiliza lile shauri hayo ma-*bench* yaliyopo, moja sijui mguu umekatika, kuna vijana karibu watano walikaa chini pale kwenye *bench* walianguka. Sasa Jaji wetu hana raha, huyo mpeleka shauri hana raha na sisi wasikilizaji wa hayo mashauri hatuna raha katika Mahakama hizi, hili ni tatizo. Sasa mtwambie kila unapokwenda katika Ofisi za Serikali kuna viti vya kuzunguka wakiona hakizunguki wanatia *gear*, hakizunguki kiti, unaweza kukipeleka juu au chini, leo Mahakamani wanatumia mabao, huu si uadui jamani? Kama si uadui, basi ni hasadi, kama si hasadi, basi ni roho mbaya ya serikali.*(Makofi/Kicheko)*

Mhe Spika, sasa niende katika maslahi ya watumishi katika Mahakama. Kwanza niwashukuru Tume ya Uajiri wa Mahakama pamoja na serikali kwa kuweza kufanya marekebisho ya maslahi ya Mahakimu wetu na majaji, lakini pamoja na hayo marekebisho yaliyofanywa majaji bado wanahitaji kuangaliwa sana ili wapate kitu cha kuwatosha mifukoni, akili yao ifanye kazi wasije wakapata vishawishi vyengine wakaja wakashindwa kutoa haki vilivyo. Mimi napendekeza pamoja na marekebisho, basi yaongezwe maslahi yao.

Mhe Spika, jengine ni kuhusu suala hili la watumishi wa chini, madereva, matarishi na makarani hawakuangaliwa katika maslahi haya, makarani wa Mahakama maslahi yao madogo mno hayakuangaliwa.

Mhe Spika, Mhe. Jaji ikiwa hakupelekwa Mahakamani na dereva hawezi kufika, ikiwa Jaji keshafika Mahakamani akusomee *file* tu, *file* namba ngapi, kesi namba ngapi na karani wa pale hawezi kufanya kazi, kwa nini hawa tusiwaone katika maslahi, maslahi ya makarani wa chini na watumishi wa kawaida katika Mahakama nayo lazima yaangaliwe. Mhe. Waziri, lazima wayaangalie hata mkata majani wa Mahakamani, pale naye kuna kesi za Mahakama Kuu zinakuja pale Chake Chake ikiwa hakufanya kazi vizuri Jaji wa Mahakama Kuu akija pale si itakuwa aibu, lazima apaweke vizuri waone na wao katika masuala haya wanajaliwa.

Mhe. Spika, sasa nihame hapa Mahakamani niende katika Ofisi ya *DPP*.

Mhe Spika: Mheshimiwa, muda umekwisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana. *(Kicheko)*

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, tunakushukuru kwa mchango huo isipokuwa Waheshimiwa Wajumbe, nataka muelewe tu kwamba Ofisi ya Jaji Mkuu na Ofisi ya Spika haikupenyeza bahasha kwa Mheshimiwa. Ni mchango wake binafsi kwa mujibu anavyoona. Kwa hivyo, isije ikahusishwa kwamba labda kuna bahasha zimepita hapana, hakuna hicho kitu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo kuna tangazo moja, mara baada ya kuakhirisha shughuli zetu mchana huu, Waheshimiwa Wawakilishi wa *CUF* wanatakiwa wakutane ukumbi wa juu. Baada ya tangazo hilo, Waheshimiwa Wajumbe sasa niakhirishe kikao hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nikushukuru kunipatia nafasi hii jioni, hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii, lakini pia, niwapongeze watendaji wake kwa kufanikisha hadi akaiwasilisha hapa leo.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba nianze na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kuhusu jengo la Wizara. Ni muda mrefu sana tangu Wizara iwe na lengo hili la kujenga jengo la Wizara, lakini juhudi zao kwa kweli zinakwamishwa na ufinyu wa bajeti na uingizaji wa pesa ambao Serikali inaingiza. Niunge mkono hotuba ya Kamati na hapa nasisitiza tu kuwa serikali ni vyema wakaingiza kwa mpangilio na inavyotakiwa fedha ambazo Wizara ya Katiba na Sheria inahitaji ili kuona kwamba inajenga jengo lile la Wizara.

Mhe. Spika, kwanza ucheleweshaji wa jengo hili unapelekea kupoteza kodi ya wananchi.Kweli tunajua kwamba ujenzi utakavyoujenga sasa sivyo utakavyoujenga mwaka unaofuata. Kwa hiyo, kucheleweshwa kwa jengo hili kwanza ni kutupa kodi za wananchi ambao ni wavuja jasho wanahangaika wao, lakini ucheleweshaji wa miradi kama hii hupelekea kupotea kwa kodi hizi.

Mhe. Spika, lakini pili, Taasisi za Idara hizi nyingi zina ufinyu wa nafasi, kwa mfano Tume ya Kurekebisha Sheria wao wame-*settle* hivi karibuni tu baada ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhama na kuhamia Mazizini, ndio angalau wamepata nafasi, lakini kila siku walikuwa wakihangaika kutokana na kutokuwa na Ofisi Maalum, lakini ukamilishwaji wa jengo hili utasaidia sana, lakini hata taasisi zake nyengine kama Vizazi na Vifo, *Wakfu* na Mali ya Amana pia ile sehemu ambayo wanakaa sio nzuri. Kwa hiyo, ni vyema serikali ikaliona hili na kuona kwamba sasa ipo haja ya serikali kuingiza pesa ipasavyo katika ujenzi huu, ili kuona kwamba kwanza wana-*save* ile kodi ambayo

ya wananchi inapotea. Lakini pili, taasisi ambazo zipo chini ya Idara hii zipate utulivu wa kufanya kazi kwa kuhamia jengo ambalo ni bora ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Mhe. Spika, naomba niingie kidogo katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Napongeza sana juhudi zinazochukuliwa na Ofisi hii katika kuona kwamba inafanya kazi kwa ufanisi, lakini pia, kwa uzalendo. Kwa sababu tunaona kwamba pamoja na ufinyu wa bajeti ambao upo katika Ofisi hii tunaona kazi zinaenda pamoja na yote. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali na Wizara kwa ujumla iwe inaangalia Ofisi hii. Bajeti pamoja na kwamba tunaambiwa haitoshi mara ile nilisema kwamba wenyewe wanasema siku hizi hamna keki kuna visheti, lakini nilisema kwamba kisheti hicho, basi sio mnafyonza sukari yote, halafu ndio mnawapatia wenzenu, kigaiwe sawa sawa ili tuone kwamba kila mtu anapata utamu wa hicho kisheti.

Mhe. Spika, saa nyengine ndio maana ile hekma ambayo imesema "Ukipewa wa kulia mkono wa kushoto usijue" naiona umuhimu wake, kwa sababu kuna Ofisi nyengine zina majukumu madogo, lakini unaona kwamba uingizwaji wao wa pesa ni afadhali, kuliko Ofisi nyengine ambazo zina majukumu makubwa, mtu ana Ofisi ndogo ndogo katika Mahakama za Wilaya, lakini unaona kwamba ule uingizwaji wake wa pesa sio mzuri. Kwa hiyo, ni vyema hili likatizamwa tena.

Mhe. Spika, sote tunafahamu kama maelezo ya hotuba ya Mwenyekiti ilivyosema kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka ni mtendaji tunamjua tunamfahamu, lakini sasa hii kutoingiziwa pesa kwa wakati na pesa ambayo kidogo, kidogo inarudisha nyuma ule utendaji wake. Kwa hiyo, tunaomba hili lizingatiwe serikali ione kwamba iipe umuhimu kwa sababu ufinyu wa bajeti wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, namaanisha kwamba hata wananchi nao wanakosa kupata ile haki yake ipasavyo. Kwa sababu kama Ofisi hii haitafanya kazi ipasavyo na wananchi kwa kweli watakosa hii haki yao.

Mhe. Spika, vile vile, hata mishahara ya waendesha mashtaka najua suala hili linashughulikiwa na serikali, lakini ni vyema likaangaliwa kwa umakini zaidi tukaona kwamba ipo haja ya kuongeza. Hawa wanafanya kazi kubwa kwa sababu wao wanashuka kwenye *field* kabisa, sio kama wanakaa Ofisini *on the desk.* Kwa hiyo, ni vyema mishahara yao ikatizamwa, lakini sambamba na mishahara pia waendesha mashtaka wanakosa usafiri, mtu inabidi anakwenda kazini na nguo mbili kwa sababu ukishakumaliza kusikiliza kesi yule ambaye unamtia hatiani hawa jamaa zake hawatokuelewa. Kwa hiyo, inawafanya kuchukua nguo mbili kwamba akimaliza kazi anabadilisha ili akitoka nje aonekane sio yule mwendesha mashtaka. Kwa hiyo, haipendezi ni vyema tukaiangalia Ofisi hii.

Mhe. Spika, lakini pia, ufinyu huo huo wa bajeti unapelekea kwamba kutokuwa na ufanisi kiutendaji katika zile Ofisi zao za wilaya, lakini sisi kama Kamati tulikwenda katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na tuliambiwa kwamba kuna baadhi ya wilaya bado hawajawa na Ofisi za kudumu za Wakurugenzi wa Mashtaka na baadhi ya wakati inawabidi wamhoji shahidi katika gari.

Mhe. Spika, haipendezi, mimi sijaona serikali yenye *mobile offices* kama gari. Najua mabenki yana *mobile offices*, lakini serikali haiwezekani. Kwa kweli haipendezi ni vyema wakaingiziwa hii bajeti yao vizuri ili kuona kwamba ofisi hii inafanya kazi.

Mhe. Spika, Mwenyekiti amesema, tunaamini hapa Mkurugenzi wa Mashtaka ni mtendaji, lakini kwa kweli tunamrudisha nyuma kutokana na ufinyu wa bajeti wa Ofisi yake, wakati mwengine tunaweza kufikiri labda kwamba wanam-*sabotage* makusudi. Kwa hiyo, naomba serikali iangalie hili wamuingizie pesa zake kwa wakati ili tuone ule utendaji wake.

Mhe. Spika, sitaki kusema mengi, lakini niseme kwamba sio yule ambaye tulikuwa tunamjua, yaani utendaji umeshuka kutokana na bajeti ambayo ameingiziwa.

Mhe. Spika, naomba niingie katika Ofisi ya Msajili wa Mali na Biashara, kama nilivyoeleza katika matatizo ambayo Mkurugenzi wa Mashtaka anakabiliana nayo, ni matatizo yale yale ya ufinyu wa bajeti ambayo yanamkabili Msajili wa Mali na Biashara, lakini nimepata faraja kidogo kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha wakati anawasilisha hotuba ya mapendekezo na makadirio ya mwaka huu alisema kwamba katika hatua za kuimarisha mapato 2014/2015 wana mpango wa kuimarisha usimamizi wa kimaeneo na katika hatua za kuimarisha mapato hayo Ofisi ya Msajili wa Kampuni na Biashara nayo imetajwa. Kwa hiyo, kidogo nina matumaini na Ofisi hii na nimwambie tu Mhe. Waziri

wa Fedha kwamba ili kuifanya Ofisi hii yale malengo ambayo wametegemea yawe *effective* ni bora malengo hayo yaendane sambamba na kuimarisha utendaji wa Ofisi hii.

Mhe. Spika, bajeti ile iliyopita nji asilimia 31 tu ya bajeti ya maendeleo ambayo Ofisi hii imefanya. Sisi tulienda, lakini tuliona kwamba hamna chochote kilichofanyika kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, ni vyema tumepata faraja kwamba imetajwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha, labda huenda mambo yakabadilika, lakini hata hivyo waitizame sana.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo, mimi sitosema mengi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hiyo, nikiisema itakuwa kama narudia yale ambayo Mhe. Mwenyekiti, ameyasoma katika hotuba yake.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tu naomba niingie Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Naunga mkono pongezi za Kamati kwa Ofisi hii, kwa kweli napo hapa kazi nzuri inafanyika. Kama hotuba ilivyosema kuwa Ofisi hii inatekeleza kwa vitendo masharti ya sheria ya kuanzishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Ni kweli hata nilipokuwa naangalia kitabu cha *PBB* unaona kabisa vile viashiria vinavyo-*determine* kuwa kazi inafanyika vinaonekana.

Mhe. Spika, kwa mfano katika programu hii ya *PBB* wamesema kwamba moja katika lengo ni kuimarisha utawala wa kisheria na ukiangalia ni kweli kwa vitendo kabisa wameanzisha vitengo mbali mbali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na unaona kabisa kwamba kazi zinafanyika, mabadiliko yanafanyika, misaada inawasilishwa kwa wakati na yale malengo mengi ambayo wamelenga kuimarisha, kwa kweli unaona kabisa kwamba yanaimarika. Kwa hiyo, niseme tu kama hotuba ilivyosema kwamba ni vyema sisi wengine tukaiga mfano katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuona kwamba tunapoanzisha kitu, basi tuwe na utayari wa kuanzisha kile kitu. Kwa mfano tunapoanzisha sheria, basi tuone kwamba ile sheria inawekwa katika matendo kabisa kama walivyofanya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba ya Mhe. Mwenyekiti, lakini pia, hongera za pekee ziende kwa Mwanasheria Mkuu pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini pia, niwapongeze watendaji wao kwa sababu wao ndio wanasababisha kwamba viongozi hawa wawili wanafanya ile kazi ambayo inatakiwa.

Mhe. Spika, nimalizie na Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki, hapa sitosema mengi kwa sababu bajeti ya mwaka jana nilisema sana na Mhe. Waziri aliniahidi kwamba lile deni la *ZBC* kwa Ofisi ya Hakimiliki kwamba litalipwa kidogo kidogo ili kuona angalau linapungua, lakini mpaka hivi leo ninavyosema *ZBC* hawajalipwa hata shilingi moja katika lile deni. Kwa hiyo, sitosema sana, lakini nasubiri bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ili nione Waziri mara hii atasema nini.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hii asilimia mia juu ya mia na nawaomba Wajumbe wenzangu waijadili, waunge mkono na waipitishe.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii vile vile kumpongeza na kuwashukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake katika Wizara hii kutokana na kazi nzito na ngumu ambayo wanaendelea nayo. Haidhuru kuna baadhi ya matatizo ya hapa na pale, lakini kama binadamu tutajitahidi kushirikiana pamoja mpaka tuhakikishe kwamba matatizo hayo yanamalizika.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kwenda katika ukurasa wa 323 kifungu 0011, kifungu kidogo 281400 Gharama za Kukodishwa. Kifungu kidogo 281402 Gharama za Kukodi Ukumbi wa Mikutano.

Mhe. Spika, katika bajeti kuu iliposomwa hapa nilimsikia Mhe. Waziri wa Fedha akisema kwamba kuna mpango wa kuweza kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima na hususan katika kutumia kumbi hizi za mikutano na kuonekana kwamba matumizi haya ya kumbi zetu za kawaida yatumike zaidi kuliko kwenda kukodi kumbi katika hoteli nyengine ambazo hazistahili, lakini hapa nikiangalia nakuta kwamba katika makisio yaliyofanyika mwaka 2013/2014 Mhe. Waziri, aliomba milioni 4 kwa ajili ya shughuli za mikutano katika kumbi mbali mbali, lakini

mwaka 2014/2015 Mhe. Waziri ameomba milioni 18,500. Ongezeko hili ni kubwa mno na bado sijashawishika kuruhusu fungu hili la fedha kuweza kuendelea kutumika katika Ofisi yake mpaka pale atakaponitosheleza kwa maelekezo ya kina ambayo yatanishawishi ili nikubaliane na matumizi ya fedha hizi ndani ya Wizara hii.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakuja katika hoja ambayo imeletwa na mwananchi na kutaka kwamba tulisemee hili. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba hii Mahakama hasa ni lini zitakuwa zinatenda haki kwa watu wanyonge na watu wa kawaida. Kwa sababu kuna mwananchi mmoja ambaye amehukumiwa kifungo cha miaka 10 jela, lakini akaja katika utaratibu wa rufaa. Baada ya kufika kule kwenye rufaa wakili wake, sasa ni mwezi wa nne anapigwa "danedane" katika kutafuta ile *proceeding* tu ili aweze kuendelea na taratibu zake haki yake iweze kupatikana.

Mhe. Spika, lakini hadi leo hii njoo kesho, njoo kesho kutwa, njoo mchana, njoo jioni. Mhe. Waziri atakapokuja hapa, naomba atusaidie ni utaratibu gani unaotumika kwa watu wanapoomba *proceeding* ili waweze kupata haki zao za msingi na wananchi waweze kurejesha matumaini na imani zao katika vyombo hivi vya kuhukumu kisheria.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo kuna na kesi nyengine ya mtoto ambaye amebakwa na ametiwa mimba, lakini alipokuja katika taratibu za kisheria huyu mtu ameambiwa kwamba hawezi kupata mwelekeo wa kesi yake mpaka mtoto yule ajifungue. Mtoto yule ukiangalia umri wake ni mdogo, umbile lake ni dogo, lakini vile vile, mambo haya yapo na hawa watu wanataka kujua mwelekeo wa hatma yao, lakini hakuna kitu cha msingi na cha maana ambacho wanaweza kukielewa wakajua hatma ya suala lao ambalo limewakabili. Mhe. Waziri atakapokuja hapa nitaomba pia na yeye atusaidie kupata mwelekeo wa suala hili.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika eneo la dini kidogo. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa siku ya leo anisaidie ufahamu ndani ya Zanzibar yetu tuna misikiti mingapi? Lakini pia, katika hiyo misikiti tuliyonayo baina ya Unguja na Pemba, ni misikiti mingapi ambayo inasaliwa sala ya Ijumaa. Vile vile, naomba kupata ufahamu wa uwiano wa utendaji wao baina ya ofisi hii inayoongozwa na yeye ambayo inaongoza masuala ya misikiti, pamoja na misikiti hii ambayo inasalisha sala za Ijumaa. Nini mahusiano yao baina ya Wizara na misikiti hii?

Mhe. Spika, na nikiondoka hapo sasa ninakuja katika jambo ambalo ni kero kwa ndugu zetu wa Kimahakama na si jengine, bali ni utaratibu mzima wa *court recording system*. Mfumo huu wa *Court recording system* umekuwa unatumika katika maeneo mbali mbali duniani. Ukiangalia hata wenzetu Tanzania Bara wanatumia mfumo huu, Kenya vile vile, hata na Uganda na Rwanda wanatumia mfumo huu.

Mhe. Spika, lakini mfumo huu matokeo yake yanasababisha kesi kuweza kupelekwa kwa haraka na kuweza kupata hukumu kama vile ambavyo watu wanakuwa wanatarajia. Sasa ni sababu zipi zinazosababisha kwa upande wetu hapa Zanzibar hatutumii mfumo huu. Ningemuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa ni namna gani wizara yake imejipanga katika kuhakikisha kwamba na wao kama hawatumii mfumo huu wanajipanga katika kuutumia mfumo huu.

Mhe. Spika, jengine pamoja na kelele nyingi zinazopigwa, maelezo mengi yanayotolewa ikiwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na vyombo mbali mbali juu ya suala zima la madawa ya kulevya pamoja na namna ya kuweza kudhibiti madawa haya kwa waingizaji na watumiaji wa madawa haya, lakini kumetokezea kitengo ambacho kimetusikitisha sisi pamoja na wale watu ambao wanaotoa hukumu juu ya masuala haya madawa ya kulevya na mambo mengine.

Mhe. Spika, atakapokuja hapa Mhe. Waziri, nitaomba anisaidie ufahamu ni sababu zipi zilizopelekea nyumba za Majaji ambao walikuwa wakilindwa zamani na Jeshi la Polisi na watu wengine wengine, kuondoshewa ulinzi na sasa hivi nyumba zile kuwa wanakaa bila kuwa na ulinzi na vile vile kuhatarishiwa maisha yao na wakawa hawana imani na hakika ya maisha yao kutokana na matokeo na kesi nzito ambazo nyengine huwa wanazihukumu.

Mhe. Spika, kama unavyojua watu wanaoshughulikia na biashara hizi wanakuwa ni watu ambao wana mtandao mkubwa, wana nguvu kubwa, wana mambo mengi, lakini kitengo cha kusababisha kuondoshewa ulinzi Jaji ambaye atakuwa anatoa hukumu kwa kesi kama zile kwa mfano, ni jambo ambalo linahuzunisha sana. Ningelimuomba Mhe. Waziri akija hapa atwambie ni sababu zipi zilizosababisha Majaji hao kuondoshewa ulinzi katika nyumba zao.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa ninapenda vile vile nifahamishwe na Mhe. Waziri aje kutoa tamko hapa juu ya deni la Afisi ya Hati ya Miliki. Ni lini deni hili litalipwa na kama deni linashindikana kulipwa, basi Mhe. Waziri akija hapa atusaidie majibu ili wale ambao wanasubiri fedha hizi waweze kujijua kwamba wamezikosa au watakuwa wanazipata.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo kwa heshima na taadhima, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja hii kwa asilimia 80, naweka asilimia 20 hadi pale nitakapopata majibu yatakayonitosheleza ili niweze kukubaliana na hoja hii.

Mhe. Spika, ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ninakushukuru Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Ni zamu yake sasa Mhe. Ali Salum Haji, baadae Mhe. Abdalla Juma Abdalla, wakati Mhe. Panya Ali Abdalla anajitayarisha.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia jioni hii ya leo. Mimi sina makubwa sana katika wizara hii na niseme tu kabla sijaanza kuchangia naiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mambo yangu yatakwenda katika hoja kama nne. Moja nilikuwa ninataka Mhe. Waziri hili atusaidie kulitetea suala la mirathi. Kiutaratibu watu wanapokwenda kufanyiwa masuala yao ya mirathi katika Afisi hii, kunakuwa na asilimia ambayo inachukuliwa na serikali. Sasa unajua sisi wengine huwa tunapata tabu kwamba leo mtu yatima kilichoachwa na wazee kinakuwa ni kidogo, lakini unakuta kuna asilimia inabidi ni lazima iende serikalini.

Mhe. Spika, kwa nini inanipa tabu, inanipa tabu kwamba makato haya sijui yanafanya kazi gani. Kwa sababu wafanyakazi wana mafao kutoka serikalini, lakini ninaamini hata vitendea kazi navyo tunaviweka kwenye bajeti kama *stationaries* na mambo mengine. Sasa kufikia pahala kwamba ile mali ya yatima. Pia, tukafika pahala tukaweza kuichukua kuipeleka serikalini, mimi hili ninataka Mhe. Waziri anisaidie. Kwa kweli mimi ninahisi hatuwatendei haki kwa wananchi wale, kwa sababu yatima anakuwa ni mtu mnyonge, haki yenyewe inakuwa ni ndogo, wakati mwengine unakuta kile kinachogaiwa ni kidogo, lakini na *still* unakuta na serikali inafika pahala kile kile kidogo ambacho tunahisi kingeweza kumsaidia mayatima, basi serikali inazichukua, baada ya kuwajenge uwezo mayatima kuwasaidia zaidi, basi tunakuwa tunachukua na zile haki zao ambazo wazee wao wameziacha.

Mhe. Spika, sasa mimi nilikuwa naomba moja kama kuna uwezekano wa kufanya jitihada ya kuweza kuiondosha ile asilimia, basi iondoshwe kabisa, kama haiwezekani, basi angalau ile asilimia tuipunguze pale ilipo izidi kushuka chini. Kwa sababu imefika pahala tuseme ukweli kuna watu sasa hivi wanakimbia wanaogopa hata kumwambia uende ukakague mirathi yako, anakwambia nikenda huko kuna pesa zitakatwa, sasa kunakuwa kuna taabu. Inabidi watu wanagawana mirathi katika njia za uraiani na inakuwa njia za uraiani wakati mwengine taaluma zinakuwa ndogo, inafika pahala haki inakuwa hatendeki.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala zima ambalo wenzangu wamezungumza masuala la majengo ya Mahakama, lakini mimi ninataka kwenda katika maeneo mawili tu. Ninataka labda nimwambie Mhe.Waziri labda hivi kweli ameliona hili eneo la jengo la Mahakama ya Mwanakwerekwe na Mahakama ya Mfenesini na ameviona vile vyumba vya makarani ambavyo katika utendaji wao wa kazi. Hivyo, kweli tunaweza kuwatendea haki katika hali kama ile.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri hebu aliangalie kwa uhalisia zaidi kwamba bado Majaji wetu na hususan katika maeneo haya mawili, sisemi kwamba binaadamu kwamba kila pahala tunaona. Tunashukuru kwamba kuna baadhi ya majengo tumeyaona, mimi nimefika Makunduchi nimeona mabadiliko ya Mahakama ya Makunduchi na nilimtembelea mpaka Mhe. Jaji alipokuwa kakaa katika ile Afisi ya Mkuu wa Wilaya kule. Sasa mabadiliko tunakuwa tunayaona, lakini sasa tuangalie na hawa wenzetu wa maeneo haya yaliyobakia, basi kufanya jitihada ili na wao kuweza kuondosha ili waweze kufanya kazi zao katika mazingira yaliyokuwa mazuri.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Salim Ali, wakati alipokuwa anachangia pale alitaja mfano wa feni, akasema kwamba feni halimletei raha Karani au Mhe. Jaji, wakati linazunguka kwa ule mlio, lakini mimi ninaweza kusema kwamba alisahau kitu kimoja tu kukielezea kwamba pia unaweza kufanya kazi kwa wasi wasi unaogopa lile feni likaanguka ukahatarisha maisha yako. Kwa hivyo, unaweza kuhukumu katika mazingira ambayo yaliyokuwa sio mazuri. Sasa labda nimuombe Mhe. Waziri achukue jitihada katika hili.

Mhe. Spika, lakini jengine na kubwa ambalo limenikaa katika nafsi yangu mimi na ningemuomba Mhe. Waziri anisikilize kwa utulivu sana hapa. Sisi Waislamu tuna utamaduni na hususan katika mazingira ya nchi yetu ambayo tunasema karibuni asilimia 90 ya Wazanzibari ni Waislamu na Wajumbe wengi wanapozungumza katika Baraza la Wawakilishi, wanazungumzia katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kuweka kinga na wengine wanapiga vifua sana, hususan Mhe. Saleh Nassor Juma hapa kwamba watu wanakuwa wanakula ovyo, watu hawavai vizuri na serikali yetu tunaitaka iwe makini katika suala hili.

Mhe. Spika, lakini kuna jambo mimi linanipa taabu ambalo Mhe. Waziri naomba anisaidie. Sisi tunaiambia serikali ifanye jitihada kwa wale ambao wanakula mchana kweupe ili iwachukulie hatua, lakini sasa hivi tumejenga utamaduni huu unatupa mashaka. Huu utamaduni wa Uislamu wa pande mbili; kote Waislamu, sasa sijajua ni Uislamu wa madhehebu au Uislamu wa mapenzi, kwa sababu kumekuwa na hitilafu katika suala zima hili la ufungaji.

Mhe. Spika, kuna watu wanatizama mwezi wa dunia, kwa imani zao, kwa matakwa yao na kwa mapenzi yao, lakini kuna watu wanatizama mwezi wa nchi kwa imani yao, kwa matakwa yao na ufahamu wao wa kielimu. Sasa hili linakuwa linatupa tabu. Tabu inayotupata ni kitu gani? Tabu inayotupata kuna watu ambao wanaanza kutangulia kufunga, wale ambao hawajaanza kufunga wanawafanyia riha wale wenziwao. Sasa inafika pahala inakuwa watu wanakula ovyo.

Mhe. Spika, sasa sisi tunakataza kwamba watu wasile ovyo, lakini wale ambao hawajaanza kufunga wanaanza kuwafanyia riha wale ambao wenziwao wameanza kufunga. Wewe umefunga nini bwana! mwezi umeshaandama mtu anakula. Sasa tunakataza nini kwamba tumefika pahala tunashindwa kulizuia suala hili. Haya ya mwezi mzima wa siku 28 kwa nini tuyazuie, kwamba kuna baadhi ya siku sheria inakuwa haifanyi kazi, watu tunawaacha wanafanya wanavyotaka, lakini kuna baadhi ya siku sheria inapotaka kufanya kazi, sasa nahisi kwamba inafika pahala tunawaonea watu bure.

Mhe. Spika, kama tunaamua kwamba mtu ale kwa mapenzi yake na sheria zake zinamruhusu tu afanye anavyopenda, basi tuwaache tu isijekuwa kuna baadhi ya siku tunabagua. Kwa sababu hata zile siku za muandamo wa mwezi wa siku za Sikukuu kuna watu kwa imani yao na elimu zao, wanasema leo mwezi mimi haujaandama mpaka amsikie Mufti atutangazie mwezi, lakini kuna mtu anakwambia mimi mwezi wangu wa Saud Arabia umeshaandama.

Mhe. Spika, sasa sisi tunakuwa katika funga, wenzetu wao wanakuwa wanaendelea na mambo ya Iddi na wanakula. Sasa hii inakuwa inatupa taabu kwa wale Waumini. Sasa mimi ninafikiri labda tuandae utaratibu uliokuwa mzuri na Mhe. Waziri ninafikiri ananifahamu vizuri. Hata kama watu imefika pahala wanafungua kwa imani zao, basi kuwe na utaratibu kama tulivyojenga utaratibu watu wasile ovyo, hata zile ibada zao wazifunge kwa utulivu, kwa sababu hili linatuharibia hata vijana wetu.

Mhe. Spika, kwa nini ninasema linatuharibia vijana. Kwa sababu kuna vijana bado wana Ujahili wa kutokuwa na imani ya kutofunga. Sasa wakishasikia Saud Arabia imefungua, ijapokuwa yeye hajafunga, vipi bwana! Saud Arabia imeshafungua bwana wache tule. Sasa inakuwa vijana wetu wanatafuta sababu za kula ovyo pasipo na kufungua na kutubebesha majukumu.

Mhe. Spika, sasa hili Mhe. Waziri atusaidie vizuri sana kwa sababu ni suala ambalo linatupa mashaka, sisi tunahimizana kwamba mwezi Mtukufu wa Ramadhani uheshimiwe, watu usiku ibada wafunge ,lakini kuna watu kwa imani zao, sasa imekuwa balaa tena, maana yake kila siku zikenda ndio mambo yanazidi. Tangu ilikuwa Saud Arabia, sasa wanatuanzia kuwa umeandama Iran, sisi ni Wayahudi. Sasa itafika pahala tunaanza mwezi ishirini kila mtu anaanza kula, inakuwa ule utaratibu wa kujijengea heshima wa nchi yetu unakuwa unaondoka.

Mhe. Spika, sasa ningemuomba Mhe. Waziri tuandae utaratibu uliokuwa mzuri au tutoe taaluma nzuri kwa wale wenzetu ambao imani zao, kwa sababu mtu imani yake huwezi kumkataza, kwa sababu kila mtu ana imani yake na kila mtu ana ufahamu wake wa kielimu. Mimi mwalimu wangu ni Sheikh Mussa Makungu ameshafariki na nilikuwa ninamuheshimu sana na Mwenyezi Mungu amrehemu.

Mhe. Spika, nikishatoka hapo, nilikuwa ninataka nije katika suala la sheria za nchi. Nimuombe Mhe. Waziri hebu tufanye jitihada ya kukaa sasa na kuangalia. Ninajua una kazi kubwa sana na tulikuwa tuna matumaini labda tukishakurudi kwenye Bunge la Katiba, baada ya kupitisha Katiba na sheria labda tukirudi hapa labda tutaendelea na Katiba ya Zanzibar kuifanyia *review* ili twende nzuri. Unajua sheria nyingi zimekuwa zimepitwa na wakati, yaani sheria hazina nguvu. Mwenyezi Mungu kama utaziangalia sheria za Mwenyezi Mungu kwa wale Waumini wa Dini ya Kiislamu, utahisi kama Mwenyezi Mungu anatuone hivi kwa sababu anasema, "Ukiiba ukatwe mkono".

Mhe. Spika, sasa suala la kwamba mtu kaiba nazi mmoja ukamkate mkono, ndio mwizi hata haijaambiwa kaiba nini, wewe ukiiba tu iwe shilingi hamsini au shilingi moja, adhabu yako ukatwe mkono. Sasa inafika pahala mtu kaiba shilingi mia akatwe mkono. Ndio Mwenyezi Mungu kwa sababu kaweka adhabu kali ili watu wafahamu na waache kufanya vitendo viovu. Unaambiwa ukizini kama mjane uuliwe. Sasa inafika pahala unaona ni adhabu nzito.

Mhe. Spika, lakini sasa na sisi zile adhabu zetu zinaonekana bado kuwa zipo *weak*, kwa sababu kwanza ni za muda mrefu na hazifanyiwa *review*. Sasa zinatupa *disturbance* kwa wananchi wetu. Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu imefika pahala yale matendo ya uvunjaji wa sheria mtu anakuwa hana hofu na inafika pahala matendo yale yanatuletea majanga. Sasa hivi mtu unamkuta gari ya mizigo anapakia na abiria, hajali. Gari wanavyozitengeneza wenzetu wanazitengeneza kwa *balance* kwamba hii inatakiwa ibebe mizigo kwa sababu ikibeba abiria, gari ikija iki-*hang* anakosa *balance* inapinduka.

Mhe. Spika, sasa unamkuta mtu haoni taabu kwa sababu anajua, hata mimi nikikamatwa na askari nikipelekwa Mahakamani anajua faini yangu ni shilingi mia tano au shilingi elfu. Sasa hizi sheria zinafika pahala bado zinakuwa zinaathiri jamii. Leo inafika pahala Mwenyezi Mungu atuepushie mbali, kama utakaa njia ya Fuoni, njia ya Mwanakwerekwe kuelekea Makunduchi, kuna utamaduni wa gari za Kusini, sasa hivi kwamba ni gari za abiria unaikuta ndani imetia abiria, lakini juu imeekwa shehena ya matofali. Ninasema *Yarabi* Mungu ifike salama, lakini ikija ikikatika na gari zenyewe unakuta kuwa *board* tunatengeneza, sisi wenyewe Wazanzibari, *board* za mbao ambazo hazina *guarantee* kwamba labda kule juu uweke wa tani ngapi? Ikija ikikatika matofali yanauwa watu, labda yatakapouwa watu ndio itajulikana.

Mhe. Spika, na gari hiyo hiyo inapita katika vituo vya Polisi vyote. Sasa ninasema watu wamekuwa hawaogopi, kwa sababu mtu amekuwa haogopi hata nikija kutiwa hatiani faini yenyewe ni shilingi mia tano, wakati yeye anapata faida shilingi elfu. Sasa unakuta anachokipata ni kingi kuliko kile ambacho yeye hata akikamatwa na kupelekwa Mahakamani inakuwa ni kidogo.

Mhe. Spika, sasa niombe tu Mhe. Waziri aziangalie hizi sheria nyingi za zamani ambazo zinakuwa zinatupa mashaka na ukiangalia hazina makali ya kufika pahala watu kuweza kuheshimu sheria. Kwa hivyo, hilo ndilo ninalotaka kuzungumza na zipo nyingi sheria ambazo kidogo zimekuwa zipo *weak* kutokana na wakati wetu, tangu hayo mambo ya kikoloni faini ya shilingi moja na faini shilingi tano. Sasa ndio mambo yanakwenda pasipokuwa na utaratibu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ninafikiria hilo nitakuwa ninamalizia, ninasema sina mashaka sana kwa sababu hii ni taasisi ninaiheshimu sana, ni taasisi iliyokuwa na watu Maulamaa. Sasa ninadhani sisi tunataka radhi za Maulamaa, tukija tukikosa radhi za Maulamaa itakuja kuwa ni mtihani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana, Mheshimiwa mwenzangu hapa alizungumzia hii Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hapa leo hatusemi sana kwa sababu tunajua wa kuja kumwambia ni Mhe. Waziri wa Fedha namna ya uingizaji wa fedha katika suala la Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, Afisi hii ina masikitiko makubwa sana na tunakuwa tunapata tabu. Inafika pahala mpaka mtu unahisi labda unafanya kwa njia ya kufanya *demotion* kwamba labda aione tabu ile kazi aache.

Mhe. Spika, mwaka jana kama sikosei bajeti yao imepata angalau asilimia 52, wameshindwa kufanya kazi zao vizuri. Mwaka huu ile bajeti imepunguzwa. Sasa sisi tunakuomba kitu kimoja. Mwaka huu tunaomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, kile ulichompunguzia mpaka ikafika pahala cha mwaka jana humpi, unampa kidogo, basi mwaka huu hebu mpe kadiri itakavyostahiki ili hicho kidogo atakachoweza kukipata ili afanye shughuli zake.

Mhe. Spika, hii taasisi ni lazima tukiri. Ninafikiri Mhe. Waziri akija ataniambia, sasa hivi wanasheria katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wanakimbia, kwa sababu ya kufanya kazi katika mazingira magumu. Watu wote wanaangalia maslahi ndio dunia sasa hivi, hata leo na wewe tuseme tukutengenezee maslahi uwe na vimurimuri na ma-*body guards* ndio dunia. Sasa isije kuwa tunaangalia upande mmoja, upande mmoja hatuangalii. Kuna hatari kufika pahala hiyo Afisi ikawa haina wanasheria. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hata *AG* anakiri ninafikiri kuna mtu ameshakimbia ameshakwenda kwake, kuna mwengine kenda uwanja wa ndege, kuna mwengine kakimbilia Bara. Sasa atakuja kufanya kazi Mhe. Ibrahim Mzee Ibrahim peke yake pale, akae na majarada yanataka kwenda kwenye kesi wanasheria hana, makesi yatarundikana itakuja kuwa kuna matatizo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa naomba tumuonee huruma sana huyu kijana. Sisi tuna imani sote hakuna mmoja asiyejua jitihada au uwezo wa ndugu yetu Ibrahim Mzee Ibrahim. Ni kijana muadilifu, kijana mchapa kazi, mtu ambaye ana *knowledge* ana uwezo wa kila hali, lakini amekuwa anapata matatizo ya utendaji wa kazi kutokana na hii halisi iliyokuwepo hapa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nina wasi wasi hata huyo Mkurugenzi mwenyewe wa Mashtaka akija akifika pahala aka-*resign*, akasema bora nikae nyumbani, kwa sababu huwei kufanya katika mazingira kama hayo hata siku moja, nina wasi wasi na ninamuombe dua Mwenyezi Mungu ampe imani aendelee kutumia nchi yake na nina imani kwamba Waziri wa Fedha atumuonea huruma.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naunga mkono hotuba niseme tena, sina mashaka kabisa. Nina imani majibu yangu yatakuja mazuri. Nakushukuru, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Abdalla Juma Abdalla baadae Mhe. Panya Ali Abdalla wakati Mhe. Awadhi Salmin Awadh anajitayarisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi ninakushukuru kunipatia nafasi hii ya kusema maneno mawili matatu katika hoja hii iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, ninataka nianze na ukurasa wa 10 kuhusu Mahakama. Kwa kawaida utendaji wa Mahakama huwa hauhojiwi sana kwa sababu ni muhimili unaojitegemea, kazi zake ni kazi maalum na wanahitaji *independence* ya kutosha, lakini mara nyengine huwa tunalazimika kulenga lenga jicho kidogo pale Mahakamani kwa sababu kazi moja kubwa ya Mahakama ni kutoa haki.

Mhe. Spika, na ukishasema kutoa haki, maana yake unaigusa jamii moja kwa moja ambayo kwa upande moja na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni wadau wa hii jamii ambayo inatakiwa ipate haki kutoka Mahakamani.

Mhe. Spika, sasa sitaki niseme sana, lakini naomba sana Mahakimu wetu, Majaji wetu kwa kweli wajitahidi kidogo, kwa sababu kuna mambo yanatokea ambayo hayafurahishi sana, mengine yako nje ya uwezo wao. Kwa mfano, kama kucheleweshe kesi, hili limekuwa ni tatizo au changamoto ya muda mrefu sana, lakini changamoto hii haimo ndani ya uwezo wa mahakama peka yake, kwa sababu wadau wa kesi ni wengi. Mara nyengine mahakama iko tayari kusikiliza kesi lakini wadau wengine wanachelewesha.

Kwa hivyo, kwa hili ni nung'uniko la watu wengi, lakini hatuwezi kuibana mahakama peke yake moja kwa moja. Mara kwa mara tumesema na tunapata sababu za msingi kwamba tatizo hili ni kubwa na ni gumu na litaendelea kwa muda mrefu, kwa sababu hata ukiangalia kesi zilizopokelewa na ambazo zinapatiwa ufumbuzi basi utaona kama kutakuwa na mrundikano wa kesi na siku moja itafika kesi 10,000 katika nchi hii, hazijapata majibu au hazijapatiwa ufumbuzi. Nasema hili sio la mahakama peke yake na wadau wengine, naomba niseme kwamba kila mdau anayehusika wakiwemo wakili wa serikali na wakili wa kujitegemea, mashahidi na polisi wajitahidi kuharakisha

kesi, kwa sababu unapochelewesha kesi mara nyengine unasababisha mazingira yasababishe ushahidi upotee. Mazingira yanasababisha hata hiyo kesi iwe haina maana tena. Kwa hivyo, ajitahidi kila mdau anayehusika na kesi.

Mhe. Spika, lakini kuna mengine ambayo ni ya kibinadamu na mara nyengine tunapswa kuwalaumu kidogo mahakimu wetu na hii mimi kama Abdalla Juma Abdalla siwezi kusema kitu kwa sababu sio mtaalamu wa sheria, wala sijui kesi zinavyoendeshwa kule. Lakini hawa hawa wadau wa kesi ambao ni wataalamu wa kujua kesi zinahukumiwaje, sijui *appeal* inakatwaje. Ni hawa hawa ambao wanatulalamikia kwamba kuna baadhi ya wenzetu kana kwamba hawako *serious* katika kutoa hukumu. Tuliyasema haya kwa wizara na wizara ilichukua hatua, lakini bado matatizo kama haya yanaendelea kujitokeza Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana wenzetu hawa wa mahakama wajitahidi kwa sababu ni hatari unapokuwa unajaribu kukwepa kufanya haki mpaka jamii ikajakupoteza imani na vyombo kama hivi, itakujakuwa tatizo kubwa. Maana leo mtu anakuwa na imani mtu akinifanyia sivyo wacha nimpeleke mahakamani ili haki yangu ipatikane, sasa akija kukata tamaa kwamba kule haki sitoipata basi atalazimika kufanya analojua yeye mwenyewe, sasa na hiyo haitokuwa sura nzuri kwa jamii yetu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana wajitahidi.

Jambo jengine kuhusu mahakama Mhe. Spika, kwa kweli wenzangu wamesema humu na mimi nataka nisisitize tena. Miundombinu ya mahakama imechakaa mno, majengo yale ya mahakama hata ukiangalia mule kwenye zile chemba za mahakama kwa kweli zimepitwa na wakati sana. Tunapaswa kwa namna moja ama nyengine na hili sio la waziri moja kwa moja, lakini mwenyewe yumo humu Mhe. Waziri wa Fedha. Hii miradi ambayo wizara ina-*propose* kwa ajili ya mahakama au kwa ajili ya taasisi mbali mbali, kwa kweli ni muhimu sasa ipewe kipaumbele nayo, kwa sababu miaka 50 hii ya Mapinduzi mpaka leo tunatumia. Kuna mjumbe mwenzangu alisema, mpaka leo tunatumia majengo yale ya kurithi ambayo yalipojengwa, yalijengwa kwa wakati huo. Wakati huo idadi ya Wazanzibari ilikuwa watu 300,000, sasa hivi tuna milioni moja karibu na 400,000, sasa bado tunatumia majengo ya miaka hiyo, yamepitwa na wakati sana.

Mhe. Spika, pale Chake Chake kamati yetu ilipokwenda kukagua, kwa kweli unaweza kulia, hata ile hali ambayo uliiwacha wewe pale sasa haipo. Maana yake mahabusu hawana pakukaa, ofisi ya *DPP* pale imewekwa sehemu maana yake ukiiona unaweza ukalia, kama ni mtu kweli na taaluma yake na heshima yake anaweza kukaa pale akafanyakazi. Baada ya pale alipo *DPP* huku kuna choo na wala sio choo ni matofali yamewekwa, hakuna bati, hakuna chochote, vundo la mikojo ya mahabusu pale, yaani ni aibu! Kwa hivyo, naomba sana majengo kama yale yalengewe jicho bwana, tusiwe tunalemaa mpaka katika muda kama huu.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda sio rafiki sana, naomba niache hapo niende kwenye Ofisi ya Mufti kidogo. Ofisi hii ya Mufti Mhe. Spika, ina kazi muhimu sana katika nchi hii na miongoni mwa kazi ambazo mimi nazipa uzito mkubwa sana ni kuhusiana na kujitahidi kutoa mawaidha na nasaha kwa ajili ya kulinda maadili yetu ya Wazanzibari. Lakini pamoja na kazi ngumu sana ambayo Ofisi ya Mufti wanapaswa kuifanya, Mhe. Spika, inasikitisha kwamba ofisi hii haiwezeshwi, maslahi yao yanakuwa ni madogo mno ukilinganisha na kazi zao, hawawezi kufikia malengo yao hata kwa nusu ya malengo waliyojipangia kwa mwaka kutokana na pesa ndogo ambayo wanapewa. Ukiangalia *other charges* mwaka huu ambao unamalizika, walipangiwa shilingi milioni 183, walichogaiwa ni shilingi milioni 62 peke yake ambayo ni asilimia 34.

Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuangalia Ofisi hii ya Mufti ni taasisi ambayo ina sheria yake, hivyo inapaswa kuwa na *vote* yake, lakini mpaka leo bado haijawekewa *vote* yake na matokeo yake inategemea wizara ndio iipangie mambo yake, haiko huru hii Ofisi ya Mufti. Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, akishirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha wajitahidi hii ofisi kuipatia fungu lake na hata maslahi yao kidogo yaongezwe, ili waweze kufanyakazi vizuri sana.

Mhe. Spika, nilitaka nizungumzie huu mmomonyoko wa maadili ambao unashughulikiwa na Ofisi ya Muftip. Najua peke yake hawawezi kufanya, lakini wao ndio wamepewa jukumu. Nchi yetu Mhe. Spika, sasa inatisha, kwa sababu nchi hii ina Waislamu wengi sana, karibu asilimia 98 sijui nukta ngapi na hata hawa wasiokuwa Waislamu ni watu wana dini na wanapaswa na wao kuwa na maadili mema, lakini nchi yetu imeanguka sana kimaadili.

Kwa mfano, kuna maeneo Mhe. Spika, katika nchi hii sasa hivi yanaitwa majina ya ajabu ajabu. Kwa mfano utaambiwa pahala fulani panaitwa *buibui pack.* Mimi nilipouliza *buibui pack* maana yake ni nini. Nikaambiwa

maana yake wanakwenda wasichana ambao ukiwatizama huku nje wamejihifadhi vizuri mpaka zile nikabu zao, lakini wanasehemu wakifika wanajipambazua yote yale na wanabakia katika hali ya kutisha mno, ni hatari sana Mhe. Spika, mambo haya yanafanywa katika nchi hii.

Mhe. Spika, kuna maeneo sasa hivi katika nchi hii kuna biashara ya ngono wazi wazi, anakwenda mtu anasema mahitaji yake, nataka mtu mwenye sifa hii na hii bei gani, anaambiwa bei, halafu anapewa mtu anakwenda kustarehe naye pahali, yanafanyika ndani ya nchi hii. Mambo haya sisemi ni ya Ofisi ya Mufti peke yake, lakini ni mambo ya dola nzima. Mhe. Spika, ni aibu mambo haya kuyasema kwenye watu kama hivi, lakini kutokana na hali ilivyo tusipo yasema hapa basi Mwenyezi Mungu hatotusamehe.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu ana vyombo vingi vya sheria, kuna Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inashughulika na mambo hayo, kwa sababu ni uvunjifu wa sheria. Kuna mahakama na vyombo vyengine kama vya Mufti vinashughulika na haya mambo. Mimi nadhani mambo haya kuna haja ya kuyashughulikia ipasavyo, tukiiwacha jamii iendelee hivi Mhe. Spika, nchi yetu ni visiwa tena visiwa vidogo. Lile wimbi lililowapata watu wa Indonesia, sisi nusu yake tu litatumaliza hapa. Kwa hivyo, naomba sana sisi kama viongozi wa jamii hii ili tusiiwachie kabisa tulichukulie hatua ili kukomesha vitendo vya aina hii.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulichangia ni kwamba Ofisi hii ya Mufti moja katika kazi zake ni kusajili Misikiti na kusajili Madrasa za Qur-ani. Sasa katika nchi yetu tuna dini zaidi ya moja. Kuna Waislamu hapa, kuna Wakristo na inawezekana kukawa na dini nyengine pia sina hakika. Sasa nilikuwa nauliza Ofisi ya Mufti kazi yake ni kusajili Madrasa na Misikiti ambayo ni mambo ya Kiislamu, je, hivi dini nyengine usajili wake unasajiliwa wapi? Kwa sababu nimekuta humu kuna taasisi tatu zinasajili, lakini kuna moja inasajili Vizazi na Vifo, nyengine inasajili biashara na mali sijui na nyengine inasajili Hakimiliki, lakini sijaona inayosajili hizi taasisi nyengine za kidini.

Nasema hivi Mhe. Spika, kwa sababu moja katika nyenzo ya kulinda amani na utulivu katika nchi yetu ni kutendeana vyema hasa sisi wana dini, dini ya Kiislamu, dini ya Kikristo na kama kuna dini nyengine tuwe tunafanya ibada zetu bila ya kubughdhiana na bila ya kufanyiana aina yoyote ya vitendo visivyostahiki.

Mhe. Spika, kuna kesi ambayo nimeipata mimi, hii kesi inawahusu watu wa pale Kisauni kuna kijiji kinaitwa Mitondooni. Mitondooni kuna Msikiti pale, kuna wenzetu walikwenda kununua eneo na huyo muuzaji kwa kuwajua aliwaambia mnanunua eneo hili lakini pana Msikiti karibu, naomba sana msijekujenga Kanisa hapa na bahati nzuri hao wanunuaji wakakubali hilo sharti, wakasema tunanunua madhumuni yetu ni kujenga *Dispensary* na kujenga shule kwa ajili ya kusaidia watu wa Mitondooni.

Mhe. Spika, shule ilijengwa lakini badala ya kujenga *Dispensary* wakajenga kama banda hivi, halikuwa rasmi, lakini hatimaye banda lile likageuka Kanisa. Sasa kilichokuwa kinafanyika hakikuwa kinapendeza, kwa sababu walikuwa wanafanya ibada zao, lakini ibada zao kidogo zinatofautiana na sisi Waislamu, ibada zao mara nyengine wanakuwa wanatia kanda zile za *CD* zinapiga kwaya na mambo yao mengine tena kwa kutumia kipaza sauti, na bahati mbaya sana walikuwa wanafanya hivyo nyakati za swala. Sasa watu wa pale hawakufurahia hilo tendo.

Siku moja wakatoka watu wasiopungua 50 wakaja kwenye Ofisi ya Mufti kwa ajili ya kuja kushtaki kidogo. Ofisi ya Mufti ikashughulikia kikamilifu, ikenda mpaka kwenye *site* ikaona na kuwakusanya wahusika, watu wa Msikiti walikuwepo, wana kijiji walikuwepo, watu wa hilo Kanisa walikuwepo, muuzaji wa hicho kiwanja pia alikuwepo; wakafanya *lujna* kubwa ya kuzungumza. Mazungumzo yao yalithibitisha kwamba ni kweli na yule mnunuzi alikiri kwamba ni kweli niliambiwa mimi kuwa hapa nisije nikajenga Kanisa.

Mhe. Spika, pamoja na hayo lakini suluhu haikupatikana kwa sababu baadaye yalitokea maneno yaliyokuwa hayakumfurahisha Mhe. Mufti na akaiandikia barua Ofisi ya Mrajis, sijui ni Mrajis yupi ndio nilikuwa nataka kujua ni Mrajis yupi anayesajili taasisi hizi za dini. Lakini pamoja na kumuandikia mapendekezo yake, maana yake Ofisi ya Mufti ilitoa mapendekezo ili kuumaliza mgogoro huu usije ukavunja amani, ifanywe (a), (b), (c), na (d), bahati mbaya mpaka leo jawabu halikupatikana na watu wa pale pahala, mpaka leo wana nung'unika na hata juzi walinipigia simu wakaniambia tatizo lao bado lipo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili suala alifanyie utafiti na ikiwezekana na akigundua kuwa pana kasoro, basi kuna haja ya kuchukua hatua vyovyote atakavyoona yeye inafaa, lakini amani na utulivu ya eneo lile isije ikapotea, Mhe. Spika amani ni kitu muhimu.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, labda nimalizie kwa kuzungumzia kidogo kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Spika, moja katika kazi za kamisheni hii, ina kazi nyingi pia nayo, lakini moja katika kazi zake ni kukusanya Zakka za Waislamu halafu wakazigawa. Mhe. Spika, hii ni kazi moja muhimu sana kwa jamii, tukiangalia Zakka kwa Muislamu ni nguzo kabisa, kama ilivyo nguzo ya Swala, ilivyo nguzo ya Hijja, ilivyo nguzo ya Swaumu basi na Zakka nayo ni nguzo. Inapaswa Waislamu waithamini Zakka au waifanyie kazi kama wanavyoifanyia kazi Swala. Sasa bahati mbaya hili suala halijapata kufanyiwa kazi sawa sawa, yaani Zakka inayokusanywa kwa mwaka ni ndogo sana ukilinganisha na mazingira yetu ya Zanzibar.

Kwa hivyo, labda nitumie fursa hii kuwanasihi Wazanzibari wenzangu huu ni wajibu wetu, kuanzia sisi wanasiasa tuliopo humu ndani, lakini na wafanyabiashara na watu wengine. Zakka ni wajibu wetu na tunapaswa tuithamini Zakka au tuitekeleze kama ambavyo tunatekeleza Swaumu na Hijja. Tusipofanya hivi Mhe. Spika, mabalaa mengi yanazipata jamii kwa kukiuka maadili ya Kiislamu na kuikwepa Zakka ni kukiuka maadili ya Kiislamu na tusidhani hata siku moja kwamba Mwenyezi Mungu atatutizama tu sisi, ni lazima atatutia adamu kwa njia moja ama nyengine.

Kwa hivyo, naiomba sana Ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, ijitahidi kutoa taaluma, ijitahidi kuwa na nyenzo za kukusanyia Zakka, lakini pia ijitahidi katika kusimamia na kuratibu namna ambavyo Zakka inapelekwa kwa watu wanaohusika, ni muhimu sana.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nizungumzie kidogo kuhusu Mrajis wa Vizazi na Vifo. Kwanza nataka nimpongeze kwa juhudi zake, amefanya juhudi kubwa ya kuboresha miundombinu hii ya ofisi. Amejitahidi sana hapa Unguja na sasa jicho lake linaangalia kule Pemba, naamini atakuwa na ofisi nzuri. Lakini kuna kasoro moja Mhe. Spika, inajichomoza na hii inaweza ikaharibu sifa nzuri aliyonayo Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Spika, hizi shughuli sasa zinafanywa katika Ofisi za Wilaya, mategemeo yangu mimi nilidhania pamoja na kuwa ofisi hizi ziko katika Ofisi za Wilaya, lakini uratibu wote unafanywa na Wizara hii ya Katiba na Sheria, kumbe mambo yanaanza kubadilika na matokeo yake majukumu yote wanaachiwa ile Ofisi ya *DC* ifanye, na bahati mbaya Ofisi ya *DC* imetawala na wanasiasa zaidi. Sasa hii haki ya kuwapatia wananchi targisi za vizazi na vifo sasa inaanza kuingia dosari kwa sababu Mhe. Spika, kuna vyeti vinatayarishwa vingi sana, ambavyo sijui kwa misingi gani.

Mhe. Spika cha kushangaza hata Ofisi ya Mrajis mara nyengine hawajui kinachoendelea, wakati yeye ndio mdhamini wa Vizazi na Vifo, lakini kuna vyeti vinatayarishwa vinagaiwa kwa watoto na yeye Mrajis hajui kinachoendelea, sasa hii ni hatari. Kwa sababu sasa hivi kumeanza kujitokeza matatizo ya vyeti, mimi nina cheti changu cha kuzaliwa au nina cheti cha mwanangu lakini siku nyengine naweza kuitwa kule mimi nikachukue cheti changu kule Ofisini cha cha mtoto wangu. Mimi cheti changu ninacho hicho chengine cha nini, sasa hapa kuna jambo linafanywa na mimi namuomba sana Mrajis ili kujiweka katika nafasi nzuri, ni vizuri uratibu wa vyeti vya kuzaliwa ukabakia katika ofisi ya Mrajis kupitia katika Wizara ya Katiba na Sheria, na pale ofisini Wilayani pale iwe ni nyenzo tu ya kuwakaribishia wananchi ile huduma ipatikane kwa karibu zaidi, lakini wasiachiwe Ofisi za DC na watu wake, hawatutendei haki.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja hii na namuomba Mhe. Waziri yale ambayo nimeshauri namuomba yafuatiliwe, ajitahidi kuyafuatilia ili ufanisi upatikane katika Wizara hii. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae katujaalia uhai wake tukaweza tukakutana hapa jioni hii, pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi ili niweze kusema mawili matatu katika hotuba hii. Kabla sijaanza mchango wangu na mimi nataka nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanikisha katika kutuletea bajeti hii.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeeleza katika tume ya kurekebisha sheria imefanya utafiti wa kuonesha sheria na ikasema kuna Sheria 34 ambazo hazina utata, Sheria 61 zisizotumika na zilizopitwa na wakati na Sheria 120 zilifutwa. Mimi nilikuwa nataka nijue hizo sheria ambazo zimepitwa na wakati ni ngapi ambazo zitaletwa ili tuweze kuja kuzifanyia ukarabati mzuri na ziweze kutumika.

Nataka nimuombe Mwanasheria Mkuu katika sheria ambazo zitakuja kufanyiwa marekebisho basi na ile sheria inayohusu mavazi nilikuwa naomba sana iletwe kwa sababu ilikuwa ikitusumbua sana wajumbe kuona sasa mila na utamaduni wetu unapotea kwa kasi kubwa .

Mhe. Spika, niende kwa Mkurugenzi wa Mashitaka; na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Mashitaka kwa bidii kubwa anayoifanya katika utendaji wake wa kazi pamoja na ufinyu wa bajeti yake, hata hivyo anaonekana kwa kile ambacho anakipata basi anakitumia ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao. Mhe. Spika, niombe Ofisi hii bila ya kuiwezesha ni kweli tutakuwa tunalia msongamano wa kesi kwa sababu yeye ndiye ambaye anatayarisha wafanyakazi ambao wanakwenda kusimamia kesi, kwa hivyo niombe serikali izingatie kumuwezesha bajeti yake ambayo sisi wenyewe tumekuwa ni walalamishi wakubwa, tunasema kama kesi haziendi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende Ofisi ya Mufti na nilitaka niulize suali kwa sababu kazi yake ni kutembelea misikiti pamoja na madrasa zetu na kutatua migogoro mbali mbali inayowahusu waislam. Mimi nilitaka niulize Ofisi hii ya Mufti inazisaidia vipi vifaa vya juzuu na mas-hafu zile madrasa ambazo zimeshasajiliwa lakini wao bado hawajabahatika kuzitembelea, ili kama kuna utaratibu unaotumika na wao waweze kuutumia huo utaratibu na wao waweze kufaidika na vifaa hivyo kwa kuwasaidia wanafunzi.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Ofisi ya Mufti kwa kushirikiana na waislam katika kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S. A. W) lakini pia niwashukuru kwa kushirikiana na waislam kwa kuadhimisha mwaka mpya wa kiislam kwa sherehe zilizo nzuri. Hili niseme ni faraja kwa waislam kwa sababu tulikuwa tunapitwa na kuzingatia mwaka wetu, lakini Ofisi hii ilivyojitahidi kuandaa sherehe hizi kwa sasa Waislam tumekuwa tunajifunza mengi na tutaendelea kujifunza mengi katika matukio mbali mbali ambayo yanahusiana na historia ya dini yetu. Nawapongeza na waendeleze na kila kukicha sherehe hizi zizidi kufana sana.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii vile vile inajishughulisha na kujibu maswali ya dini ambayo mengine yanahusu ndoa na talaka, mimi nataka nitoe ushauri katika Ofisi hii, masuali ya talaka yanapoulizwa na hizo talaka zenyewe ndio zimeshatoka ndio mtu anauliza ndio apate kipengele lakini nishauri ofisi hii kuweza kutayarisha somo maalum la ndoa na talaka kabla ya wanandoa hawajafunga ndoa, ili kuepusha hizi talaka na ndoa ambazo zinavunjika kiholela holela.

Mhe. Spika, pia niulize Ofisi hii ambayo ndio Ofisi hapa kwetu inayoshughulika na mambo ya kiislam, niwaulize ni vipi wanakemea mambo ambayo tunayaona yanadhalilisha uislam, kwa sababu kuna vitendo ambavyo wengine wanavifanya hivi kwa kweli huwa vinaudhalilisha uislam, sasa wao ofisi hii inavikemea vipi. Kwa mfano unaposikia walimu wa madrasa wanashutumiwa juu ya kesi hizi za ubakaji! Kwa kweli kitendo hiki huwa hakileti sura nzuri, kwa hivyo ofisi hii pia ilitakiwa kukemea sana tukio hili kwa sababu walimu ndio ambao tunawategemea kuzalisha vizazi vilivyo bora.

Mhe. Spika, pia inakemea vipi inapotembelea katika misikiti na kuona misikiti inakithirisha kuzungumza siasa ndani ya misikiti badala ya kuwafunza waislam ambao wamefika katika misikiti ile wakaweza kujifunza dini yao, kwa sababu Mhe. Spika, si kila anayekwenda msikitini anaijua dini ipasavyo, hivyo mashekhe tunawaomba sana tunapokwenda katika misikiti yetu huwa tunatarajia kupata elimu ambayo itatusaidia katika dini yetu, tuweze kujua mambo ambayo yanaharamisha, tuweze kujua mambo ya faradhi na sunna yanatendwa vipi. Kwa hivyo tunaomba sana Ofisi hii inapotembelea Misikiti na hili iweze kulisema ili mashekhe waweze kurudi katika mstari, waweze kutusaidia waislam tuweze kutekeleza ibada zetu ipasavyo.

Mhe. Spika, niende katika ofisi ya Vizazi na Vifo; kwa kweli ofisi hii nayo naipongeza kwa juhudi ambazo inazichukua, lakini pia kuna changamoto ile ya usajili wa vifo ambalo hili bado ni tatizo kubwa na bado wananchi hawajaelewa. Kupitia nafasi hii niliyoipata hapa naomba nitoe wito kwa wananchi wajitahidi kama wanavyojitahidi

wakati wa kuwasajili watoto ambao wamewazaa basi vile vile kinapotokea kifo waweze kukisajili kifo cha mtu yule kwa sababu kuna faida kubwa za kufanya hivyo.

Mhe. Spika, niende katika Ofisi ya Hatimiliki; Ofisi hii nayo naipongeza kwa kazi nzuri ambayo inachukua kwa kuwashughulikia wasanii wetu pamoja na wabunifu ili waweze kupata haki zao, lakini ofisi hii nayo bado ina changamoto ya wafanyakazi, kwa hivyo niiombe Wizara kushughulikia suala hili ili waweze kupata wafanyakazi wa kutosha waweze kuendelea na majukumu yao vizuri.

Pia niiombe Wizara ya Habari ambayo kwenye Shirika la utangazaji la ZBC waweze kuwalipa fedha zao ili na wao wenyewe waweze kujiendeleza katika mambo yao mengine.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye Ofisi ya Wakfu na Mali ya amana; Mhe. Spika, hapa pia nina suali; ofisi hii kwa kweli imeweza kufanya kazi nzuri mwaka 2013, iliweza kutoa misaada ya kheri kwa vikundi 88, mimi nilitaka kuuliza juu ya mafanikio ambayo yamepatikana katika utunzaji wa mali hizo ili ofisi iweze kuendelea kuwajsaidia wajasiriamali wengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na tulipokwenda katika Ziara tulipotembezwa na Kamisheni ya Wakfu tulitembelea katika mashamba na tulikuta mashamba mengi yakiwa yana miti mikongwe tena mmoja mmoja na tukawashauri waweze kuipanda tena miti mipya ili yaweze kupatikana mavuno na wale wastahiki waweze kupata mafao kama kawaida. Nilitaka kuuliza tukio hili limefikia wapi, na pia walisema watashughulikia mipaka ya mashamba hayo, nilitaka kujua suala hili limeshafanyika na kama limefanyika limefikia wapi.

Mhe. Spika, niende katika Mahakama; nami pia nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa jitihada pamoja na changamoto za uingizwaji wa fedha, lakini pia na wao wawe wanajitahidi pale panapoingizwa fedha basi kwa kweli wawe wanaweza kukarabati majengo, kwa mfano jengo letu la Mahakama kuu kwa kweli sasa hivi kidogo linaridhisha sio kama lilivyokuwa pamoja na wezangu wanapendekeza kwamba tujenge majengo mapya, hiyo ingezidi kuleta sifa zaidi, lakini yale ambayo yamekarabatiwa pia tunashukuru.

Mhe. Spika, pia niwashukuru na niwapongeze kwa kuweza kuwalipa ma-*assessors* madeni yao yale ya nyuma ingawa bado changamoto hii ya madeni bado ipo lakini pia wameweza kufanya vizuri. Basi niiombe serikali kuongeza juhudi za kutatua changamoto hiyo. Pia niiombe Wizara na wao waweze kuingiziwa fedha kwa wakati ili waweze kutatua changamoto zao.

Mhe. Spika, niseme na nimpongeze Mhe. Salehe kwa jambo ambalo alilisema leo, katika siku ambayo alisema jambo kubwa na zuri na ni kweli tunapaswa sote kuzingatia jambo hili, sio jengine ispokuwa kuhusu viongozi wetu wakuu akiwemo Jaji Mkuu na Mhe. Spika, kwa kweli viongoi wetu hawa sio wa kuwafananisha tu na viongozi wengine wowote na wao wana sifa zao, na wao wanastahiki mambo mengine kufanyiwa. Viongozi hawa ni wakuu katika nchi hivyo Mhe. Spika wetu wa Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa wetu Spika wa Bunge haki anazozipata Spika wa Bunge basi ni kubwa wakati ni Tanzania moja hii hii na cheo ndio hicho hicho kimoja, kwa hivyo tunaomba sana Serikali iweze kulizingatia jambo hili kama viongozi hawa na wao wapewe heshima inayostahiki.

Mhe. Spika, sambamba na hilo pia Mahakimu wetu na wao kuwaacha bila ya kuwa na usafiri wa uhakika hatuwatendei haki, kutokana na mazingira ya kazi zao. Mimi mchango wangu ulikuwa mdogo na nilitaka niseme hayo kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa dakika hizi ishirini kama nitazimaliza nizungumzie hutuba ya Mufti wetu hapa Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza yeye kwa kusimamia Wizara hii lakini pia niwapongeze na watendaji wake wote katika Ofisi zake kwa kufanya kazi nzuri katika mazingira magumu kwa kiasi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa ameeleza mengi katika hotuba yake lakini mimi nitazungumzia zaidi katika Idara zake tatu ambazo muda huu utaweza kutosha, lakini kwanza nizungumzie juu ya hiyo bajeti yenyewe. Katueleza

mpango wa Mapato na Matumizi ya Wizara yake na utekelezaji wa mpango huo kwa bajeti iliyopita na makadirio ambayo yanategemewa kupatikana katika kipindi kijacho.

Kwa kweli Mhe. Spika, bajeti ni ndogo hata pale mnapokadiria makadirio yenyewe yanakuwa ni madogo lakini inatokana na hali halisi ya mapato yetu na safari hii Mhe. Waziri wa Fedha ametwambia bajeti halisi imezingatia uhalisia sio bajeti ile ya kukadiria pesa nyingi halafu ukapata kidogo, kwa hivyo tunaweza ku-*challenge* mwakani huu uhalisia ama umepatikana au vipi.

Jengine Mhe. Spika, ninalotaka kusema kwamba Baraza hili la Wawakilishi la wananchi Mheshimiwa Aboud Jumbe alipolizundua alisema kwamba ni ngome ya wananchi, Baraza la wananchi ni ngome ya wananchi kwa hivyo kama ni ngome ya wananchi wananchi wamekuwa wakitegemea sana chombo hiki ama kupitishia mambo yao ama kupitishia malalamiko yao, na hasa pale baada ya kuona kwamba wamegonnga ukuta au shughuli zao hazishughulikiwi katika taasisi husika.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tusije tukaonekana kwamba chombo hiki ni Mahakama kwa sababu wapo baadhi ya watu wanasema Baraza la Wawakilishi sasa limegeuka Mahakama, linahukumu, hapana sisi hatuhukumu isipokuwa tunawasilisha hapa malalamiko ya wananchi na hiyo ni haki yao, kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi na tunawakilisha hapa malalamiko ya wanananchi ili basi Wizara au watendaji wanaohusika warekebishe hiyo hali na waone kwamba kama wanafanya vizuri au wana fanya vibaya basi chombo hiki ndicho chenye mamlaka, kwa sababu Baraza la Wawakilishi ni chombo pekee chenye mamlaka ya kuiambia serikali, hakuna chombo chengine. Kama si Baraza la Wawakilishi kusema sasa kutakuwa tena hakuna chombo chengine cha kuiambia serikali. Kwa hivyo moja kati ya jukumu letu ni kuiambia serikali na wananchi wanajua hivyo na ndio maana tunakuwa tunapokea pokea baadhi ya mambo ambayo tunalazimika tuyawasilishe hapa, ili yapate ufafanuzi na pale tutakaporidhika basi tunaridhika na wananchi wanatusikia.

Mhe. Spika, nije sasa katika chombo cha Mahakama; mimi niipongeze Mahakama kwa juhudi zao za kufanya marekebisho ya Ofisi zao, ofisi ambazo ni muda mrefu tumekuwa tukizizungumza, tumeona jengo la Mahakama Kuu pale limefanyiwa ukarabati mkubwa na majengo mengine yanajengwa majengo ya kisasa, tuwaombe waendelee na ujenzi ule ili ofisi zile ambazo wananchi wanazitumia basi ziwe katika hali nzuri zaidi huko tunakokwenda. Isipokuwa mbali ya majengo na shughuli nazo zinatakiwa ziende kwa ufanisi.

Mhe. Spika, wananchi wanazitegemea sana Mahakama zao kwa kupata haki zao, kusikiliza kesi zao. Sasa wananchi wanapofika pahala wakakosa imani na Mahakama zao hili ni jambo la hatari. Kwa hivyo tumuombe sana Jaji Mkuu pamoja na majaji wengine na Mrajis kuona kwamba Mahakimu wetu katika ngazi mbali mbali wanafanya uadilifu wa hali ya juu, wanatoa maamuzi juu ya kesi zinazopelekwa pale. Maamuzi ambayo kwa wanavyofahamu wao na kwa uwezo wao wanajua kwamba hii ndio haki.

Itakuwa si vyema Hakimu au Jaji anahukumu kesi au anatoa maamuzi akijua kwamba hivi ninavyohukumu sivyo. Hakimu kama huyo ana dhima kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu sisi ni binaadamu, binaadamu hatujakamilika, tunatakiwa tutumie uwezo wetu, maarifa yetu na akili zetu za mwisho kuona kwamba hivi ninavyofanya ndivyo. Kwa hivyo niwaombe sana wahukumu kwa uadilifu, wafanye shughuli zao kwa uadilifu ili baadae wasije wakapata tabu huko mbele ya safari tunakokwenda kwenye maisha ya milele.

Suala la ucheleweshaji wa kesi nalo ni suala kubwa na zito, wananchi wamekuwa wakilalamika zimekuwa zikiahirishwa bila ya utaratibu, watu wanaacha shughuli zao wanakwenda Mahakmani lakini kesi utasikia imeahirishwa bila sababu za msingi. Kwa hivyo tuwaombe Mahakama kwamba wawe wanazisikiliza kesi na kutoa maamuzi kwa muda unaostahiki kuliko kucheleweshwa cheleweshwa. Haki iliyocheleweshwa Mhe. Hamza alisema juzi hapa haki iliyocheleweshwa *so and so and so on.*

Kwa hivyo moja ambalo nilitaka kulizungumzia juu ya Mahakama zetu siku hizi kumekuwa na utaratibu wa Mahakama zetu kutoa hukumu lakini hukumu zile hazitekelezwi. Sasa mimi najiuliza nchi yetu hii tunaiongoza kwa misingi ya utawala wa sheria. Lakini Mahakama inatoa hukumu lakini hukumu zile hazitekelezwi na Mahakama yenyewe iko kimya. Maana imekuwa kama wao wanaondosha njiani hukumu.

Mtu aliyepewa amri ya kutekeleza ile hukumu hatekelezi na hakuna kitu kingine ambacho kinafuata baadaye. Mimi naona wanazidhalilisha hata Mahakama zenyewe kwamba wewe Hakimu au Jaji umetoa hukumu lakini hukumu yenyewe haitekelezwi na wewe mwenyewe uko *silence* na hakuna lolote linaloendelea.

Kwa hivyo mimi nadhani Mahakama nazo sasa ziwe *serious* na kuhakikisha kwamba zile hukumu wanazozitoa hata kama zinaigusa serikali, basi zitekelezwe. Kwa sababu hayuko mtu aliyekuwa juu ya sheria. Leo utashangaa Mahakama inatoa amri ya kukamata gari za Shirika, gari fulani fulani ikamatwe lakini Polisi hawatekelezi amri ya Mahakama na wenyewe Mahakama bado wapo tu wanaangalia. Kwa hivyo nchi hii inaendeshwa kwa misingi ya sheria tunavyosema sisi, pale hukumu inapotolewa hata kama ni taasisi ya serikali basi kwanza sheria ichukue mkondo wake. Kama kuna mazungumzo basi yatafuata baadae. Lakini leo mambo yanakwenda zigzag, vurugu tu, mwananchi tayari hukumu imeshatolewa lakini hakuna kinachoendelea, kwa kweli tutakuwa hatwendi vizuri.

Jengine Mhe. Spika, nizungumzie juu ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume hii tumekuwa tukiisema sana hasa katika masuala ya utendaji wao; kuna sheria nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho lakini hatuelewi Tume hii ya Kurekebisha sheria inafanya nini. Maelezo haya wameyatoa lakini kwa kweli hayaridhishi katika utendaji wao. Sasa sijui kutokana na ufinyu wa bajeti au vipi. Lakini kuna sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati.

Mhe. Spika, yapo malalamiko ya wafanyakazi wa Idara hii ya Tume ya Marekebisho ya Sheria, kama nilivyotangulia kusema wamekuwa wakilalamika sana na wamekuwa wakimlalamikia hasa Katibu wa hii Tume. Katibu wa Tume amekuwa akilalamikiwa sana na watendaji wake na nadhani pengine hii inachangia kuwa shughuli hizi haziendi. Unapofika pahala wasaidizi wako wanakulalamikia wewe ulio juu hivi utegemee kutakuwa na ufanisi! Kuna milolongo ya malalamiko juu ya Katibu wa Tume hii ya Marekebisho ya Sheria, malalamiko ambayo kwa kweli hayaleti taswira nzuri katika taasisi kama ile muhimu.

Mimi Mhe. Spika, ninavyotaka kusema kwamba Katibu huyu ajirekebishe. Katibu wa Tume afuate maadili ya kazi yake, awapende wafanyakazi wake, awape haki zao zinazostahiki na wala asije akafika pahala akawagawa akawafanya makundi. Unapowagawa watu katika Taasisi yako utegemee kwamba ufanisi hauwezi kupatikana. Watu wake wale amewagawa makundi mawili. Kuna la kwake na kundi ambalo sio la kwake, huu sio utendaji mzuri wa kazi. Unatakiwa kiongozi uwaunganishe watu, uwaunganishe wafanyakazi wako ili ufanisi uweze kupatikana. Unapoanza kuwagawa na kuwaona hawa ndio hawa sio ufanisi huwezi kuupata.

Kwa hivyo, nimuombe sana Katibu kupitia kwako Mhe. Waziri Katibu wa Tume afanye marekebisho juu ya uongozi wake katika Taasisi ile. Wafanyakazi wake wamekuwa na malalamiko mengi. Ninayo malalamiko hapa yameorodheshwa mengi kwa sababu mimi sifanyi kazi kule lakini *staff* wake wameandika orodha kubwa ya malalamiko juu ya matendo ya Katibu wao. Sasa kama ni kweli ama si kweli anapaswa kujirekebisha. Kubwa lililozungumzwa ni juu ya kuwagawa makundi wafanyakazi wale.

Kwa hivyo ajirekebishe ili Ofisi yake iweze kufanya kazi vizuri na Mwenyekiti wake wa Tume nadhani kama yupo na yeye anasikia kwamba hapana uongozi ulio bora katika Taasisi hii. Kama hakuna uongozi ulio bora maana yake hakuna ufanisi na malalamiko na kasoro zitajitokeza kila siku hata upewe bajeti kubwa kiasi gani huwezi ukafanikiwa hata siku moja. Kwa hivyo lazima afanye marekebisho Katibu wa Tume ili kuona Taasisi yake hii inafanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, la mwisho, nimesema nitazungumzia mambo matatu, la mwisho nitazungumzia juu ya Ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka. Hapa Mhe. Waziri katika Ofisi hii kama sikupata maelezo mazuri nitakuwa mgumu sana kupitisha fungu hili. Pamoja na kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi wamesema Mkurugenzi wa Mashtaka anapewa fungu dogo hawezi kufanya kazi lakini kuna kasoro ambazo pengine zinasababishwa na ukosefu huo wa fedha. Kuna mengine hayahitaji ukosefu wa fedha. Unahitaji utendaji mzuri na ufanisi na ufuatiliaji.

Ofisi hii kwa kweli Mhe. Spika, wananchi wamekuwa wakiitegemea sana Mhe. Spika. Kwa sababu ni Ofisi ambayo inashughulikia mashtaka, pale ambapo kasoro imefanyika basi ofisi hii iweze kushughulikia na kuyawasilisha katika Taasisi inayohusika. Lakini pale ambapo Ofisi hii inakuwa kimya, mambo yamefanyika na hakuna majibu mazuri juu ya jambo lililofanyika wananchi watakosa imani na Ofisi hii pia na serikali yao. Sasa hili ambalo Mhe. Waziri

nataka kulisema nataka uje unipe maelezo mazuri sana na hao walalamikaji waridhike juu ya hili tukio au hili jambo ambalo limefanyika.

Mhe. Spika, kuna wananchi wanalalamikia wazee wa askari mmoja ambaye aliuwawa anaitwa Said Abdulrahman, mwezi wa 10/2012 pale Bububu na askari huyu aliuwawa kinyama na mpaka hadi leo hakuna mashtaka yoyote yaliyofunguliwa dhidi ya wahusika. Mhe. Spika, kitendo kumuua mwenzio au kumhujumu mwenzio ni kitendo kibaya, pamoja na kwamba utajiona umejificha lakini Mwenyezi Mungu anakujua, Mwenyezi Mungu anatuona. Iwe waislamu, iwe wakristo, iwe dini nyengine yoyote inayoamini Mungu kama yupo. Unapomfanyia hujuma mwenzio Mwenyezi Mungu kwanza anakuona wewe hata ujifiche vipi na kisha iko siku utarudi kwake na hukumu utaipata huko utakakokwenda. *(Makofi)*

Tunao utaratibu wa kidunia ambapo mtu anapofanya matendo kama haya na ikibainika basi apelekwe katika vyombo vya sheria ikiwemo kupelekwa Mahakamani na Mahakama zetu hizi za kidunia basi nazo zichukuwe mkondo wake. Sasa linapotokea jambo kama hili na watuhumiwa wakakamatwa lakini wakashindwa kupelekwa Mahakamani kutokana na sababu zisizoeleweka kwa kweli wananchi wanakuwa hawatuelewi na ndio maana wakati mwengine wanafika kwetu kutuletea malalamiko. Kwa hivyo Mhe.Waziri nataka uje unieleze kwa kina suala la askari aliyechinjwa, aliyekatwa kichwa pale Bububu na watu ambao wanajulikana hadi leo limeishia wapi.

Kwa sababu ukimya huu umekuwa wa muda mrefu, wazee wake wamepatwa na mfadhaiko mkubwa; Baba yake mzazi kapata maradhi wanaohangaika sasa ni wale ndugu zake baba wadogo. Hii inatokana na kwamba hakuna hatua yoyote ya kisheria ambayo imechukuliwa.

Kwa hivyo tunasema nchi hii tunaiendesha kwa utawala wa sheria kwa hivyo lazima sheria ichukuwe mkondo wake. Watu hawa waliohusika na jambo hili wakamatwe, wapelekwe katika Mahakama washtakiwe kwa mujibu wa sheria na kama wanahusika sheria ichukuwe mkondo wake. Na kama hawahusiki pia sheria ichukuwe mkondo wake. Lakini si vyema jambo hili kuliachia tu kama vile amechinjwa mbuzi au kondoo, yule aliyekatwa kichwa ni binaadamu na ameuliwa akiwa katika sehemu yake ya kazi na waliofanya hivyo wanajulikana.

Leo iweje Mhe. Waziri watu wale waliohusika na tendo lile wameachiwa tu na hakuna maelezo mazuri kwa wazazi wa kijana yule aliyechinjwa mpaka wanafika pahala leo wanawatafuta Wawakilishi wao kupeleka malalamiko yao.

Wameandika barua kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, hakuna majibu yoyote juu ya jambo hili. Wameandika kwa Makamu wa Pili wa Rais wanataka kuonana nae, nafasi ya kupata kuonana nae wameshindwa. Hili si jambo la kufurahisha hata kidogo, matendo haya lazima hatua zichukuliwe na mambo haya hapa kwetu sasa yamezoeleka. Kuna matendo mengi yanafanyika hapa lakini mwisho wake hujui kinachoendelea, sasa hata haya ambayo yamejulikana pia nayo yanashindwa kupelekwa katika vyombo vinavyohusika!

Nataka maelezo Mhe. Waziri utakapokuja hapa kufanya *wind up* ueleze juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika hawa ambao walifanya kitendo cha kinyama na hayo ya akhera tunamuachia mwenyewe Mwenyezi Mungu huko tunakokwenda, lakini ya duniani hapa lazima hatua zichukuliwe. Wahusika wakamatwe wapelekwe katika vyombo vinavyohusika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nitakuwa mgumu kama nilivyosema katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kama fedha zao hazitoshi sasa zitakuwa hazitoshi kabisa maana nitazuia mpaka pale nitakaporidhika na maelezo ambayo Mhe. Waziri atanieleza juu ya kadhia hii iliyofanyika pale Bububu.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kunipa fursa ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nianze kwa kuchangia ukurasa wa 24 Ofisi ya Mufti wa Zanzibar. Mhe. Spika, nianze kwa kuipongeza Ofisi hii kwa kufanikisha vizuri sana Sherehe ya Maulid ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad Salallahu Alayhi Wassalam. Kwa sababu sherehe hii na mimi nilihudhuria, napenda niwasifu sana kwa

kweli wamejitahidi kuandaa vizuri sherehe hii na wananchi wa Zanzibar pia ninawapongeza kwa kujitokeza kwa wingi.

Pia pamoja na pongezi zangu nilikuwa naomba kwa sababu hii sherehe ni ya kitaifa na ni sherehe ya waislamu wote wa Zanzibar au waislam wote wa Duniani basi kila siku mimi husema kuiga jambo jema sio vibaya. Mhe. Spika, hii sherehe isifanywe hapa Zanzibar tu. Hii sherehe inavyostahiki ni vizuri ifanywe kitaifa katika Wilaya mbali mbali zilioko Zanzibar au Mikoa mbali mbali iliyoko Zanzibar. Mwaka huu ikifanywa Mkoa huu mwaka wa pili ifanywe Mkoa mwengine.

Kwa sababu waislamu wa Zanzibar wanataka na wao wafaidike sherehe hii, sasa kila siku kuadhimishwa kitaifa pale Maisara basi sisi tunaona uchoyo na sisi tufanyiwe katika Wilaya zetu au Mikoa yetu na ifanywe kitaifa na wenzetu ndio wanavyofanya. Kwa mfano tunasikia kwenye radio Tanzania Bara siku nyengine wako Tabora inaadhimishwa kitaifa, siku nyengine wako Mwanza. Kwa hivyo na sisi tunataka tuige mfumo huo. Hilo ni moja.

Suala la pili Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri na mimi anisaidie kwa sababu ninafikiri mara nyingi huwa kuna pesa zinazotolewa za zaka kwa ajili ya watu kwenda Makka. Lakini sijui kunatumiwa vigezo gani vya kuwachagua, kwa sababu sijawahi hata siku moja kusikia kama Micheweni ama Chake Chake amesaidiwa labda iwe sipati taarifa lakini sijawahi kusikia mimi kwa kweli. Kwa hiyo, hivyo vigezo vinavyotumiwa vijuilikane kwani Waislamu maskini wapo wengi. Pia Mhe. Waziri atueleze wameshapata watu wa pahali kadha na pahali kadha ili na sisi tupate kuelewa.

Jengine Mheshimiwa nikiendelea na ofisi hii ya Mufti nashukuru kama anawaunganisha Waislamu, anatembelea misikiti lakini pia ningemuomba Mheshimiwa kwa sababu misikiti sasa hivi inakuwa na migogoro sana. Migogoro ya kidini inakuwa imo haimaliziki na kila mara, basi ningeomba Mheshimiwa kwa sababu yeye ofisi yake hawezi kujigawa kila siku ingawa kuna msaidizi kule Pemba, lakini zingeundwa Tume maalum za Wilaya za kusimamia hii migogoro ya kidini ya Waislamu wakasimamia kufanya suluhu.

Mhe. Spika, jengine keshokutwa Mwenyezi Mungu akipenda tunategemea tutaingia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, waziri ofisi yake anajitahidi sana pamoja na Rais wa Zanzibar kutangaza na kupunguza bei ya vitu; Waislamu wafanye ibada, wafanye hivi. Lakini Mheshimiwa nchi yetu kwanza serikali yetu haina dini, lakini nchi yetu ina waumini wa dini wa aina mbali mbali na kila mmoja anatakiwa aheshimu dini ya mwenzake. Kwa hiyo, Mheshimiwa nawaomba sana kupitia ofisi hii ya Mufti suala la watu kwenda ovyo ovyo na kuvaa nguo za maajabu mwezi wa Ramadhani hili mlipigie kelele. Kwa sababu watu wanakwenda ovyo ovyo na wanavaa nguo ambazo kwa kweli pamoja na kuwa kila mtu ana dini yake, lakini na hili likemewe kwani lazima mtu aheshimu dini ya mwenziwe.

Kwa hiyo, kwa sisi Waislamu kwa mwezi wa Ramadhani tunaofunga basi wenzetu wapunguze nguo za kimaajabu ili tufunge mwezi mtukufu wa Ramadhani. Hili naliomba sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka nizungumze ni suala la hii Tume ya Kurekebisha Sheria. Mheshimiwa na mimi nataka niseme kama wenzangu waliotangulia, wamesema kama kuna sheria nyingi ambazo zinastahiki kupitiwa na kuona kama hizi sheria zinataka kufanyiwa marekebisho. Kwa hiyo, moja ya sheria ambazo zinataka kufanyiwa marekebisho kwanza mimi nasema hii sheria inayotoa hivyo vyeti vya vizazi na vifo ni moja inayotaka kufanyiwa marekebisho. Mhe. Spika, kwa sababu nimeshazungumza mara nyingi hapa kama sasa hivi umekuja wakati wa kuwa na vitambulisho vya uzanzibari mkaazi na huwezi kukipata kama huna cheti cha kuzaliwa.

Hiki cheti cha kuzaliwa ni lazima sasa kuna watu kwa bei hii iliyopo hawawezi kukipata. Kwa sababu kuna watu ni wazee sasa hivi wanataka wapate cheti cha kuzaliwa, lakini kwa bei iliyopo shilingi 40,000/= au 30,000/= inakuwa ngumu.

Kwa hiyo, tushazungumza mara nyingi kama wizara hii ya Katiba na Sheria iwapunguzie watu kidogo ili waweze kumudu kupata hivi vyeti. Mhe. Spika, pengine nyumbani kuna watu watatu au wanne hawajapata cheti, kwa sababu zamani cheti ilikuwa tunadharau, lakini sasa umekuja wakati wa kuwa ni lazima uwe na cheti, kama huna cheti hupati kitambulisho, hupati kazi wala hupati fedha benki. Kwa hiyo, ni lazima.

Mhe. Spika, na juzi nilisema hapa kama sheria inasema kama mtu hana kitambulisho afungwe mwaka mmoja, sasa basi kama sheria haikurekebishwa tuwafungeni hao watu si hivyo sheria ifanyiwe marekebisho. Hilo ni jengine.

Mhe. Spika, wakati huo huo naunganisha pamoja na sheria hiyo ya vitambulisho kwamba nayo ifanyiwe marekebisho ili wananchi wapate sehele nikisema sehele ni unafuu msije mukaniuliza ni nini, wa kupata hivi vitu kwa sababu ni haki zao za msingi.

Mhe. Spika, nirudi tena suala la vizazi na vifo. Mheshimiwa kule Micheweni bado usumbufu upo wa vizazi na vifo kwa sababu gani? Kwa sababu zile *machine* za kupatia vile vyeti vya kuzaliwa zimeharibika karibu mwaka wa pili huu, watu wanatumia *machine* moja ya kuazima. Kwa hiyo, Mheshimiwa nakuomba sana mufanye jitihada kama iwezekanavyo mutupelekee *machine* za kutolea vyeti vya kuzaliwa ili wananchi wasipate usumbufu kama wenzetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala hili la huyu wakala wa usajili wa biashara na mali. Mheshimiwa hili ni suala zuri sana kusajili biashara na mali lakini ninavyoshauri watu wapewe elimu, kwa sababu hizi biashara haziko mijini tu, biashara zimeenea mpaka vijijini na mali ziko vijijini, sasa watu wa vijijini hawana elimu hii. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa ofisi yako iteremke mpaka kule Wilayani, Majimboni, na Shehia ili watu wapewe elimu waweze kusajili hizo mali zao pamoja na hizo biashara zao. Hili nakuomba sana Mheshimiwa hakuna kitu kikubwa kama kuwapa watu elimu wakajua wanalolifanya, kama watapewa elimu watu basi watakuja kwa wingi kusajili hizo mali zao na biashara zao.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka kulizungumza ni wakfu na mali ya amana. Mhe. Spika, Zanzibar zamani ilikuwa watu wengi wanawekeza kwenye wakfu na mali ya amana kutoa kupitia misikiti na madrasa, sasa nauliza Mheshimiwa hii wizara yako je, imefanya utafiti na kuratibu kujua wakfu zilizopo? Kama haipo basi naomba wizara yako ifanye bidii iteremke na ifanye utafiti na usajili wa kujua kila pahali penye wakfu na mali ya amana.

Suala jengine ninalolizungumzia kwenye hii wakfu ni kwamba hawa wafanyakazi wanalalamika kwamba na wao nyongeza hizi za mishahara hawapewi, wanaambiwa kwamba wao hawamo. Kwa nini wasiwemo? Mheshimiwa naomba wizara yako isimamie hawa na wao wapate haki zao kama wizara nyengine wanavyopata haki zao, kwa sababu nao wanafanyakazi masaa 24, kwa hiyo ikitokea faida wapewe na ikitokea hasara wapate kwa pamoja.

Mhe. Spika, nilikuwa na hayo baada ya kujibiwa masuala yangu nitaunga mkono na sizuii kifungu cha aina yoyote ile.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Subhanahu Wataalah aliyetujaalia leo kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli zetu hizi.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kunipa fursa hii yakuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kweli kwa kutuletea hotuba nzuri pamoja na watendaji wake, lakini vile vile nimpongeze kama kitabu chake kinavyoanisha kwamba kuna mengi ambayo katika kipindi hiki cha mwaka 2013/2014 yamefanyika chini ya uongozi wake Mhe. Waziri. Kwa hiyo, nampongeza sana.

Mhe. Spika, nianze moja kwa moja katika ukurasa wa 11. Mhe. Spika, katika eneo la Mahakama kwenye kipengele cha 35 kinazungumzia masuala ya Mahakama za Watoto. Mhe. Spika, tunakumbuka hapa nilileta hoja binafsi inayohusu masuala ya udhalilishaji wa watoto na katika maazimio hayo Mhe. Waziri aliahidi kwamba kutokana na makubaliano ambayo yalifanyika katika mkutano siwezi kuukumbuka, lakini ni Zaire walikubaliana kwamba kuwe na Mahakama ya Watoto na akaahidi kwamba ipo na kitakuwepo kitengo hicho ambacho kitasaidia katika kesi za udhalilishaji wa watoto. Hasa kwa kuwa kesi nyingi zilikuwa hazipati hukumu zake, pamoja na hilo kwamba limefanyika lakini kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Spika, Mahakama hii bado haijafikia lile lengo ambalo tumelikusudia.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2013/2014 pamoja na zile kesi nyengine ambazo zimechukuliwa ambazo zinasema kwamba idadi yake ni 56 za miaka ya nyuma lakini pia walipokea mpya 23 ambapo imefanya hizo ziwe 79. Ni kesi 4 tu ambazo kwa kweli zimeweza kupata hukumu, zilizobakia zimekosekana mashahidi. Sasa mimi nina wasi wasi

Mhe. Spika kwamba kama kukosekana kwa mashahidi katika kesi hizo 79 ni 4 tu ambazo zimeweza kutolewa hukumu, basi kuna matatizo Mhe. Waziri na matatizo haya niseme kwamba ni makubwa haiwezekani kuwa karibu asilimia 90 na zaidi kesi hizi zisiwe na mashahidi hasa kwa sababu sasa hivi elimu kubwa inatolewa kuhusiana na masuala haya.

Mhe. Spika, zaidi tunataka kujua kuna tatizo gani zaidi ya hili kukose mashahidi? Pia na ofisi yako imejipanga vipi kuhakikisha kwamba haya matatizo yanaondoka? Kwa sababu kuna jengine tunasikia kuna mfano wa kesi moja ambayo ilikuwa tofauti yake ni kwamba yule aliyedhalilishwa amesema alivaa shuka, lakini mwenyewe ambaye aliyedhalilisha amesema amevaa seruni. Sasa tofauti ya shuka na seruni imefanya kesi ile ishindwe, kwa sababu haina ushahidi.

Kwa hiyo, kesi ile imeshindwa! Jamani shuka na seruni inaweza kutofautiana katika kusema mimi naweza nikaliita shuka mwenzangu akaliita seruni lakini itakuwa ina maana ile ile. Sasa Mheshimiwa ndiyo yale ambayo tunazungumza hizi sheria na nyinyi wana sheria ni mahodari sana, wanasheria mahodari kwa sababu wanaweza wakapindisha kitu wakakifanya kile kitu basi ikawa kimekuwa tofauti. Sasa hili kwa kweli litasababisha matatizo na linavunja moyo sana wananchi na ndiyo maana utakuta tunakosa ushahidi kwa sababu wananchi wanaona bado hatua hazichukuliwi, wananchi wanailaumu sana serikali.

Sasa mimi ningeiomba sana wizara yako, pia ningekuomba wewe binafsi kwa sababu Mhe. Waziri nakujua sana namna unavyoumwa na hizi kesi, nakujua sana tumeshawahi kuzungumza zinakuuma lakini bado hizi kesi Mhe. Waziri zinatushinda, kwa nini?

Mhe. Spika, naendelea katika ukurasa wa 14 nichukue fursa hii Mhe. Spika kwanza kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu. Nampongeza Mwanasheria Mkuu kwa sababu kwanza katika mambo yake ambayo alijipangia kuyafanya asilimia kubwa yamefanyika. Tumeona hapa aliahidi kwamba atatuletea miswada na kwa bahati nzuri miswada sita ilifika kwa wakati katika Baraza la Wawakilishi na tukaipitisha. Vile vile ameweza kufanikiwa kuanzisha ofisi za vitengo vya usimamizi wa mikataba, usimamizi wa kesi pamoja na vitengo vya uandishi wa sheria.

Mimi nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kweli kwa kazi zake anavyozifanya vizuri, lakini vile vile ameweza kutusaidia katika kupitisha miswada ambayo ni muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli zetu za utendaji katika mawizara yetu.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye ukurasa 17 katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, hili limezungumzwa na wengi na mimi nitalizungumza na kwa sababu ni suala nyeti ambalo kwa kweli linahitaji kuzungumzwa sana. Suala hili likiwa litaendelea hivi hivi basi bila shaka Mhe. Spika kutakuwa na tatizo kubwa sana katika utekelezaji wa sheria zetu tulizonazo.

Mhe. Spika, tuna sheria hapa za aina mbili; kuna sheria ambazo zilitungwa kabla hata ya Mapinduzi bado zipo na zinaweza kutumika kwa sababu hazina mbadala mwengine, lakini kuna sheria ambazo zimetungwa baada ya Mapinduzi na BLM. Kuna hizi sheria ambazo tumezipitisha sisi, sheria hizi zote ukizitizama kwa sababu ya mabadiliko mengi sheria hizi nyengine zimepitwa na wakati na hilo ndiyo linalosababisha sheria hizi kwamba haziwezi kutekelezeka.

Mhe. Waziri hili ni tatizo kwa sababu mara nyingi sana tunapoingia kwenye sheria na kujaribu kutafuta haki, ndani ya sheria hizi tunazikosa kwa sababu sheria zenyewe zimepitwa na wakati. Sasa mimi ningeomba sana Mhe. Waziri katika mipango yako ya mwaka huu basi uhakikishe kwamba kwa kweli tunafanya *amendment* ya sheria zetu nyingi. Lazima tufanye *amendment* ili sasa na hii Mhe. Waziri nikwambie kwamba inasababishwa kutokana na sheria zetu kwa mfano kama sheria za barabara; sheria za barabara ukitizama makosa yanafanyika, watu wanafika kuua lakini mtu kifungo chake anachofungwa hakistahiki kulingana na kosa alilolifanya.

Sheria za barabara utaona kwamba watu wanalipishwa anatakiwa alipe fidia lakini fedha ambayo anatoa ni ndogo mno. Sasa na serikali pia inakosa mapato kutokana na wahalifu na hilo nafikiri Mhe. Waziri wa Fedha atakubaliana na mimi. Moja katika njia ya kupata mapato ni kutokana na wale watu ambao wanakiuka sheria, na mtu akishakiuka sheria inabidi alipe. Lakini sasa ikiwa sheria zenyewe zina ulegevu fulani mtu anafanya kosa kubwa lakini anapigwa faini ya shilingi 30 au shilingi 5000 hata yule ambaye anamshtaki basi hana nguvu. Askari barabarani hawana nguvu

kwa sababu hiyo. Kwa sababu sheria zetu kwa kweli sasa hivi zimepitwa na wakati, kwa hiyo ningekuomba sana Mhe. Waziri hili ulifanyie kazi kuhakikisha kwamba sheria zetu sasa hivi ziko kwa wakati.

Mhe. Spika, nazungumzia ukurasa wa 20 ambao unazungumzia Mkurugenzi wa Mashtaka, mimi nina masikitiko makubwa; Mkurugenzi wa Mashtaka tunamfahamu vizuri, tumekuwa naye katika kipindi kirefu ndani ya Baraza hili na tunafahamu ari, mori na uwezo wake wa kufanya kazi. Lakini bado kuna malalamiko mengi hasa kuhusiana na ofisi hii, tatizo ofisi hii ni namna inavyoingiziwa fedha. Kwa kweli kuna matatizo makubwa fedha anayoingiziwa ni kidogo na hii inasababisha ofisi yake inashindwa kutekeleza kazi ambazo imepangiwa kutekeleza.

Mhe. Spika, nasikitika kusikia amepangiwa kuwa na ofisi ndogo ndogo katika wilaya, lakini kwa bahati mbaya sana ofisi zile bado hazijawepo baadhi ya wilaya na hii inasababisha watu wake kufanya kazi ndani ya gari. Nataka kusema kumekuwa na *mobile office*, sawa siku hizi kuna maduka ya *mobile* unaweza ukanunua kitu gari inatembea mitaani, lakini hata ofisi ya mashtaka iwemo ndani ya gari? Kwa kweli hiyo ni aibu na inaweza kusababisha kitu kibaya, rushwa!

Mhe. Waziri nakwambia hilo linaweza kutokea, rushwa itafanyika kutokana na kwamba hakuna ofisi eneo maalum la watu wale kufanya kazi na kuweza kuchukua ushahidi wa watu mbali mbali. Kwa hivyo, ningekuomba sana na najua katika bajeti hii kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuziimarisha hizi ofisi za wilaya, lakini hata hivyo, ningeomba sana kwamba uingizwaji wa fedha hizi zinapoingizwa basi ziende katika yale maeneo yaliyoelekezwa.

Mhe. Spika, niendelee kwa kutoa pongezi katika idara hii kwa utoaji wa mafunzo na utafiti wa sheria katika nyanja mbali mbali za sheria. Mhe. Waziri nilikuwa nataka kujua kwa sababu hapa inaonesha kwamba kutakuwa na mafunzo ambayo yatakuwa yanatoa mpaka shahada. Sasa nilikuwa nataka kujua chuo hiki sijui kimekuwa *attached* na chuo chengine gani kikuu hapa Zanzibar na kama vyeti vyake vinatambulika. Nilikuwa nataka kujua hilo na kama hakijawa *attached* na chuo chochote kikuu cha Zanzibar sasa mimi naona wakati umefika wa kuweza kukipa uzito hiki chuo. Kwa sababu nikitizama hapa katika mafunzo ambayo yanatolewa kwa kweli ni mafunzo muhimu sana, wataalamu hawa ambao ni wa uandishi wa sheria Mhe Waziri anajua kwamba hata sisi hapa Baraza la Wawakilishi tunawahitaji sana.

Vile vile wanapewa mafunzo katika *public service law* ambayo tunahitaji sana kwenye masuala ya *drafting* pia. Lakini kuna umuhimu mkubwa wa kwamba watakapomaliza masomo yao basi vyeti vyao vitambulike kitaifa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nitakwenda katika ukurasa wa 24 unaozungumzia Ofisi ya Mufti wa Zanzibar. Kwanza niipongeze vile vile ofisi hii na niipongeze kwa hatua ambayo wameichukua ya kusajili vyuo pamoja na misikiti. Moja katika jambo ambalo nilikuwa nikilizungumzia kwenye bajeti mbali mbali ni suala zima la kwamba vyuo vingi tulivyonavyo katika maeneo yetu havijasajiliwa, hivyo vinakuwa havitambuliki. Kutokutambulika vyuo hivi inaweza kusababisha kuleta ile hatari ambayo tunaizungumza ya kwamba watoto wanadhalilishwa na watu ambao hawatambulikani kama wanafanya kazi ya kukaa na watoto hawa. Kwa sababu unapokuwa unafanya shughuli ya kushughulika kama unasomesha watoto basi lazima utambulikane na vyombo vya serikali kama unafanya shughuli ile. Sasa kwa bahati mbaya sana vyuo vyetu vingi havijakuwa vikitambulika kwa muda mrefu. Tuna imani ile ile ya zamani kwamba mwalimu fulani tunamjua, watu wanampelekea watoto lakini kumbe watu wamebadilika na matokeo yake tunasikia kwamba walimu wengi ndio wanaoharibu watoto wa kike na wakiume.

Kwa hiyo, mimi nimeshukuru sana kwamba hili linaendelea kufanyika na ninaomba lifanyike kwa kina kabisa, lisiishie tu katika ku-*register* hivi vyuo, lakini liende mpaka ku-*register* walimu ambao wanasomesha vyuo hivi na kuwajua wao pamaoja na familia zao, ili kuhakikisha kwamba tunawaweka na tunawakinga; tunawawekea usalama watoto wetu.

Jengine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la maadili, mmong'onyoko wa maadili. Suala hili limezungumzwa na wengi na mimi nataka kulitilia mkazo na naomba sana wizara niipe kazi na watusaidie wenzetu. Wenzetu wana uwezo mkubwa wa kushawishi wananchi na kuona kwamba hali ya maisha yetu hapa Zanzibar inabadilika, maadili yetu yanaporomoka kwa nguvu sana, na wao wana uwezo mkubwa ambapo wanaweza kusaidia katika kutoa ushauri lakini vile vile vipindi mbali mbali ambavyo vinaweza kusaidia angalau kuweka maadili katika hali nzuri.

Mhe. Spika, tunazungumzia suala hili ambalo ni la udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji. Nataka kumuomba sana Mufti kwamba wapewe mafunzo watoto wetu kuheshimu watu wote, kumekuwa na matatizo sana siku hizi. Mwanamke unapopita katika maeneo fulani ukikuta vikundi vya watoto wanaume wanaanza kusema maneno ya ovyo, watoto wetu tuliowazaa wenyewe lakini wanazungumza ovyo wanaweza kumzomea mtu, wanaweza kufanya jambo lolote lile. Heshima zamani haikuwa hivyo watoto wanaume wakikaa kwenye vigenge lakini mwanamke hapiti akahesabiwa namba, sasa hivi mtu akipita anaanza kuhesabiwa hamsini mia, hamsini mia, kumbe yule mtu anapigiwa hesabu.

Mhe. Spika, hilo ni kweli linatokea, sasa utaona kwamba maadili yetu yameporomoka si jengine lolote, badala ya kukaa watoto kuwaza au kufanya mambo mazuri wao wanafikiria mambo ambayo hata hayamo ndani ya umri wao. Kwa hiyo, naomba sana suala la maadili litiliwe mkazo katika ofisi hii ili tupate jamii nzuri.

Suala jengine nasikitika sana sasa hivi kuona kwamba utakuta watoto wadogo wa kike wameachwa wajane. Mheshimiwa talaka za watoto zimekuwa nyingi, mara nyingi sana mimi kinachonishangaza ni kwamba wanawake sisi tunapewa mafunzo tunapoingia kwenye ndoa tuwe wavumilivu, tuwe wastahamilivu, tuwe hivi, tunapewa na ndio maana ukawakuta wanawake wanakuwa wastahamilivu sana kwenye ndoa, lakini wanaume hawapewi.

Mhe. Spika, hilo ni tatizo ndio maana maadili yetu yanaporomoka, wanaachwa watoto hawana wazee, baba anatoka watu wanaitumia Dini ya Kiislamu vibaya na matokeo yake tunapata watoto wa mitaani, tunapata wanawake ambao wanafanya mambo ya ajabu kwa sababu ya hii tabia iliyoko sasa hivi. Mhe. Mufti pamoja na wafanyakazi wake na ofisi nzima wafanye kazi,waokoe ndoa tupate jamii nzuri.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nimemaliza nakushukuru sana kwa kunipa muda huu, mimi nasema tu kwamba naunga mkono hotuba ya waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante sana, nakushukuru.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Mgeni Hassan Juma najua ulikusudia kusema kwamba baadhi ya wanaume si wastahamilivu. Haya, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata fursa hii ya kuzungumza machache juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii kusimama mbele ya Baraza hili. Pia nikupongeze wewe kunipa nafasi hii, kadhalika nimpongeze waziri na watendaji wake wote katika ofisi yake kwa kazi nzuri waliyofanya kutuandalia kitabu hiki kilicho mbele yetu.

Mhe. Spika, mimi nianze katika muhtasari wa fedha walizoomba katika wizara, walizopata kwa miezi tisa iliyopita na kile walichokuwa hawakupata kwa miezi tisa. Wizara hii ni wizara moja muhimu sana kwa sababu ina mambo mawili muhimu; ina katiba na sheria, bila ya sheria tutakwenda ovyo. Kwa hivyo, hii ni wizara ambayo pamoja na ugumu wa kifedha uliopo ilikuwa bajeti yao itekelezwe vizuri kwa sababu ni wizara ambayo inasimamia mambo ya sheria na katiba na pengine mmong'onyoko wa maadili ni kwa sababu ya taaluma ndogo za jamii kuhusu masuala yetu ya kisheria. Sasa ili sheria ziweze kusimamiwa, ili wizara hii iweze kufanya kazi zake barabara ile bajeti wanayoomba ni vyema ikatekelezwa vizuri kidogo.

Mhe. Spika, katika bajeti yale matumizi yanayoambiwa matumizi mengineyo ndio hasa yanayotumika katika ofisi. Ofisi hii kwa kipindi cha miezi tisa iliyopita wamepata asilimia 41 tu ya hiyo matumizi mengineyo, kwa hivyo, utendaji wao kadhalika utakuwa mdogo. Sasa wao itakuwa hawalaumiki sana kwa sababu nyenzo moja kubwa ya utendaji ni hii fedha ambayo hawakuipata vizuri. Ningeomba katika kipindi kinachokuja cha mwaka huu wa 2014/2015 wizara hii iangaliwe vizuri.

Mhe. Spika, nianze ukurasa wa 24 hadi 28 unaozungumzia Ofisi ya Mufti, nianze katika kifungu cha 72, naomba ninukuu kidogo mpaka nifike pale nilipokusudia tu. "...Ofisi ya Mufti imetekeleza malengo yake ikiwemo kufanya Mikutano ya Baraza la Maulamaa, Kuratibu na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi, Kufanya ziara Misikitini na Vyuo vya Qur-ani,...". Hapa nililokusudia ni huku kuandama kwa mwezi, pengine mimi

itakuwa nimefahamu sivyo kidogo hapa. Nadhani Mhe. Waziri wakati wa kujibu kama dhana yangu sio anaweza kunirekebisha. Nadhani wamekusudia kuandama - kuingia kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, hapa tuna tatizo kubwa sana, kuingia kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kutoka kwake. Kwa kweli hapa Waislamu tumegawika na kila mmoja katika mgawanyiko huo anajiona vile anavyofanya yeye ndio sahihi na mwengine anafanya sivyo na tunafika kuambiana maneno ya kiajabu ajabu, kuitana hata makafiri kutokana na mgawanyiko huu wa imani unapoingia Mwenzi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, wale ambao wanatangulia siku moja au mbili wanaonekana wanafunga kabla ya Ramadhani kuingia, hivyo wanaonekana kuwa wanaitanguliza Ramadhani kabla ya wakati wake. Kwa upande mwengine na wao wanaona wale ambao hawafungi wanakula mchana Mwezi wa Ramadhani ambapo ni hatari kweli kweli kuwa mwezi wa Ramadhani ushaingia ukawa hukufunga.

Kadhalika wao waliotangulia watamaliza Ramadhani mwanzo, kwa hivyo, hili kundi jengine wataona kuwa hawa wanakula mchana mwezi wa Ramadhani kitu ambacho hakikubaliwi. Wao wataambiwa hawa wengine kuwa mnafunga siku ya sikukuu ambapo ni haramu kufunga siku ya sikukuu. Kwa hivyo, kambi mbili hizi za kidini ndani ya Zanzibar zimeleta mgawanyiko katika dini yetu; dini ambayo lengo lake ni kuwaweka Waislamu pamoja lakini hapa tunagawika, sijui ofisi hii inachukua hatua gani kuhusu suala hili na kila mmoja anavyofanya anajiona ni sahihi kwa sababu aliyetangulia anatumia aya hiyo hiyo na anayechelewesha anatumia aya ile ile, hakuna anayetumia aya nyengine. Wanatumia aya inayosema fungeni kwa kuuona na kadhalika, kila mmoja anatumia aya hiyo.

Mhe. Spika, hili ni tatizo kwa sababu ni tatizo la kidini. Mara moja kuna Sheikh mmoja mkubwa ambaye ameshakufa hivi sasa Sheikh Abrahman Msaada alikuja siku moja Kengeja, katika kuzungumza kwake tatizo kama hili anasema walizungumza katika Kongamano la Kimataifa. Waisilamu tunapohitilafiana tufanye nini? Wakazungumza walivyozungumza hatimaye wakafikia *conclusion* ambayo ni sahihi, tufuate Qur-ani na hadithi za Mtume Muhammad (*S.A.W)*, hapo ndio *top.* Sasa kwa kuwa Wazanzibari ni wasomi barabara watu wanakunja vitabu yeye akanyanyua mkono akauliza swali lake moja tufuate Qur-ani na Hadithi kama alivyofahamu nani? Kwa sababu kila mmoja anavyofanya anajiona anafuata Qur-ani na Hadithi, je, hapa tufuate Qur-ani na Hadithi kama alivyofahamu nani?

Mhe. Spika, hapa hapakuwa na jibu na kwa wakati huo Zanzibar ilikuwa na wasomi wakubwa kweli kweli, masuala wakati mwengine yalikuwa yanashinda Al-Azhar Chuo Kikuu cha Misri yakija Zanzibar yakajibiwa.

Mara moja kuna suala fulani ambalo lilishinda kule mashekhe wakaagiza liletwe Zanzibar basi Wazanzibari walijikuna kichwa kidogo tu wakatoa fat-wa iliyo sahihi, Al-Azhar wakakaa kulitafakari wakaona jibu hili ndilo na waliamua kuipa zawadi Zanzibar kuwajengea tawi la chuo chao cha Al-Azhar hapa Zanzibar, kama ni heshima ya elimu waliyonayo Wazanzibari. Lakini kwa bahati sisemi mbaya, kabla ya utekelezaji wake yakatokea mabadiliko ya kiutawala, kile chuo hakikujengwa tena. Lakini kilikuwa kinajengwa kwa sababu ya elimu iliyopo Zanzibar. Zanzibar ilikuwa ni chemchem ya dini ya kiislam. Leo Mhe. Spika, wale ambao walitoka kule kuja kusoma Zanzibar elimu iliyopo, leo sisi Wazanzibari mtu akitaka kusoma dini kweli kweli lazima atoke aende kule ambapo zamani ilikuwa wao ndio wanaofuata. Hilo Mhe. Spika, nilikuwa niseme hivyo na nimuulize Mhe. Waziri, ofisi hii inafanyaje kujaribu kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, niende kwenye *paragraph* ya 74 na hapa kuna kitu natafuta kidogo ambayo mwenzangu Mhe. Mgeni Hassan Juma kalizungumza sana. "Vipindi hivyo zaidi vilihusu mambo yanayoathiri jamii yakiwemo masuala ya ndoa na talaka, mmong'onyoko wa maadili katika jamii, udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji.

Kwanza niipongeze ofisi kuwa wanashughulikia mambo haya. Mhe. Spika, kuna miezi Wazanzibari tunauona kwa wingi sana, lakini kuna miezi kama ndoa zilizofanyika, pia ndoa vile vile zinaporomoka kwa wingi sana. Hapa ni kwa sababu wafunga ndoa wawili hawana elimu hii ya ndoa. Kijana kajiona kuwa niko *fit* nahitaji mke kumbe hamuwezi, baada ya siku kadhaa kagombana, kampiga mateke, kwenu. Hapa ni kwa sababu ya ukosefu wa elimu hii ya ndoa. Mhe. Spika, wengine wanaoa kwa shinikizo, vile vile ndoa ya aina hii haina maisha mazuri.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma kazungumzia huu mmong'onyoko wa maadili ambao kila dakika tunayokwenda unaongezeka badala ya kupungua. Mhe. Spika, jinsia hizi mbili za kike na kiume moja wapo ni

pleasant flower, ni ua zuri sana, na nyengine ni mdudu ambaye anasaka asali. Sasa ua linatembea katika ile hali Mhe. Mgeni aliyoisema hamsini mia, hamsini mia, lazima mtu atafuata. Hapa mmong'onyoko wa maadili unatokea. Kwa hiyo tuna kazi kubwa Mhe. Spika, ya kuelimisha jamii katika masuala haya.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nije katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, Tume hii ni muhimu na ningeiomba ichunguze sheria zote ambazo zimepitwa na wakati ili zirekebishwe, na zile sheria ambazo kwa namna moja au nyengine zinamkosesha mwananchi haki yake fulani. Mhe. Spika, ningeiomba Tume hii irekebishe sheria mbili, moja inayohusu Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, na moja Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Ningeomba sheria mbili hizi ziangaliwe na zifanyiwe marekebisho. Kwa sababu hii ya uchaguzi ina hadhi kubwa mno. Mahakama haithubutu kupeleka mkono wake kwenye matatizo ya kiuchaguzi. Mahakama ambayo ilikuwa haina pa kukimbilia, lakini kwenye kesi ya kiuchaguzi Mahakama inakimbia inaogopa Tume ya Uchaguzi na maamuzi yake. Kwa hiyo sheria hii ambayo ipo juu kuliko Mahakama ningeomba itazamwe na ifanyiwe marekebisho.

Mhe. Spika, jengine ni la Vizazi na Vifo; hapa waliosajiliwa waliozaliwa wanaume ni wengi kidogo kuliko wanawake, na pia waliokufa wanaume ni wengi kuliko wanawake. Lakini hawa waliokufa ni kidogo sana, wengi walikufa lakini udogo wao ni kwa sababu hii elimu ya kusajili waliokufa bado ni nyembamba mno, watu wengi hawajakuwa na umuhimu wa kuona kuwa mjomba, shangazi, bibi au babu kafariki tukamsajili. Isipokuwa ni mtu anafanya kazi Serikalini wakamsajili kwa kutaka ile mirathi ya haraka haraka zile haki zake za Serikalini. Vyenginevyo wengi wetu hatusajili. Kwa hiyo ningeiomba Wizara hii itoe elimu maalum ya kuwataka watu na wale waliofariki nao pia wasajiliwe, kama watakavyokuwa na umuhimu wa kuwasajili hawa wanaozaliwa.

Mhe. Spika, halikadhalika nimuombe Mhe. Waziri apunguze ada ya hii mtu anapotaka cheti cha kuzaliwa baada ya wakati ambao si wa kwake. Wengi wanakimbia hii ada iliyopo, ikiwezekana ada hii ifanywe nyepesi ili watu waweze kupata hivi vyeti vya kuzaliwa na hatimae waweze kuwa Wazanzibari, yaani wapate kitambulisho cha Mzanzibari.

Mhe. Spika: Muda umekwisha.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Lakini na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake na ufasaha wa hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi nitakuja kwenye Mahakama na majengo. Mhe. Spika, moja kati ya mihimili mitatu mikuu ya hapa nchini kwetu ni Mahakama. Kazi ya Mahakama ni kutoa haki kwa wananchi wake. Kwa hiyo Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri kuna haja ya kuangalia sana majengo haya kwa makini kwa sababu yameshakuwa machakavu na ya kutisha. Vile vile tunasema kwamba ni kama kumbukumbu. Mhe. Spika, kuwa na kumbukumbu kwa majengo haya ni vizuri katika nchi yetu na nchi inataka angalau ionekane majengo yalivyo mazuri kama nchi za wenzetu. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie sana.

Mhe. Spika, jengine naipongeza sana Ofisi ya Mufti kwa kuweza kusimamia vyema shughuli za kidini pamoja na kutembelea vyuo kadhaa vya Zanzibar. Mhe. Spika, kwa kweli vyuo hivi ni muhimu sana katika kusimamia mafunzo pamoja na maadili ya watoto wetu katika misingi ya kiislam. Pamoja na hayo Mhe. Spika, niseme kwamba kuna walimu kwa hivi sasa ambao wanasomesha katika vyuo hivi hawana uwezo. Nimuombe Mhe. Waziri awasaidie japo pesa ya sabuni walimu wetu wale wanaowafundisha watoto wetu kwa sababu jambo si dogo wanalolifanya.

Pia Mhe. Spika, nije katika matatizo ya vyuo; kwanza majengo mengi ya vyuo vyetu ni mapungufu, mengi hayana vyoo. Vile vile Mhe. Spika, niseme maeneo ya kusomea yaliyotenganishwa baina ya watoto wa kike na wa kiume pia ni tatizo. Mhe. Spika, ili maadili ya kiislam yapatikane ni lazima vyuo vyetu vya Qur-an viweze kutenganishwa baina ya wanawake na wanaume.

Mhe. Spika, lakini pamoja na hivyo, tatizo la pili tabia mbaya ya baadhi ya walimu wanaosomesha katika madrasa. Walimu wa madrasa Mhe. Spika, wana matatizo ya kuwaharibu wanafunzi wao. Hili ni tatizo kubwa Mhe. Spika, kwa baadhi ya walimu wa madrasa. Mhe. Spika, pia walimu hawa wanaweza kuwadhalilisha wanafunzi kijinsia.

Hili Mhe. Waziri aliangalie sana kwa sababu walimu hawa wanavyo vitendo kama hivyo jambo ambalo ni kinyume na maadili ya kiislam.

Mhe. Spika, niseme kwamba Mhe. Waziri jambo hili ni lazima Ofisi ya Mufti iwe makini kwa vyuo vyenye walimu wa aina kama hii. Pia Mhe. Spika, kuna haja walimu kama hawa wanaobainika kufanya vitendo kama hivi kuchukuliwa hatua za kisheria ili wapate funzo kwa wengine.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 20 nataka Mhe. Waziri anifafanulie kifungu cha 60 (1) kinachosema "Kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar zifuatazo:-" Naomba Mhe. Waziri anipe maneno haya kwa kiswahili kwa sababu wengine si wazungu humu. *"The Succession Decree* sura ya 21/1917, *The External Probates Decree* sura ya 22/1918, *The Vagrancy Decree* sura ya 21/1962 na Sheria ya Utalii Nam. 6 ya 2009 kama ilivyorekebishwa na Sheria Nam. 7/2012". Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie kuhusu suala hilo.

Mhe. Spika, nije katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Spika, ofisi hii ni muhimu sana katika kusimamia mashtaka ya wananchi Mahkamani. Kwa hiyo Mhe. Spika, ofisi hii inatakiwa kuwezeshwa katika suala zima la utendaji. Mhe. Spika, katika ofisi hii kuna matatizo ya wanasheria wa *DPP* Pemba hawatoshi; jambo ambalo linapelekea kuzorota kwa shughuli zao za kazi.

Pia Mhe. Spika, ofisi za *DPP* za Wilaya, kuna ofisi kama vile Konde, Mkoani na Wete. Mhe. Spika, ofisi hizi hazina kiwango. Namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie sana katika ofisi zetu hizi.
Ukija kwenye usafiri, ofisi hii haina usafiri wa kuwasafirishia wanasheria wetu, hautoshi. Waheshimiwa wenzangu hapa wamelisema sana lakini na mimi nalisisitiza suala hili uliangalie kwa makini. Kwa hiyo mapendekezo yangu Mhe. Spika, Serikali iongeze usafiri pamoja na kuwaajiri wanasheria zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii jioni hii. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa mliyotoa katika kuendesha shughuli zetu. Muda uliobakia si wa kutosha kumkaribisha Mheshimiwa mwengine ili kuchangia. Hivyo tukubaliane kwamba shughuli hii iendelee kesho asubuhi, lakini tukielewa kwamba asubuhi hiyo hiyo Mhe. Waziri tutamuomba afanye majumuisho. Kwa hiyo asubuhi tutakuwa na Wajumbe kama wanne kabla ya kumwita Mhe. Waziri ambao ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Rufai Said Rufai na Mhe. Suleiman Hemed Khamis, nategemea ni pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Baada ya Wajumbe hao tutamwita Mhe. Waziri ili kufanya majumuisho.

Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, sasa naakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 05/06/2014 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:38 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 05/06/2014 saa 3:00 asubuhi)